# LUKA 10

## KAZI TULIYOKABIDHIWA KAMA INAVYOELEZWA NA YESU

**STEVE na MARILYN HILL**

***" Yesu alikuwa kiongozi bora mwenye ujuzi zaidi, ambaye hajawahi kuonekana hapa duniani. Kwa nini basi tuamini kwamba sisi tunao mtindo bora wa kutenda mambo ? "***

# Luka 10

## Kazi tuliyokabidhiwa- kama inavyoelezwa na Yesu

**C 210** Kimeandikwa na **Stephen na Marilyn hill**

**Harvest-now**

**35 colony trail Boulevard**

**Holland Landung, Ontario**

**L9N IC6**

**(905) 836 8943**

www.harvest-now.com

stevehill@harvest-now.com

ISBN

**Mtafisiri Guillaume Kachuba**

**Msahihishaji : Mwene Inga & Bahati Chantal**

***Maneno na vifungu vyote vya Biblia vimekunuliwa kutoka Biblia - Swahili-Union -version 1997 @ Bible societies of Kenya & Tanzania***

***HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA***

# KIFUNGU CHA LUKA 10

## (Ujumbe kama ulivyoamriwa na Yesu)

## Yaliyomo:

**Dibaji:**

**Utangulizi:**

**1) Tatizo La watenda kazi**
- A) Tatizo la moyo
- B) Tatizo la maandalizi (matayarisho)
- C) Tatizo la Maono wala kulaumu mavuno

**2) Maombi na tatizo la kijeographia**
- A) Maombi yanayopotea
- B) Bwana wa mavuno
- C) Maombi kama tulivyoamriwa

**3) Hatari iliyo mbeleni**
- A) Inafikiriwa kuwa ni hatari
- B) Maisha ya Yesu inadhihirishwa kupitia mateso
- C) Tumebarikiwa ili tuwe baraka

**4) Mkoba wa pesa, kikapu, viatu & kusudi**
- A) Mkoba wa pesa na misheni
- B) Mkoba wa pesa na mila
- C) Viatu na mbinu
- D) Habari ya mwanapunda
- E) Salamu na kusudi lake

**5) Amani yenu na mwana wa Amani**
- A) Amani iwe nanyi
- B) Kumpata mwana wa Amani

C) Vipi kuhusu mila ya kisasa na ile ya magharibi ? ulaya)

**6) Agizo kuhusiana na kula na kunywa**

A) Kukaa: uaminifu katika uhusiano na kuongezeka

B) Kula, kunywa na kukubaliana , kuwa muhusika, mwenendo na imani

C) Kuustahili mshahara na matatitizo mengine yanohusiana na majukumu

**7) Kutangaza na kuhudhihirisha ufalme**

A) Ponyeni wagonjwa na Mdhirishe ufalme

B) Tangazeni na mkautangaze ufalme

C) Nani anayehusika?

D) Daima kama mtumwa, na wala sio kama mfalme

E) Yesu,kichwa kamili,na wala sio kichwa cha maumbile tu

**8) Kukataliwa/kukubali ukweli wa Mambo**

**9) Kufurahia uhusiano**

A) Mamlaka yote

B) La muhimu zaidi ni ushirikiano

C) Ninawaita ninyi marafiki

D) Majukumu na uhuru wa urafiki

**Apprendix #1**, Mitume , watumwa wa Kristo

**Apprendix #2**, Makanisa ya nyumbani katika Agano jipya

**Apprendix #3**,Mojawapo wa zile Amri

**Apprendix #4**,Huduma ya wakati wote na pesa katika Agano jipya.

# DIBAJI

## Ushuhuda kutoka Grâce

## ( mhudumu mpya )

Namshukuru Mungu kwa sababu ninampenda , namtumikia na kumtukuza. Nimejaa furaha tele kwamba Bwana amenichagua kueleza yale ameyatenda mwaka huu. Miaka mingi imepita tangu nilipoyatoa maisha yangu kwa Yesu, lakini ni mwaka huu tu ndyo macho yangu yamefunguliwa kwa ule ukweli mkuu wa Yesu, kwamba mimi ni binti mpendwa wa Mungu na kwamba ana kazi anataka mimi kufanya. Mwaka jana nilikuwa nikimlilia Bwana anisaidiye maana nilikuwa na mahitaji makubwa. Nilikuwa nimeshakuwa mvuguvugu, furaha yangu ilikuwa imetoweka na sikuwa na msaada wowote wa kiroho. Ndipo nikakutana na dada A ambaye nilimfahamu kwa muda mrefu. Tulizoea kwa pamoja kwenda kanisani kabla ya mimi kuondoka kwenda Kazakhastan na baadaye Rusia kwa ajili ya kazi.

Nilibatizwa Rusia na niliporudi hapa, niliendelea kuhudhuria kanisa.

Nilipomwona A nilishangazwa maana alionekana kukomaa kiroho dhidi yangu mimi. Nilivutwa sana na uchangamfu na upendo wake kwangu hata nikamuuliza kama amekuwa mchungaji .

Akanijibu kwamba hapana lakini yupo katika kundi moja lijulikanalo kama kanisa la nyumbani na kwa wakati mwingine huwa anaenda hata inje ya mipaka ya mji wao na wanajihusisha hasa na kuzidisha makanisa popote incini mwao hata na inje ya inci.

Kwa kweli nilikuwa na masito kwa mwaka wote mzima. Inawezekanaje kutoshiriki pamoja jumapili, kutomsikiliza mchungaji aliyepakwa mafuta ? inawezekanaje kwa mtu kama mimi asiyekuwa na elimu yoyote ya kiroho kuwa na uwezo wa kuelewa Biblia na hata kuyaanzisha makanisa mapya ?

Ndipo nikaanza kuwatembelea na kuhudhuria katika mikutano yao mara kwa mara na nikaona uzima hapo. Kila moja wao alikuwa na uhuru wa kueleza maono na ushuhuda. Hapakuwepo na mahubiri , bali shuhuda mbalimbali zilizokuwa zikitolewa zilionyesha kwamba kila mmoja alikuwa akihudumu kwa familia , kuwatembelea watu katika vijiji, kuwa hudumia na kuwasaidia kwa mahitaji ya kila siku na kuwajali. Chochote walichokisema kilithibitishwa na neno la Mungu. Upendo ulifurika miongoni mwao. Ndipo nikaanza kuomba. Kwa maana Mungu alinipata nilipotaka kupotea na akanipa uzima mpya , nilitamani mara kwa mara kwenda miongoni mwa watu na kutangaza habari njema pamoja na wao. Mwaka huu kupitia shuhuda mbalimbali mara tena nikasikia nguvu za upendo na sauti ya mbinguni. Nikafunguliwa kwa makosa yote na vifungo mbalimbali na ndipo

nikawezeshwa kuomba pamoja na dada yangu aliyekuwa karibu kufa na Mungu akamponya !

Maombi yangu ilikuwa kana kwamba Mungu aniwezeshe kutangaza nuru yake kwa wengine naye alijibu kilio changu. Kwa maana sasa nina wa hudumia watu wengi. Mungu amefungua milango kwa nyumba nyingi na hadi sasa wa nane miongoni mwao wameanza kutusikiliza. Pia nimewahi kutembelea marafiki na ndugu. Kila tunapo kusanyika tunamshukuru Mungu aliye tupa ufunuo kuhusu nyumba ya Amani mahali ambapo moto wa Mungu huchochewa.

Tunawaombea marafiki zetu **Steve** na **Marylin** na **G** na **E**. Mungu awabariki daima katika mambo yenu yote.

## UTANGULIZI

## (Toka tafsiri ya Asia ya Kati)

Ni fursa kubwa kwetu kukuletea kitabu hiki. Acha nianze na kusema kwamba , Biblia, katika mwelekeo wa kimila, yabainika wazi kuwa ni kitabu cha wazungu na hata Yesu mwenyewe alikuwa mzungu ! Ila angalau hata hivo, ninyi wazungu mnaweza kuelewa vizuri mafundisho ya Yesu kuliko mimi.

Hata hivo, acha nitumie mamlaka yangu kama mzungu kufafanua jambo moja.

“ Msilitendee kanisa kama tuliyolitendea sisi huko ulaya kwa miaka 100 iliyopita. Halikutumika vizuri na sisi hata kidogo. Kwa nini basi lingeli tumika kwa yeyote yule ? ”

Kihistoria huwa tunajaribu kuanza kanisa kulingana na mila yetu ya jinsi ya kulifanya kanisa (kiongozi, washirika, jengo, mikutano na mahubiri ya wiki, mikutano ya maombi ,kulitengemeza kanisa kipesa, na kuwa na vikundu vidogo ). Na baaadaye kujenga aina ya misheni kulingana na mtindo wetu wa utendaji wa kanisa. Ule uzoefu na utendaji wa mahali maalum, na wakati maalum ambapo mambo maalum yanapashwa kutendeka na mtu maalum mambo ambayo huwezi kuyatenda mwenyewe ambayo unamlipa mtu maalum kuyatenda kwa ajili yako, ni alama ya dini zote za ulimwengu. Hivo tunapoanza kanisa tunauza na mila zetu kidini.

Wakati wowote tunapoanza na mtindo wetu wa namna tunavyolifanya kanisa , ndipo hiyo namna yetu ya kuelewa misheni inakuwa tu kujaribu kuwapata watu wa kuja kwenye mikutano yetu na kutengemeza mipango ya kanisa kwa kuhudhuria ibada, kujitolea kwa kazi mbalimbali, na kutoa pesa. Na kwa namna hii ni vigumu kuita hiyo kuwa ndyo misheni. Mbaya zaidi katika hali hii ni kwamba matangazo yote hayo yanakuwa na shabaha la kuwavutia wale ambao tayari ni wa kristo, kuja kwako kuliko kuwaelekeza kanisani. Na watu hao walio waaminifu na wenye kuwa na moyo wa kujitolea hufanya yote wawezayo ili watumikie jamii zao kwa njia waliyoizoea kutenda.

Hata hivo,katika mazingira kama haya kuwafanya watu kuwa wanafunzi linakuwa jambo geni lisiloambatana na kanuni yetu ya imani na mpangilio wa mamlaka ya dhehebu letu.

Aina hizo mbalimbali za imani zetu ndyo hutufanya wakati mwingine dhehebu hili kuwa tofauti ao bora zaidi kuliko lingine. Hata hivo mambo yote hayo yanakubalika na kuaminika kwa sababu yana ukweli wake na haki kuliko wengine ambao labda hawana ukweli huo. Na kwa ajili hiyo hawaoni umuhimu wa kumuona Yesu na wafwasi wake kama mwili mmoja.

Kwa kuliweka neno hili katika upana wake, tunaanza na elimu juu ya kanisa ( namna tunavyofanya kanisa) na hiyo hutuongoza kuunda namna ya kufanya umshonari –Namna tunavyofanya misheni ) na mwishowe tunatizama jinsi gani kwa njia moja ao nyingine nama gani kundi hilo la watu linaweza kufikia kiwango cha kumjua Yesu Kristo ( Elimu kuhusu Kristo ). Hii ina maanisha kwamba kanisa na misheni ina onekana kupendeza sana katika kila mila isipokuwa tu tofauti za kidini zinazolekea kuwa kipingamizi katika mila mpya kuliko ile ya hapo kale.

***Albert Einstein*** alisema maneno haya: ***“ kuwa kichaa ni kutenda jambo mara kadha wa kadha huku ukitarajia matokeo tofauti”***

Msemo mwengine ninaotumia ni, ***“ ikiwa tunatenda yale tuyatendayo mara kwa mara, tutapata daima yale tuna yayapata ”.*** Tumetenda kwa ujinga yale tunayo yatenda daima, na huku tukimwomba Mungu jambo tafauti kutokea! Nini kinajitokeza wakati tunapoanza na Yesu? Nini kinatokea tunapomruhusu Yesu kuongoza misheni yetu na kumruhusu Yesu kulijenga kanisa lake ? Ingekuwaje kama

utaratibu ungekuwa ni elimu ya Kristo, umisheni, na mwishowe elimu juu ya kanisa ?

Iweje kama Yesu angelielekeza misheni kwa njia tofauti na ile ya mila zetu na kanisa alilolijenga kuonekana tofauti katika kila mila? Kuyatizama hayo kupitia maneno ya Yesu ndani ya ***Luka 10*** ndyo kusudi la kitabu hiki. Tunapoyatizama maneno ya Yesu kwa miaka mia moja iliyopita ,Maneno yake ilikuwa yenye kulijenga kanisa, utaratibu wote na mpangilio wa kanisa hukubaliana na lile neno. Tunalitumia neno lake kukabaliana na maadili, mapokezi yetu na yale tunayoyatenda. Hii ni ku anguka katika mtego kanisani kama tunavyofahamu. Je ? Kanisa ambalo Yesu analitaka lingefananaje ? Nini kingetokea ikiwa tungeliona kanisa kupitia neno na mfano wa Yesu ?

Labda kama tungetenda yale aliyotumuru kutenda na kufanya mataifa kuwa wanafunzi ( kufundisha mataifa kushika yote aliyotuamuru), angeweza kutenda yale aliyoyaahidi na kujenga (binafsi washirika wa mwili wake na kuwa kichwa halisi kuliko kuwa kama mfano tu wa kichwa cha mwili wake) ambalo ni kanisa lake ?

Vipi kama tungeanza na misheni kama alivyofanya Yesu na kutuamuru kutenda hivo ? Tunakualika kutembea pamoja nasi kwa kuzingatia maagizo na kujihusisha na ***Luka 10.***

# SURA 1

## TATIZO LA WATENDA KAZI

***" Akawaambia, mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache:..." Luka 10 : 2***

### A) SHIDA YA MOYO

Yesu ana tofautisha uwingi wa mavuno na uhaba wa watenda kazi. Hakutuambia kwa nini watenda kazi ni wachache , lakini kutokana na uzoefu unatuonyesha kuwa watenda kazi wanalundamana kwenye maeneo ya inci za watu waliokwisha hubiriwa injili ulimwenguni wakati ambapo sehemu zile ambazo hazijafikiwa na injili, zilizo na waumini wachache zinakuwa na idadi ndogo ya watenda kazi. Hayo wakati mwingine ni kutokana na ile shauku yetu ya kuzingatia usalama wetu, cheo, mshahara, starehe na Amani kwa maana wakati mwingine mambo kama na hayo wasioamini hawawezi kutupea !

Kuvuna wakati mwingine sio rahisi ni vigumu, ni kazi hatari ambayo unayoiendesha kwa gharama yako mwenyewe !

Hilo linatuelekeza kwenye tatizo la moyo wa watenda kazi. Wakati ninajisikia kwamba tunasonga mbele zaidi katika hali yetu ya kumfuata Mungu.

Tunakwenda mbali zaidi ili kusikia upendo wake , kufahamu msamaha wake, kupokea ujuzi kuhusu uponyaji wake.

Kwa kifupi unasikia vizuri lakini sio kwa kiwango cha kuweza kuwa na moyo wa Mungu ili kuyaendea mataifa angalau.

Mungu ni upendo. Upendo wake ni wa kihama , hatari, usiokuwa na mipaka wala woga. Kufanya kazi ya kuvuna ni moja wapo wa kazi ngumu lakini yaweza kuwa pia kazi chafu na hatari.

Mioyo yetu inapashwa kuwa mikuu kuliko yote hayo. Na tunawezafikia yote hayo kama tu tutashikamana kwa umoja na neno lake.

Tunahitaji pia kuwa makini kuhusiana na kizazi hiki kipya cha kiroho na haja yake ya ujuzi wa kiroho kama mwisho wa mambo yenyewe. Wakati akili inapotawala, mambo ya rohoni hupendelewa kuzingatiwa na wamoja kuliko wengine. Katika Agano jipya mambo hayo hayajawahi kutenganishwa kamwe. Kupata ujuzi wa Roho Mtakatifu ndyo msukumo wa maisha iliyojitoa kwa Yesu kupitia utiifu.

***“ Lakini mtopokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho mtakatifu: nanyi mtakuwa mashaidi wangu katika yerusalemu, na katika uyaudi wote, na samaria , na hata mwisho wa inci...(Mdo 1:8) ”*** . Agano jipya lina rikodi ya mambo mengi ya kiroho, lakini haya hayakutendeka kwa sababu watakatifu wa kwanza, wa kanisa la kwanza waliyaona na kuyaishi miongoni mwao. Hakuna mahali katika Agano jipya ambapo mitume walifundisha jinsi ya kwenda mbingu ya tatu, jinsi ya kukutana na malaika ao jinsi ya kuifahamu sauti ya Mungu. Kuna huduma nyingi katika inci za magharibi zinazo kuwa na viongozi wanaodai kuwa na uwezo (kipawa) cha kuwafundisha wengine namna gani wanaweza kupata ujuzi katika mambo hayo.

Wanaeleza kuhusu kwenda mbingu ya tatu sawa na kwenda kwa nyumba ya kupata chakula (hoteli). Haya ni mafundisho ya ziada kibiblia.

Je watu hupata ujuzi wa jambo Fulani katika mikutano ya aina hii? Ndyo wengi hupata , lakini wanapata ujuzi wa kitu gani? kundi kubwa la watu waliochangamka wanaopewa maelekezo ya kisaikolojia na msisimko mwingi sana tu unaofanya watu waamke kiroho lakini matunda yanakuwa madogo. Kwa sababu tu katika Agano jipya watu Fulani walikutana na Mungu hiyo haimaanishi kwamba tuwaige ao tuwafwate wao. Kuna mikutano mingi ya uamsho, na huduma nyingi kwenye Runinga (TV) ya aina hiyo wakati ambapo ni kinyume cha Biblia. Mashairi mengi ya Biblia hayatumiwi tena kwa njia sahihi kama yalivyotumiwa katika Agano jipya.

Hayo ndyo makosa ambayo kanisa la kwanza lilipambana nayo na kuyapiganisha, wakati mtu anapoanza kudai kuwa amepata ufunuo ao ujuzi fulani kutoka kwa Mungu na kuanza kufundisha mambo hayo kama ya muhimu kwa wokovu. Watu hao waliitwa ***“ wanostiki ”***, waliinua sana ujuzi wao wa kiroho kuliko mafundisho ya kawaida kutoka katika maandiko.

Katika Agano jipya, kumjua Mungu hakukupatikana kwa njia tofauti na ile ya kumtii Mungu. Walipokea nguvu za Mungu na hayo yote yalitendeka kupitia mateso na shida lakini hata hivo walichagua kumtii Bwana. Kwa mfano naweza kukubaliana na wengi wanaofikiri kuwa mbingu ya tatu ya Paulo aliyofika

ilitokea wakati ambapo alipigwa kwa mawe na kuachwa karibu kufa inje ya mji wa Lystra ***( Mdo 14:19 )***.

Jambo la kwanza lilikuwa ni kuwa mtenda kazi pamoja na Mungu! Hatupashwi kuwa wanaotafuta tu mambo ya kiroho peke yake.

Tunapashwa kuwa miongoni mwa hao wanaofahamu kuwa tuameifisha dhambi na ubinafsi katika Kristo na sasa tu huru.

Tukijionesha wenyewe kuwa dhabihu iliyo hai kwake yeye. Tunaishi kwa kumfwata Bwana wetu hadi kwa nyumba ifwatayo, kijiji kifwatacho ao inchi inayofwata. Tunatenbea pamoja naye.

## B) TATIZO LA MAFUNDISHO

Hali ya kuwaandaa watu kulingana na mapokezi yetu nayo pia yawezakuwa tatizo. Imetokea kuwa kadiri unapata elimu ya Theolojia kwa miaka mingi kadiri unaweza kuwa na uwezo wa kumleta mtu mwengine kwa Yesu.

Kwa uhakika, shule za Biblia , na vyuo haviwatayarishi watenda kazi, vinatayarisha wajuzi katika lengo la kutunza na kukuza dhehebu. Hao wanaotayariswha, ambao baadae wanafanikiwa kuona wengi wakifanyika wafwasi wa Yesu, mara nyingi hubaini kuwa iliwabidi kutojali sana yale yote waliyojifunza kwa chuo ili wawe wafwasi kamili wa Yesu Kristo, mwalimu wa wanadamu.

Pingamizi lingine ni kuwa kadiri unavyo mchukua mtu toka maeneo yake kwa ajili ya mafunzo , ni wachache mno ambao

baada ya kuhitimu hupendelea kurudi tena kwenye maeneo yao ya kazi. Hili halihusiani kabisa na mila ya wazungu lakini ikiwa unamchukua mtu kutoka inci zisizoendelea na kumfundisha katika mazingira ya ulaya, ao ikiwa ungemchukua mtu kutoka vijijini katika inci zisizoendelea (ulimwengu wa tatu) na kumfundisha mjini. Mara tena masomo hayo kidogo yanalenga kutoa wajuzi ambao wanatamani kuishi maisha ya kiwango cha juu kama watu wenye ujuzi (wasomi).

Aina hii kamwa haiwatayarishi watenda kazi walio na utashi wa kujihusisha katika kazi ngumu ya mavuno na kuishi kwenye shamba la mavuno. Watenda kazi wanatayarishwa kwenye uwanda wa kazi.

Yesu aliwatayarisha watenda kazi kwenye kazi ! Tuna pashwa kuwa wafuasi wa Yesu. Hatuna njia nyingine mbadala (iliyobora)! Yesu aliwatayarisha wavuvi, wakulima kwenye kazi na akaaidi kuwafanya kuwa wavuvi wa watu.

Hakujali sana kuwatayarisha wasomi ao wenye ujuzi wa mambo ya dini.

Alikemea, alilaani na mara kadhaa alikabiliana na wasomi wa kidini wa siku zake zile ( ***Math 23 soma hiyo )*** na angetenda vivyo hivyo hata leo.

Yesu alizungumzia kuhusu mafunzo na kazi katika ***Yohana 1:17, " mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo, kwamba yatoka kwa Mungu ao kwamba mimi nanena kwa nafsi yangu".***

Tunafahamu kupitia kutenda, nidhamu imani na taabu kwa kutenda kazi ndani ya mapenzi yaake huzaa hali ya kumtegemea zaidi pamoja na unyenyekevu wa ndani.

Kuelimishwa kwa kupewa habari za kutosha, ujuzi wa kufahamu vema kanuni  za imani ukweli,kuhusu Biblia na theolojia yaweza kuza kiburi kama ilivyoonekana kwa mafarisayo kwenye maelezo yao katika ***Yohawa 1 :49,"lakini makutano hawa wasio-ifahamu Torati wamelaaniwa ".***

Yesu alisema pia juu ya kutayarisha kwenye uwanda wa kazi katika ***Math 28 : 19-20*** pamoja na amri ya kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi ***" kwa kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru "*** .

Aina mbaya ya masomo (majifunzo)  katika shirika zetu  ni katika zile imani na tabaka mbalimbali za mamlaka ya uongozi wa dhehebu hilo. Hilo huzaa hali ya kutofautiana katika mwili wa Kristo, kujiona bora kuliko wengine maana hali hiyo hupelekea kuamini kwamba kitu chako ndicho bora zaidi kuliko cha wengine.

Kinyume na hiyo amri ya Yesu inatuomba kuwa waamifu katika ushirika kupitia msamaha na pia kuwatumikia wengine kwa moyo wa upendo wa dhati. Lakini bahati mbaya, mara nyingi ni wale wanaojulikana kuwa wenye akili ndyo dhaifu sana katika kushirikiana na wengine vizuri.

Kiburi cha elimu sio msingi mzuri wa kuwa na ushirika na wengine! Paulo mmojawapo wa wasomi wa wakati wake, anasema

katika ***1Wakorintho 8:1*** Kwamba.... ***"...Ujuzi huleta majivuno, bali upendo hujenga... ".***

Ungetamani uwe nani, mtu anayeongelea tu kuhusu miujiza? Wala anayetenda miujiza? Mtu anayeongelea tu kuhusu upendo wa Mungu ao mtu anayeweza kumkumbatia mwingine na kumuonyesha upendo wa Mungu ? Katika ufalme wa Yesu tunajulikana kupitia matunda yetu, na wala siyo kupitia yale tuliojifunza wala elimu tunayo fahamu. Hakuna shahada yeyote ile kwenye ukuta wa ufalme wa Mungu.

Yesu aliwapa ufalme wake watu wasiokuwa na elimu wala masomo. " Kwa nini tuna amini kwamba tunafanya vema ? " ***" Basi walipoona ujasiri wa Petro na Yohana , nakuwa jua kuwa ni watu wasio na elimu wasio na maarifa wakastaajabu, wakawatambua ya kwamba walikuwa pamoja na yesu ". Mdo 4 :13.*** Aina nyingine ya makosa inayoonekana katika masomo ni kwa kiongozi aliyefanikiwa mwenye karama anayeanzisha shule la Biblia. Lengo ni kufundisha wanafunzi yale kiongozi anayoyafanya katika huduma, kwa mfano ,kuponya ,neno hili linasika vema ao sivyo? Wanafunzi wataanza kuonekana kwa shule hilo kutoka sehemu mbalimbali kuja mahali hapo ambapo kiongozi huyo ao watenda kazi wenzake wanahudumia. Mara nyingi wale walio na shauku na njaa ndyo kama dhabihu njema wanaohudhuria shule hilo. Mazingira ya hali katika shule hizo na ndani ya kanisa yanakuwa ya kusisimua sana, kuvutia na ya kubadili maisha. Tatizo linakuwa ni nini hasa.?

Hivo sivyo Yesu alivyotenda wala sivyo alivyo tuomba kufanya : kwa hayo kunakuwa na tatizo ! walio wazuri huja kwa huduma hii ya masomo. Shule linakomaa lina kuwa na mahitaji mengi kama vile- haja ya kuwa na Administrator ,waalimu, washauri na watenda kazi wasaidizi .Huduma haileti baraka kwa jamii la mahali pale,jamii ambalo liliwatuma wana na binti zao kuja ku-fundishwa ili baadaye warejee kwenye shamba la mavuno katika jamii zao, badala yake wanawashikilia wanafunzi walio fanya vema kuliko kuwarejesha kutumikia jamii zao.Shamba la mavuno la mahali ambalo lilihitaji watenda kazi zaidi , linakuwa na uhaba wa watenda kazi kwa sababu ya shule hili la huduma.

Vituo hivi vya majifunzo ao huduma , vinakuwa vikiandaa kongamano ,na wachunagi ,viogozi na wengine walio na uwezo wanachukua ndege,kutembea kwa miguu ili kuhudhuria.

Na kama unataka kuwa na sifa katika dhehebu, basi inakubidi kuwa pale ! Mahubiri na maombi vyote ni sehemu kuu ya uamsho na mavuno. Ni ajabu! Ni Ajabu? Viongozi watagharimu ma mia ya pesa kwa mwaka kwa ajili ya mikutano lakini wata-wekeza kidogo ao wakati mwingine hawatawekeza kwa ajili ya watu maskini wanaoishi katika vitongoji (mitaa yao yenye umaskini). Lakini kama ule mda na pesa tunazowekeza kwenye mikutano, kongamano , ingeliwekezwa kwa ajili ya watu wasio na makadhi , maskini, wafungwa ( magereza ,vitongoji vyenye umaskini ,na wakimbizi ?) , Na vipi kama mavuno wanayo-yahubiri na kuyaombea yangelitokea kweli? . Hapa katika bara la Asia ya kati tumeshangazwa na kuona mtu ambaye amehitimu

masomo zaidi ya nane 8 ya shule za Biblia za madhehebu tofauti za kimishonari. Lakini kwa nini Baadhi yao wanatamani kuendelea kuwa wanafunzi,kusikia mambo yale yale tena na tena? Kwa nini wanatafuta mafundisho ya Ziada?

Wakati mwingine masomo hukamilishwa kwa kupewa cheo na madhabahu ,na jambo hilo linakuwa la kuvutia hasa katika maeneo haya ambapo kuna umaskini. wakati mwingine ujuzi elimu uliopata unakuletea mlango wa urafiki na dhehebu la ki-mishonari,ambalo labda wanaweza kukuajiri na kukupatia mshahara. .huo ni mvuto mwengine mkuu !

Sina uhakika kama mashirika mbalimbali ya kimishenari uwa-eleza wa fadhili wao kuwa baadhi ya wanafunzi cha chuo la Biblia wamehitimu na kumaliza baadhi ya somo zao. Nina uakika wana wajulisha tu idadi ya wale wanao wafundisha kuwa " viongozi wa taifa baadaye ". Kwa nini wanafanya hivo ? Wenyewe wamefundishwa katika shule za Biblia. Kuongoza shule la Bilibia ndiyo jambo la pekee wanalofahamu ku-tekeleza. Wanajuwa namna ya kuwatayarisha watu wenye ujuzi kwa ajili ya kushikilia nyadhifa Fulani Fulani katika dhehebu. Hawa juwi kamwe namna ya kuwatayarisha wa tenda kazi kwa ajili ya shamba la mavuno. Mafundisho yao ipo kwenye idadi ya wanafunzi waliyohitimu kwa shule lao, wana hesabu kiasi cha vyeti walivyogawa. Hawa hesabu kiasi cha wafwasi halisi waliopatikana. Kwa bahati nzuri, baadhi ya wana chuo wamechoshwa na mtindo huo, wameamua tu kumfwata Yesu na kuendelea na kazi. Lakini hata hivo baadhi ya mipangilio ya kidini nayo ina badilika. Nimewahi kusikia kuhusu shule mmoja la Biblia Indonesia , halikabidhi cheti cha kuhitimu (diploma)

kwa mwanafunzi wake hadi pale mwanfunzi huyo ata kuwa ameshuhudia na kuwabatiza watu kumi na wawili watakoanzisha kanisa la mitume la Yesu. Ukweli ni kwamba aina yoyote ya mpangilio, mamlaka ya dheebu inayoinuka dhidi ya kanisa la mahali, ina kuwa moja kwa moja adui wa kanisa la mahali. Madhehebu hayo yanagarimu pesa , na watu , nguvu za watu na yana kuwa kama ndyo kichwa cha kanisa badala ya Yesu. Ni vituo hivi ndivyo vilistahili kutoa elimu (mafunzo) na kuwatayarisha viongozi wa kanisa la baadaye, ndyo sasa yanakuwa chanzo cha mafundisho ya upotovu. Ni bayana ukweli kuhusu Antekristo, ina maanisha kuwa dhehebu lolote lile, taratibu ya upangiliaji,ao mtu anaye punguza nafasi ya Yesu kristo kama kichwa cha kanisa aliye kati ya watu wake.

Antekristo, sio tu kwamba atakuja, lakini ni roho itendayo kazi tayari katika kanisa, asema Yohana kwa kitabu cha***1Yoh.2:18-23.*** Matendo ya Antekristo inajulikana kuwa itaanzia kanisani na uongo wake mkuu ni kule kukataa kwamba Yesu sio kristo. Lakini siamini kama Yohana anaonyesha upinzani kwa kusema kwamba Yesu ndiye masiya, ila anaonyesha upinzani katika matendo juu ya uungu wa Yesu kristo kwa kanisa lake. Tunakiri Yesu ni Bwana kwa vinywa vyetu, lakini maamuzi yote tunayo chukuwa wenyewe na kwa jinsi tunamfanya kuwa mtu wa kawaida tu kuliko kumtambua kuwa ndiyo kichwa halisi cha kanisa.

Kwa kipindi cha miaka ishirini iliyopita, madhehebu makubwa ya vikundi vinavyoanzisha makanisa ulimwenguni,viliamka kutayarisha watenda kazi kwa mavuno katika shamba la

mavuno. Watenda kazi hutayarishwa uwandani ! Ndivyo alivyo-fanya Yesu. Ni katika kitabu cha ***DAVID GARRISSON kiitwcho" KUNDI LA KUANZISHA MAKANISA "*** ***http://www.churchplantigmovement.com.***

Msisimko wakutayarisha wanafunzi (wafuasi) Hujitokeza kwanza katika kundi la watu ambao hawajafikiwa,ndipo sasa tunakuwa na sababu yakuwatayarisha watenda kazi uwandani. Wanafunzi huzaa wanafunzi. Mipango na matukio tunayo kuwa nayo kanisani haiwezi kuzaa wanafunzi. inazaa watu ambao wanajuwa kuongoza ibada na kubuni matukio mbalimbali. Yesu aliaga mkutano na akawekeza maisha yake ndani ya wale kumi na wawili. Msingi mkuu katika ufalme wa mbingu ni URAFIKI (Uhusiano)

**C. TATIZO LA MAONO AO LAWAMA KWA MAVUNO**

Katika **Sura ya 4 ( ine) ya injli ya yohana** tuna historia ya mwanamke msamaria kwenye kisima. .Kwa kawaida wayaudi walidharau wasamaria kama kizazi kisichomjua Mungu. Myaudi asingeweza kupita katika mji wa Samaria , na hivo walikwepa kupita Samaria. Lakini Yohana anasema katika **shairi la 4** kwamba Yesu alitaka " kupita Samaria ". Matokeo yake ikawa mkutano kwenye kisima na wokovu wa yule mwanamke na hiyo kumsabisha Yesu kusema juu ya ***" mashamba yaliyo meupe tayari kwa mavuno ".***

***" Hamsemi ninyi , bado miezi minne ndipo mavuno ? Tazama, mimi nawaambieni inueni macho yenu myatazame mashamba yamekwisha kuwa meupe tayari kwa mavuno"*** **Yohana *4 :35***

Wanafunzi na Yesu wote pamoja walitizama shamba lile. Wanafunzi waliliona shamba lile Kama bado liko tupu bado miezi minne kabla ya mavuno. Hawakuwataka wa samaria na hawataraji ya kwamba chochote kilicho chema kingejitokeza! Yesu alifanya mapenzi ya Baba kuwa ndiyo chakula chake naye aliona mashamba meupe tayari kwa mavuno na kwa imani hiyo kupitia vipawa vya roho mtakatifu, alivuna mavuno.wote walilitizama shamba lile lile lakini waliliona tofauti kulingana na mioyo yao.kueleza shamba kama " udongo mgumu" ni kutoa unabii usiokamilika wenyewe. Ni Kama kulaumu mavuno kwa kutovunwa, na mbaya zaidi ni kama kumlaumu Mungu"." Mungu hatendi hapa kama atendavyo kwa mataifa mengine" . Kukosa maono ni tatizo la moyo. Matatizo ambayo yanapashwa kusahihishwa na Ubatizo toka kwa Moyo wa Mwalimu Mkuu - kwa miaka kadhaa huduma moja huko saudi arabia ilitanganza ujumbe huu : "njoni kwa yesu, mshiriki kanisa nzuri na muwe wanafunzi ". Ujumbe huu una matatizo maana katika inci za kiarabu makanisa hayana majumba yaliyojengwa kama kanisa. Wanatumia mbinu tofauti. Wanakuwa na mikutano ya nyumba kwa nyumba, na ni hapo wanajifunza neno la Mungu, wanabatiza,na kuwaombea wagonjwa. na sasa ujumbe umekuwa " njoni kwa Yesu na anzisheni ushirika wa wanafunzi katika nyumba yako " . makundi haya yanakuwa kwa kasi sana katika mila hiyo na kulingana na ripoti ni kwamba,kuna idadi

yakutosha ya waamini wanaobatizwa katika saudi arabia kuliko ubeljiji na ujapani. Mbinu hii ya makanisa ya nyumbani inaptikana kwenye mtandao wa internet- Tovuti

(*Http//WWW.222Ministries.org )* .

**MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA**

**1). Ni Vigumu kulaumu Moyo, Maono wala mbinu ya watenda kazi kuwa sababu ya kukosa Mavuno katika aina ya mila Fulani.Si kweli kwamba kuna Mila inayofunguka na kuwa wazi kwa Yesu? Je? Vipi kuhusu majira ya kupanda na kuvuna?**

Ndyo, Kuna majira ya kupanda na kuvuna lakini majira yote hayo yanakaribiana sana moja na jingine kama anavyoeleza Paulo katika **II Wakoritho sura ya 3.** Inaonekana pia kwamba katika kila mila kuna sehemu ya mavuno ambamo yupo mtu Fulani alyemtii Yesu na kupuuza ule “ Ugumu wa Udongo”. Baadhi ya makundi kama haya yameanza miongoni mwa watu maskini,watu waliovunjika moyo na kunyimwa haki ya uteule..

**2). Si ni hakika kwamba lisilioendeka katika Mila hii, halitaendeka katika mila nyingine?**

Tunapozungumzia kuhusu mbinu hizi huko magharibi, wengi husema kuwa hayo yanawezekana tu huko mashariki na wala sio hapa.Na Tunapozungumza na watu wa mashariki, na wao baadhi yao husema kuwa kuwa hayo hayawezekani kutendeka hapa kwetu labda huko magharibi na sio hapa.Sisi sote hutoa sababu!,

Lakini hata hivo yote hayo yanahusiana na Amri ya Yesu, Yeye ndyo Kiongozi Mkuu na Mwanadamu mwenye hekima ambaye hajawahi kamwe kuishi. Ikiwa Maneno yake yanaambatana na Mila, sisi wote tunakuwa na maswali.Maneno yake yako Juu ya mila na desturi zetu na ni ufunguo,kufungua milango yote ili mila ya ufalme wake ijaze mioyo,Familia,Miji na Mataifa.

**3). Je? Hiyo sio tu Mbinu nyingine? Je? Si kama tunaiga Jambo ambalo haliendelei sehemu Fulani, tukitumaini kwamba litaendelea hapa?**

Tunastahili kuwa wanafunzi wa Yesu.Na amri yake ni kwamba tuwafanye wengine kutii yote aliyofundisha.hatupo wanafunzi wa mwanadamu awaye yote Yule, hata wa Yule anayeonekana kufaulu! Ndyo, Tunawaheshimu baadhi ya wale waliotii maneno ya Yesu katika **luka 10** na waoonao matunda ya ule utii wao katika mila na desturi, mila ambazo kihistoria zinafahamika kuwa ni “ Udongo mgumu” kimila. Kwa hiyo sio tu kwamba ni mbinu mpya, Lakini ndivyo Yesu alivyotuamuru.Baadhi ya mbinu nyingi Juu ya kukomaa kwa Kanisa zinajenga juu ya Biashara na mtindo wa kibiashara .Baadhi ya mikutano ya viongozi. hujenga juu ya mtindo wa kampuni. Na maneno ya Agano Jipya yanatumiwa kama « mashairi ya kudhibitisha » yale yanayoelezwa, ila msingi maranyingi ni nia ya biashara. Nia zote hizo huja na kutoweka, lakini ukweli wote unapatikana ndani ya Yesu . Nasi tunautafuta ukweli huo ulio ndani ya Yesu.Sio tu kwamba ni mtindo mwingine mpya. Ni mtindo wake! lakini ni vema kufahamu kwamba baadhi ya waalimu wa wafanya

biashara hutumia sehemu kubwa ya mbinu zilizo fundishwa na Yesu kwa maendeleo ya mambo yao.

## SURA YA 2

## MAOMBI YANAYO HARIBIKA NA TATIZO LA KIJEOGRAPHIA

***"..Akawambia mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache, basi mwombeni Bwana wa mavuno apelike, watenda kazi katika shamba lake ."* Lk 10:2.**

- Fahamu kwamba Yesu hakutuamuru kuombea waliopotea, neno hilo, kidogo linachanganya lakini ni ukweli. hakutuomba kuombea mavuno. Kilio cha aliye mpweke, anayeonewa, anayetendewa ubaya, cha yule aliye mwoga, cha mgonjwa, cha mshabiki, cha aliyebakwa, cha mwenye njaa, cha mwenyi huzuni kinagusa daima moyo wa Baba. Kilio cha aliyepotea kinafaa, kina nguvu na maombi yake hayakomi kamwe.
- Yesu kristo aliyaona mashamba meupe na yaliyotayari. Hayahitaji matayarisho yeyote ile ya kiroho. Hayana haya ya maombi yetu tunahitaji kuyasikia maombi yao wana haja ya utiifu wetu.
- Tambua ya kwamba yesu hakutuamuru kufunga kila aina ya nguvu za kiroho zinazowatawala waliopotea au kufukuza kila aina ya mamlaka ya kiroho inayo kuwa na mamlaka juu

yao. Swali Hilo lina mjadala mkali pia. Sio hapo pia ambapo yeye anaona kuwa kuna pingamizi la mavuno. Hata hivo anafahamu kuwa anapashwa kushugulikia mamlaka yote ya nguvu za giza kwa kufa na kufufuka kwake.

- Tafakari juu ya **waefeso 1:16-23, wakolosai 2:14-15, waebrania 2:14-15**, nguvu za kiroho zinazoshikilia mataifa katika utumwa zilisalitiwa na kifo na ufufuo wa Yesu kwetu sisi kuomba ni sawa vile ni sisi ndiyo tunafanya kazi hiyo ni kama kutenda kazi katika hali ya kukosa Imani ao kutoamini, kwa kazi ile ambayo Yesu alikwisha kutimiza juu ya Msalaba .Ndiyo maana tunamhubiri kristo aliyesulubiwa ,” aliyetangaza kwamba tuna mamlaka juu ya nyoka na nge na juu ya mamlaka yote ya adui, “ na tunapotumia mamlaka hiyo kwa kuponya na kufungua waliofungwa, Yesu anaona kuanguka kwa shetani.
- Katika sehemu nyingi, makanisa ya kiroho yawezekana kwamba waweza kuwa na” huduma isiyo kuwa na utendaji.” “Wanaimba masaa kadhaa,” “wanafanya vita vya kiroho” “wanatangaza,” “wanafanya mikutano ya maombi,” “wanaandaa hata safari za maombi” (safari za kitalii), wanatabiri ili mavuno yaje, wanaomba ili mavuno yaje wanatangaza kwamba mavuno yamekuja, lakini hata hivo wasiutumie muda wao hata uhusiano walio nao kwa kutii ile amri ya Yesu. Katika **Luka 10** na kuzingatia mambo yanayohusu mavuno.

Kadiri tunavyoomba, tunavyotabiri, tunavyotangaza, tunavyojiandaa tunajisika kuwa salama na hatuoni hali yoyote ya kushindwa. Hakuna tendo lolote la kuhukumu.

Unaweza kuhukumu tu mazingira (hali ya Mambo). "Upako" ule mguso wa Mkutano. Unaweza ongea kuhusu " kupenya kiroho ( Ni wapi wanaeleza kuhusu kupenya kiroho katika Agano Jipya ?"). Basi inabidi kuwa kiroho ili kugundua hayo,! Mnahukumu kutokana na tafsiri ya mambo, lakini hakuna uwajibikaji katika maisha halisi. Tumepuuzia utaratibu na uwajibikaji wa kuwafanya wengine kuwa wanafunzi. Huku tukiishi katika ulimwengu wenye kupotea kiroho.

- Kwa nini tunaomba kana kwamba tunahakikisha? Bembeleza ao, kugeuza utendaji wa mkono wa Mungu katika mataifa? Maombi mengi yanafanyika kulingana na mwili kwa sababu hatujakutana na asili ya moyo wa Mungu. Ndiyo ! omba Kwa ajili ya mataifa hadi utapokuwa na moyo wa Mungu kwa kwenda
- Kwa nini tunaamini kuwa kadiri unaomba sana ao kadiri unaomba kwa sauti kuu, ndipo Mungu atasikia na kujibu? Yesu anatuomba tusitende mamna hiyo maana, ni wapagani ndiyo hufikiri kwamba kwa wingi wa maneno watasikilizwa **(Mth. 6:7)** Mungu husikia mioyo yetu.
- Mara kadhaa tunakusanyika kwa ajili ya mikutano ya maombi , Tunafikiri kwa hakika kuwa kadiri kuna watu wengi wanaoomba katika mikutano yetu , kadiri Mungu atajibu? Je tunaweza kumshawishi Mungu kwa Idadi ? ***Yakobo anatuambia kwamba maombi ya mwenye haki inatenda mengi na anatupa mfano wa Eliya (Yakobo 5:16-17) .*** Mungu anaheshimu Imani na wala sio idadi ya watu. Kwa nini tunaamini ya kuwa maombi ya vikundi

hadharani yanafaa? Tunawafanya wale viongozi wa maombi hayo kuwa nyota tu weye umaarufu, lakini Yesu alihukumu umati wa wakati wake kwa kuomba hadharani , na kusema tunapoomba sirini, Mungu atatujibu **(Math 5:5-6).** Roho ya dini itashangilia Yale Mungu aliyotenda Kwa wakati uliopita na kufurahia masihi anayekuja, lakini wakatamani kumua. Asemaye ***" leo hii kwenu ninyi msikiyao, unabii huu wa maandiko umekuwa halisi. "*** **(Luka 4:21-30).** Yale Mungu aliyotenda hapo kale yana tuhimiza na yale Mungu atakayotenda Kwa siku zijazo. Yanatuletea hali ya kuchangamka lakini sasa Mwalimu (Rabi) anaomba sasa tuwe watu wa imani, utiifu na kujitolea.

- Ukweli ni kwamba Yesu alituamuru kuwaombea watenda kazi mavuno ni tayari, na tena tayari mno! Ni kwa hali ya kiroho ndiyo mavuno yapo tayari. Matayarisho muhimu yote yamekamilika. Amekamilisha maombezi makuu. Tunahitaji sasa kuvuna matunda ya maombezi yake. Tuombe Kwa ajili ya watenda kazi.
- Hatari iliyopo katika kuwaombea watenda kazi ni sawa na ile iliyotokea kwa wanafunzi. Walitumwa haraka Kama matokeo ya maombi Yao! Wakati tunanyenyekea na kutii , tunajikutana kububujika katika mawimbi ya mapenzi yake.
- Sisi sio wakurugenzi ,wajuzi ao wafalme. Hakuna huduma yeyote katika agano jipya ao karama inayoitwa " mwombezi" wa kutoa" " unabii" hakuna "Jenerali wa maombezi" sisi sote tu makuhani na tunaomba kwa sababu hiyo ni sehemu ya kazi yetu. Sisi ni watenda kazi.

- Tuwaombee wale watakaojinyenyekeza na kufanya kazi kubwa, kazi chafu na wakati mwingine ya hatari katika shamba la mavuno. Mungu ana mbinu moja tu ni ya kulituma neno lake katika mwili kuja kuishi pamoja na watu ili wauone utukufu wa Mungu unaojaa neema na kweli. (**Yohana 1:14)** mpango wake daima ni **'A'** na wala hana mpango mwingine **'B'** hatupaswi kuomba kwa ajili ya watenda kazi bila sisi wenyewe kuwa tayari kwenda. Tuombe juu ya watenda kazi. !

**B) Bwana wa mavumo**

Katika kifungo hiki cha luka, Yesu anajiita kuwa ni " **Bwana wa mavuno**" alifanya kila liwezekanalo ili kuthibitisha cheo chake hicho. Wengi huamini kwamba kanisa litapungukiwa hadi pale Yesu atakuja Kutuokoa na giza la shetani. Wanajaribu kuamini kuwa uovu utaendelea kukua hata kuiongoza Dunia kama alivyoona Danieli katika kitabu cha **Danieli sura ya Pili (2)** na kama ilvyosemwa na Yesu katika **Mathayo 13,** Waanamini kwamba yesu atarudi akitumia nguvu na uhasama kutimiza yale ambayo hakuyatenda kwa njia ya 'upendo'. Wanaamini kweli kwamba kazi yake haikutimizwa msalabani na kujitoa kwake kama sadaka hakukutosha kuukomboa uumbaji unaopotea. Wana jaribu kuamini kwamba Yesu angeliitwa 'Bwana wa mapungufu".

Yesu alishinda ubaya msalabani kwa njia ya upendo usioshindwa! Mahesabu yanahakikishia historia kwamba ufalme wa mbingu ni ufalme unaokuwa haraka. Katika mwaka wa Arobaini (40) kundi ambalo Yesu alilianzisha

Lilikuwa na wafwasi kiasi cha **10.000.** Katika mwaka wa **300** Idadi hiyo ilifikia kiwango cha karibuni **milioni 6** ya watu sawa na asilimia kumi ya " wakadhi wa himaya ya kirumi". Kukua huko kulidumaa baada ya karne ya tatu na ni hapo kanisa liligeuzwa kuwa shirika na kufa lakini kukua kulianza tena na vikundi vya wamishonari na **Mtakatifu PATRICK** na baada ya hapo kukawa na kurudi nyuma. Kukua kulianzishwa tena na **Martin Luther**, na ni hapo mwanzo wa mageueuzi, ao kufanya upya (urejesho) na mwanzo wa vikundi vya kimishonari kwenye miaka 500 iliyopita.

Kwa karne tatu za kwanza, kanisa lilikuwa kundi la makanisa yaliyokusanyika katika nyumba. Mikutano kama hiyo ya hapo mwanzoni haijatoweka bado, lakini kwa karne kadhaa kanisa kama dhehebu liliwatesa na kuwauwa wote waliosoma Biblia katika nyumbna zao ao wale wote walioomba pamoja na watoto wao. Waliokusanyika hapa na pale na wale waliokuwa mafichoni waliamka na kulipuka kwenye karne ya ishirini na kuanza tena makanisa ya nyumbani, zaidi sana katika inchi ya china.

Kwa miaka ya mwanzoni ya mateso, waamini wengi wa kichina waliacha imani yao.....wana historia wengi husema kuwa asilimia sabini **(70%)** ya wanamemba wa kanisa kwa wakati huo walimkana Bwana. Na kwa sababu china ilikuwa imefunga milango yake, ulimwengu uliamini kuwa hakuna mkristo anayesalia... Mwishoni mwa miaka ya **1970** Bara –koloni la Africa lilikuwa na idadi ya wakadhi milioni **108 y**a watu ambao miongoni mwake **milioni 8.1** ya watu

ao asilimia **tisa 9%** walikuwa wakristo. Baadhi ya wakristo hao walikuwa wakristo wa **Orthodoxe, Copte na waethiopia**. Walizidiwa kwa idadi na waislamu ambao walikuwa **milioni 34.5** kulingana na ripoti ya wane kwa mmoja. **Mwaka 1962**.... Kulikuwepo na waislamu kiasi cha **miloni 145** na **wakristo milioni 60** - Ni kama watu 5 juu ya wawili....**Mwaka wa 2.000** kulikuwa na wakristo milioni **360 katika bara la Afrika**.... **Asilimia 40,6 %** ya wafrika walikuwa waislamu na **asilimia 45 % walikuwa wakristo**.

Tokea mwaka wa **1900 hadi 2.000** asilimia ya waislamu kulingana na ile ya wakristo ilikuwa kwa kiwango cha **waislamu** 4. **Kwa mkristo mmoja** 1. “ Kuliko kulingana mwislamu 1 kwa mkristo 1. “

Huko India, muungano uitwao nyota ya bahari, ushirika wa makanisa ya nyumbani, unaripotiwa kuwa siku ya pentekosté ya **mwaka wa 2009**, walibatiza watu **300,000**. Viongozi wa wavictor na Bidhou choudrie wanasema kuwa “ uvamizi muhimu umeingia kwenye jamii ya waBrahmane na waislamu’ , muungano wa nyota ya bahari unaoasimamia sehemu moja tu ya mashirika kama hayo ambayo yana kuwa sana kwa kasi huko india.

***« Yesu ni Bwana wa mavuno. Hilo ni mojawapo wa vyeo vyake hiyo ni asili ya utu wake. Sisi ni sehemu ya ufalme wake unaokuwa ! «***

## c. MAOMBI YENYE LENGO

« Maombi » « ya kuwatuma watenda kazi katikat shamba » yanasikilika kama yasiyo na mamlaka (kulingana na tafsiri ya

kiingereza) . Tunatuma barua, tunazituma e-meili, tunatuma barua za pongezi, barua za kutoa pole (rambi rambi). Hata hivo, **(katika luka 10**) msemo huu ungetupa picha ya mkulima anayetupa kwenye udongo mbegu toka mkononi mwake. Je ? Yesu ni Bwana wa maisha yetu kiasi cha kutuchukua mkononi mwake, kutuondoa kwenye maeneo yetu yenye starehe, maeneo tunayoyazoea, yenye usalama na kututupa katika shamba lake la mavuno ? Je ? Tuko tayari kuanguka udongoni kufa na kuzaa matunda mengi ? Msukumo wetu ni upi ? Je ? tunataka kumtumia Mungu kupata yale tunayotaka tu kutoka kwake ao tunatamani hasa utukufu wake ?.

Tafakari juu ya **Yohana 12 :23-26** ! Ikiwa tunamtukia na kumfwata Yesu ,Tutakuwa pamoja naye Mahali alipo na tutaheshimika na Baba Yake. Yesu alikuwa wapi wakati huo ? hakuwa anazungumzia Juu ya mahali fulani kileleni ao wakati fulani, lakini ni mahali anaposhirikiana na mahali hapo wanaposhirikiana ni ndani ya moyo wa Baba yake. Tunawaza kuonyesha moyo wa Baba ikiwa tunajua kwamba tunaishi ndani ya moyo wa Baba.hivo ndivyo Yesu alivyofahamu na ndivyo anavyotaka na sisi tufahamu !

Ni matukio machache sana ya utendaji wa Mungu yaliyotoka kwenye jamii ya watu wenye heshima, na waliostarehe. Matukio mengi yalianzia miongoni mwa watu maskini, wasiofaa, waliokata tamaa, waliovunjika moyo. Na ni makundi machache ya kimungu yaliyoanza na kuwaalika watu toka katika jamii ya aina hiyo kuja kuhudhuria kwa mikutano yao. Tunapashwa kuwaendea watu wa kizazi hicho. Mtu mmoja alisema kwamba kanisa

linakabililiwa na tatizo la kijeographia. Yesu alituamuru kwenda lakini sisi bado tunaomba ulimwengu kutujia sisi. Kwa nini tunafanya hivo ? kama mtu mmoja angekuja kwenye maeneo yangu ni, ni kama anakuja kwenye maeneo ambayo ninamiliki mimi, mahali ambapo nina zifahamu hata zile sheria zisizoandikwa, maeneo ambayo nina yafurahia na kuwa salama. Kadiri watu wanavyoongezeka kwenye maeneo yangu ndivyo ninavyoonekana kufanikiwa. Kukusanya idadi kubwa ya watu imefanya viongozi wengi kuwa kama wafalme, wanaoishi na kutenda kama hivo.

Aina hii inaitwa *'mtindo wa kuvutia »* wa kukua kwa kanisa. Shida ni kwamba baadhi ya hao wanaovutiwa ni wakristo tayari lakini ni waamini ambao wanatafuta jambo jipya. Ni wajibu wetu kama waamini kupata jamii ya watu ambao wanajibu mahitaji yetu kulingana na vile tunavyotamani wawe ao ni wajibu wetu kuanzisha jamii kwa wale wasiokuwa na jamii? ieleweke wazi kuwa sis sio wanunuzi ao watumiaji wa mambo ya kiroho. Tunapashwa kuwa watenda kazi katika shamba la mavuno.

Ukweli halisi ni kwamba wale wasiokuwa bado wanafunzi wa Yesu. mara nyingi hawaji kwa mikutano yetu haijalishi hata kama tumepakwa kiasi gani. Hilo ni kama mkulima asimamaye mlangoni mwa ghala lake na kuyaita mavuno akisema *« mavuno karibu ndani'!* Tunakuwa na ghala nzuri yenye kuwa na kila kitu cha kutupa starehe. Ibada zetu ni zenye kuchangamka. Mahubiri yetu yamejaa upako. Watoto wanashughulikiwa vizuri sana « *wakati wa ibada"* labda ungesema mkulima huyu amechanganikiwa. Ikiwa mavuno yake yangekuja anapashwa

kwenda kuyavuna, na hata kuyaleta ndani. Hiyo ndiyo aina ya watenda kazi tunaowaombea. Hivo ndivyo Bwana wa mavuno alivyotuamuru kutenda.

**MASWALI YANAYOULIZWA:**

1. **Je? Inamaana hauamini katika kile baadhi ya watu Fulani wanaota "mbingu ao viwango mbalimbali vya vita vya kiroho' hauamini katika kufunga nguvu za giza ambazo zinafunga mataifa katika utumwa kama matokeo ya kutopokea habari njema?**

   Hapana, siamini kamwe.Yesu hakulisisitiza jambo hilo kuwa kama sheria ya kutekeleza kwa sisi kwenda. Sasa kwa nini basi sisi tufanye hivo? hata hivo katika **Luka sura 10** tunamwona Yesu akisema " ***mimemuona shetani akianguka kama miali kutoka mbinguni*** " kulingana na maneno hayo tunaweza kusema hii ilikuwa ni matokeo ya kazi ya ufalme uliotimizwa uwanjani na mitume katika vifungu vile vilivyotangulia. Mjadala kamili kuhusu jambo hili unaweza kutizamwa kwenye somo letu juu ya " vita vya kiroho." ," Ufunuo wa utukufu wa Yesu", kwenye tovuti yetu (website.)

Amri ni kuwaombea watenda kazi na kwenda. Je? Bwana anagelitutuma sisi endapo matayarisho yote hayajakamilika? baadhi ya wamoja walio yaanza mafundisho haya yakupambanua ngome na nguvu za giza, na baadaye kuzifunga na kuziangusha, baadhi ya hao hapo awali walikuwa washirika wa shetani ambao wanadai kuwa na ujuzi wa kufahamu na kuuona ufalme wa giza. Kwa nin basi tuchukue ushuhuda wao

kuuthibitisha na maandiko ? Imekuwa ndyo maeneo ya “waombezi wengi manabii » (neno hilo silo la kibiblia) kudai kuwa wana uwezo wa kupambanua utawala wa mwovu shetani juu ya mataifa na kuwa na uwezo wa kufunga na kutupilia mbali. Na kama hiyo ni muhimu, kwa nini basi haikufundishwa na Yesu ao na Paulo ? kwa nini hakuna mahali popote panapotuonyesha kuwa hayo yalitendeka wakati Paulo alipokwenda kwenye maeneo mapya ? hilo ni kama mchezo mzuri wa maigizo kwenye vituo vya kongamano zetu. Lakini sio ukristo wa agano jipya na halina nafasi katika utendaji wetu. Tunapashwa kuponya wagojwa, kufukuza mapepo ndani ya watu. Tufanye kazi ya Yesu na wala tusifwate upotovu wa wale wanaolenga tu mapepo hewani.

2. **Je kila mtu anapashwa kwenda ?** Je sote tutakuwa wainjilisti , waanzilishi wa makanisa ? Yesu aliongea kuhusu mitume, sivyo ? ndiyo Yesu alisema na mitume wazi wazi kabisa, na sio wote waliokuwa na majukumu ya huduma ya ziada. hata hivo, ikiwa ni ngambo ya pili ya bahari, mabondeni, ao njiani, kila mmoja wetu anao wajibu na jukumu la kuutumikia ulimwengu unaotuzunguka, familia zetu, na marafiki. Kama vile ilivyo kawaida Katika maisha ya familia, kila watu waliooana hutamani watoto, vivyo hivyo ni kawaida katika uhusiano wetu na Mungu Baba kutoa moyo wake kwa wanae wa kiume na kike na kuutoa moyo wake kwa Bibi arusi mkuu na mrembo kwa ajili ya mwanae. Na kugawa moyo wake kwa ajili ya uumbaji mkuu, hekalu lililo hai kwa ajili ya Roho mtakatifu kulifurahia.

3. **Unasema kwamba kila mtu aliyeanzisha aina fulani ya huduma, shule za bibilia ana nia mbaya ?**

   Hapana, sisemi hivo. Sisi sote huanza miradi hii tukiwa na nia nzuri tunashuhuda binafsi za kuanzishwa kwa vituo vya mafunzo. Tatizo ni kwamba wakati hatufwati maneno na mfano wa mfalme Yesu mara nyingi tunaishia mahali pa baya. Tatizo la mafunzo yaliyopangwa liko wazi na lina hitaji utaalamu mwingi , linaweza kuanza na makusudi mazuri lakini wakati shirika fulani linapoinuka na kuingilia utawala wa shule hilo, sasa shule hilo linaweza kubadili malengo yake toka ilivyokuwa kwa mwanzilishi. Mwaanzilishi labda alikuwa akilenga kuwaandaa watenda kazi lakini watakao kuja baadae watalenga namna ya kukuza, kutunza, kuongeza mishahara, kuongeza na kukuza vyeo vyao. Je katika hali kama hiyo kuna chema kinachotokea ? ndiyo, lakini shirika hile lote linakuwa adui wa mavuno. Kilichoanza kama mafunzo kwa huduma kinageuka kuwa shule la biblia la miaka mitatu na kilichoanza kama shule la biblia linageuka kuwa chuo kikuu cha miaka minne, na kilichoanzishwa kama chuo kikuu, kinageuka kuwa univasti. Nia ya mwanzoni ya mwanzilishi inatoweka na matakwe ya shirika ndiyo sasa inaendelea.

   - Tunapashwa kuwa wafwasi wa Yesu. Alitutayarisha ili twende katika shamba, mahali ambayo wanafunzi wanafanywa na makanisa yanakua kwa haraka katika mila fulani, mojawapo wa tabia ya jumla ni kuwandaa watu kwenye kazi, maadalizi yanatokana na mafunzo ya muda mfupi na mapunziko ili kupata mwelekeo.

## SURA YA TATU

***« Enendeni, angalieni, nawatuma kama wana kondoo, kati ya mbwa mwitu » ( Lk. 10 :3 )***

### HATARI MBELENI

**a) MAVUNO YANAFIKIRIWA KUWA NI KAZI YA HATARI !**

Tulipokwenda Asia ya kati, niliuliza ni namna gani injili iliwafikia kwa mara ya kwanza katika jimbo lao. Jibu lilikuwa kwamba mishonari wa kwanza waliokuja, walikuja kwa ruhusa ya "**Mtume Stalin"** niliwahi kusikia **Stalin** akiitwa kwa majina mengi, lakini nilikuwa sijasikai akiitwa" **mtume"** basi hata hivo niliuliza jina hilo lilikuwa na maana gani. Historia ni kwamba katika kuyachukia mambo yote ya kimungu, aliwashika waamini kando kando ya mji wa Moscou na kuwatuma kwa treni (Gari Moshi) ndani ya mabehewa ya mifugo hadi **Kyrgyzstan** kwa leo ni mwendo wa siku tatu usiku na mchana. Waliondoka wakati ule na yale tu ambayo wangeweza kuchukua bila chakula wala maji ya kunywa njiani**. Moja ya tatu 1/3** ya watu miongoni mwao walifariki njiani wakati wa safari na **1/3** nyingine walifariki wakati walipofika, kwa sababu hapakuwepo na chakula. walipofika **1/3** ya wale walioishi ndiyo waolioshuhudia Yesu kwa mara ya kwanza katika Jimbo hilo.

**Mao tse toung** ainaitwa pia **" Mtume"** na wanamemba wa mwili wa kristo china. Mara tena waweza kuswali kwa nini? Wakati alipotawala, kanisa la china lilipanuka sana

magharibi na mashariki mwa inchi, likitegemea sana kufadhiliwa kifedha na inci za Magharibi. , ambako huko nako kuna udhaifu. Mao akawahamisha wageni, akazibomoa shule za kikristo, seminari, majengo ya makanisa na akaanza hata kuwashika waamini na kuwatuma mahala popote inchini kama watumwa, kufanya kazi katika viwanda, kwenye machimbo ya madini, na katika mashamba. Ushuhuda wa waamini, kutokana na vile walivyoishi, walivyotumika, walivyoteseka,na kufariki ukawaleta wengi kwa kristo. Ushuhuda wa Yesu ambao ulionekana kutengwa katika mila ya kigeni na kulundikwa katika sehemu moja ya inchi, ulipendwa ndani ya taifa lote kwa gharama ya serikali ya kikomunisti ya China. Wachunguzi wa mambo toka inchi za magharibi walifikiri kanisa limekwisha china, lakini sasa kanisa china lina kishindo, linakua, na linaendelea kuteswa. Kama bado hanjasoma***" mtu wa mbinguni"*** historia ya **ndugu YUN,** unahitaji kufanya hivyo. Je waamini hawa waliteswa? Ndiyo! Na wengi walifariki ? **Staline ao Mao** ndiyo wana neno la mwisho? Hapana walipotamani kulifinya kanisa, ndipo walipolifanya liendelee zaidi kwenye udongo wa mataifa.

**B) NI KATIKA MATESO NDYO ASILI YA YESU INADHIHIRISHWA**

> ***Heri minyi watakapowashutumu na kuwandi na kuwa menza kila neon baya kwa uongo, kwa ajili yangu. Furahini, na kushangilia, kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni, kwa maana ndivyo walivyowanahi manabii waliokuwa kabla yenu….' ( Math 5:11-12).***

Amri za Yesu zilizotolewa kwenye mlima zanakabiliana na ukweli huu. Amri ya kuwapenda Adui zetu, kuwabariki wale wanaotulaani na kuwatendea mema wale wanaotutendea ubaya kulingana na ***Mathayo 5:44***. Ni utimilifu wa amri hizi ndyo uliogeuza mioyo ya watu wengi kwa Yesu ndani ya gereza la kichina na ile hali ya kufanya kazi kwa shurti amri zina kabiliana na nia zetu, amani, na mafanikio. Tuna mpango mzima katika makanisa, ambapo tunafundisha kwamba alama ya Baraka za Mungu ni mafanikio yako na kwamba shida, umaskini, ne mateso ni alama ya dhambi aliyotenda mtu ao kukosa imani, hii ni kupotosha injili ya ufalme. Katika mazingira potofu kama haya yenye amani na anasa watu hujiuliza kama kweli bado Mungu anawapenda wakati wanapo kabiliana na mambo ya kuwavuruga vichwa. Mungu sio mtumwa wako. Hatuji kwa Mungu kwa ajili ya yale tu ambayo tutapokea toka kwake. Tuna imani isiyofaa usimweke Mungu mfukoni mwako. Mungu sio kama ile mashini ya kuuza ambayo ukiweka dola ya imani, dola ya utoaji, dola ya ukiri,unapokea lolote unalotamani .

Tumeufisha ule utu wa kale wa dhambi na kutoa maisha mapya kwa Mungu kwa ajili ya utukufu wake, ingawa hata kama hiyo ina maanisha mateso na kujitoa kama dhabihu. Ukweli miongoni mwa ulimwengu wa kiislamu ni kwamba kumwamini Yesu, hakutafanya maisha yako kuwa rahisi. Itayafanya maisha yako kuwa na magumu (shida) nyingi na hatari . ukweli juu ya mateso na dhiki unakabiliana na injili rahisi, injili inayo washawishi watu kuja kwa Yesu kwa ajili tu ya yale atakayowatendea ao watakayoyapokea kutoka kwake. Tofauti yake Paulo anamwambia ***Thimoteo (2thim 3:12)*** "***Naam na wote wapendao kuishi maisha ya utanwa katika kristo Yesu wataudhiwa..***" baadhi ya watu wamegeuza kabisa maandiko haya, na wamefundisha ya kuwa ikiwa tuna imani yakutosha ndani ya Kristo, maisha yetu yatakuwa yenye afya , utajiri, na yenye kujaa amani na starehe. Injili hii ya amani na mafanikio sio injili ya Agano Jipya. Tumebatiza **" *hali ya watu wa magharibi ya kupenda vitu kama ndiyo kutafuta ufalme wa Mungu*".**

Haijalishi ni maandiko ngapi umeyahubiri kwenye televisheni (runinga) umetumia kudhibitisha kuwa hali ya kuwa na vitu na kupenda fedha ndio kubarikiwa na Mungu, Tunafahamu kwamba sehemu kubwa ya maneno yao ni kuhusu Baraka na laana na njisi gani tunabarikiwa ao kulaaniwa kutokana na yale tuyatendayo, zaidi sana katika maeneo ya kile tunacho watolea. Agano letu ndani ya agano la kale ni Agano la Baraka na laana lenye msingi wake juu

ya sheria ya Musa, inahubiriwa na kuwekwa katika matendo hadi siku za leo . . Hata kama hatumo tena katika Agano la kale. Inci ya ahadi ya agano la kale imekuwa ndiyo Roho tuliyoaidiwa katika agano jipya. Baraka za mafanikio katika inchi ya ahadi zimekuwa baraka za kuwa ndani ya Yesu katika kila hali. Tumebarikiwa ndani ya Yesu, kwa sababu ya yale aliyotenda na baraka hizo za uzima mpya, zina amani, nguvu ya kutosha kutufanya wenye furaha, hata wakati tunapoteswa.

Kanisa la waebrania liliteswa, hata ***« …hivyo…tena mkakubali kwa furaha kunyanganywa mali zenu… » (Waebr.10 :34).*** Kama kweli tumeuona uzima wa milele, maono hayo hayo huyaweka pamoja nyakati na mambo yake yote katika mazingira. Hatupaswi kujibu kama waathirika, lakini tuwe na imani kwamba baada ya kufanya mapenzi ya Mungu, tutapokea ile ahadi. !

Paulo anasema kwa wathesalonika katika ***Wathesalonika 3 :3 « Mtu asifadhaishwe na dhiki ; hizi ; maana ninyi wenyewe mwajua ya kuwa twawekewa hizo…. »*** Hatukuitwa kwa ajili ya mafanikio tu, tumeitwa kuwa sawa, na Yesu na hiyo yaweza maanisha tumeitiwa mateso.

Wachina wa leo na wengine wengi katika mazingira yao ya mateso na dhiki wanafwata ile siri ya msalaba wa Yesu huku wa wakigeuza mabaya kuwa neema ya msamaha na laana kuwa neema ya Baraka. Baraka zina nguvu dhidi ya laana yoyote ile na msamaha una nguvu zaidi kuliko aina

yeyote ile ya ubaya. Hukuchagua lolote labda kwa yale yanayotokea kwako, lakini unaweza kuchagua nia yako na majibu yako. Uwe mwenye imani, imani, furaha na msamaha mbele ya upinzani ni ushuhuda kwamba kristo anaishi ndani yako.

**b) Tumebarikiwa ili tuwe baraka**

Yesu alitumia mfano mwingine na kusema tunapashwa kuwa « ***werevu kama nyoka, lakini wapole kama njiwa*** « ***(math 10 :16).*** Ndyo, tumebarikiwa ili tuwe baraka ! Huwezi kubariki wengine mpaka uwe umebarikiwa mwenyewe. Tunapashwa kutoa kama waliopokea bure ! Mambo haya ni baraka za msingi za neema, msamaha, uponyaji kufunguliwa, na upendo katika yote hata wale wanaotenda kama maadui, tumebarikiwa katika sehemu zote za maisha, kuanzia afya, ushirika,hadi pesa. Tunapashwa kuwa werevu katika kushughulikia mapato, Biashara na pesa na tumeamriiwa kutoingia katika madeni. Sawa na **John Wesley**, **mwanzilishi wa kanisa la Methodist** alivyosema ***» tuieka kadiri uwezavyo, weka kadiri uwezavyo, toa kadiri uwezavyo".***

Baraka kila mara huleta pia majukumu makuu kwa wale wanaoteswa na wale wanaokwenda ! Namna ya kukabiliana na Baraka ni somo lingine lakini kimsingi agano jipya linatambua maeneo mawili nayo ni kutoa na kupokea sadaka. Moja ilikuwa kwa ajili ya maskini na nyingine ilikuwa ni kwa ajili ya tume la kitume ili kutumika katika maeneo mapya. Lakini tukifanya baraka kuwa ndiyo lengo

basi itakuwa ni hatia ya kupata furaha, usalama, starehe na ukosefu wa lengo lenyewe !

Sababu moja iliyofanya Yesu aweke bayana hatari hii kwenye mstari wa mbele kabisa, ni kudhibitishia wanafunzi wake ushaidi juu ya dhiki, na namna wanavyopashwa kuitikia kwa njia ya upendo na msamaha na hivo alitaka yazama ndani ya nafsi za DNA zao. Hayo ni mambo ya kwanza ! Ndyo hata hivotukilinganisha na usalama wa watu wa inci za magaribi, wakati mtu anapokuja kwa Yesu, tuna sukumwana mara nyingi kumwambia aishirikiane na marafiki zake wa hapo awali, huku tukiogopa kuwa marafiki zake hao wa hapo awali huenda wakamshawishi akarudi nyuma. Hakuna hata ukakamavu mbele ya majaribu ya kawaida. Tunasahau kwamba, ***« aliye ndani yetu ni mkuu, kuliko aliye ndani ya ulimwengu »*** **1Yohana 4 :4) »** waumini hawa wapya huambatana nasi kwa hofu ya dunia na wanageuka baadaye kama wanaotufanana wanaongea kama sisi, na kutenda yale tuna yotenda. Wanakuwa sehemu ya nusu-mila ya kikristo, na baadae kama tunawaomba kwenda kushuhudia na kuwaleta marafike zao wa hapo awali kwa Yesu wanajikuta kwamba hawana tena rafiki yeyote yule wa hapo awale ! Urafiki wowote ule umevunjika. Sisi ndyo jibu kwa woga wa ulimwengu huu unaotuzunguka, na tunajiuliza tena kwa nini mvuto wetu kwa ulimwengu unakuwa mdogo sana. Tunaufanya usalama, ulinzi, na starehe kuwa lengo letu na hata tunajiuliza kwa nini bado tunaishi katika hali ya woga.

Tunapoifanya baraka , zaidi sana baraka za pesa kuwa muhimu, tunapoteza hazina ya imani, upendo na uhusiano.

Tumekuza Theolojia ya Mafundisho yasiyo sahihi juu ya baraka lakini kwa uzaifu sana Theolojia kuhusu dhiki na mateso. Paulo anataja orodha ya mateso yake ***(2 Kor.11 :23 – 33)*** kama alama ya kuwa « **mhudumu wa kristo** » na kumaliza katika ***(2 Kor.12 : 10)*** ya kwamba « ***nafurahi kuwa katika ufidhuli, udhaifu, misiba na adha, na shida kwa ajili ya kristo…Maana niwapo dahifu ndipo nilipo na nguvu !… »*** Tuna haja ya wengine wengi wanaoweza kutaja mateso kama alama ya uthibitisho wa huduma zao !

Majawapo wa tabia ya kusikitisha kwa madhehebu ya kale ya kiortdodoxi ni kuwa baadhi ya vijana huachana na Imani Wapokuwa watu wazima. Sababu labda yaweza kuwa kuto-andaliwa katika ujzi wala kutokuwa watendaji, na waangalizi wa utendaji wa mambo ya dini haijalishi maabudu ya kisasa, ao jinsi ujumbe uaonyovutia ? Tumeumbwa kuenda kwa imani na upendo. Tumefanywa kuishi kwenye ukingo kati ya falme mbili na kupunguza pengo ili wengine wengi na wao pia waweze kuingia katika safari hii pamoja na Mungu. Mungu ni hatari. Mungu hapendezi. Ni mwenye upendo lakini Upendo wake ni wa kikatili. Haubashiriki na unaelezwa pia kuwa ni kama moto ulao, ni kama maji yenye nguvu na upepo mkali. Tumeumbwa Kwa ajili yake. Hatukuumbwa kwa ajili ya uhakika wa Theolojia na mapokezi ya faraja. Tumeumbwa kwa ajili ya kuthubutu na uhusiano.

Vijana wetu wanaona uhakika mdogo kanisani kama tujuavyo sisi. Wanaona mabadiliko Mengi ya tabia, hotuba juu ya mikakati binafsi ya mtu ; sheria na uwiano wa nje wanafahamu la kutenda katika jamii ili wakubalike, wanainuliwa, wako salama, lakini ni wachache walio safarini waliozaliwa mara ya pili wanaofanana na upepo unaovuma upendako, ***"na sauti yake wuisikia, lakini hujui inakotoka wala inakokwenda" ( Yoh.3:8 )***

Kutembea pamoja na Yesu haimanishi ndyo kuwa salama. Inamanisha ni kusuthubu. Ina maanisha ni hatari ndivyo Yesu alivyoahidi.

***«hayo ni mewambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki, lakini jipeni Moyo Mimi nimeushinda ulimwengu» (Yoh.16 :33)***

Kutafuta mateso ni alama ya ugonjwa wa kiroho. Ni Kuandaliwa kwa ajili ya yale yatakayokuja kwa maana tunamfwata Yesu, hata mateso ni alama ya kuwa na afya kiroho. Baadhi ya makanisa mara nyingi hasumbuliwa na serikali mbaya. Baadhi husumbuliwa na chuki ya mashirika za kidini. Wengine husumbuliwa na makanisa yanayo shambuliya wale wote wasioikubali imani yao, matendo yao, ao mtindo wao Binafsi wa maisha. Paulo alizungumuza juu ya ana hizo mbalimbali za mateso katika ***2 wakorinto 11 : 26 "... hatari kwa taifa langu ... hatari kwa mataifa mengine ... hatari kwa ndugu za uongo... ».*** Kutembea pamoja na Yesu kutakufikisha mahali ambapo tutapimwa na hapo tutaelewa kuwa ni Yeye peke yake aliye rafiki, ngao yetu, mlinzi wetu, Bwana wetu na uzima wetu.

## MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

1) **kwa nini kueleza sana habari ya kumfwata Yesu ? hilo halitawafanya watu wakimbie ?**

Yesu katika ***Luka 14 : 26-33*** anasema kwamba hatuwezi kuwa wafwasi wake bila kuhesabu gharama ya kujikana. Na gharama hiyo aliiweka wazi.

Tunajaribu kuficha gharama na kukazia sana faida ! Ukweli ni kwamba njia ya tofauti utakazotumia kuwaleta watu kwa Yesu, zitakuwa kanuni za msingi katika maisha yao ya kiroho. Yesu anataka kutuandaa kwa huduma ya kutoa maisha yetu kwa ajili ya wale walio wadogo, kwa njia ya imani na upendo na katika kuyaacha yote ili kumfwata. Kwa jinsi hiyo Anataka kutupata kwa njia ya mwito wa kujitoa kwa ukamilifu kwake na kwa ajili yake yeye Tu. Anataka kutupata ili tuwe wake pekee na mwito wa kuishi kama alivyoishi.

Tuwapatapo watu kwa kujilinganisha na Yesu kupitia mwito wa asili wenye ubinafsi, unaotafuta anasa tutaendelea kujiburudisha na kukutanna haja za hali hiyo ya asili. Na wakati matarajio ya kimwili hayatoshelezwi, wanaacha na kusema kama ukriosto hauwezekani.

Hatupaswi kufurahisha watumiaji wanapokuwa wanafunzi.

Mwito wa kuyatoa maisha yetu una pashwa kuwa wa kwanza.

Mithali moja husema: ***"hatukupata kiwango cha ukristo, tumeona ni kigumu, lakini hatukujaribu!!"***

Ukweli ulio katika msemo huu ni kwamba hayo hayawezekani kwa nguvu zetu, lakini tu ni kwa neema kupitia kujitoa kikamilifu.

**2) Je ? hauamini kuwa Agano Jipya ni Agano la Baraka za vitu ?**

Hapana, Agano Jipya sio Agano la Baraka za mwili (vitu). Ni Agano la utukufu linalotueleza tu kutoa maisha yetu kwa Yesu, hilo litamletea Mungu utukufu haijalishe njia gani tunayoipitia.

Ishara ya msalaba hutenda kazi kubadili mateso yetu kwa utukufu wake.

Agano la kale lilikuwa ni Agano la Baraka za muda na baraka hizo kwa jumla zinaelekea familia, jamii na mataifa. Dhambi na ubinafsi huleta magonjwa, woga, upweke, umaskini na uharibifu lakini badala yake ***« haki huinua taifa »*** Mataifa hayatabarikiwa kwa sababu ya ubepari, ubinafsi ao kwa sababu ya demokrasia, lakini kutokana na kiwango ambacho Jamii lote kwa jumla wanafuwata zile amri kumi.

Agano Jipya ni agano lililo bora sababu ni kupitia agano hili, Mungu ana kuja kuishi ndani ya watu wake na wala sio tu miongoni mwa watu wake. Watu wake wana kuwa hekalu. Na utukufu wa hekalu hilo unastahili kuleta utukufu kwa Mungu. Haijalishi njia gani tunapitia.

# SURA YA 4:

## MFUKO, MKOBA, VIATU, NA SALAMU

***" Msichukue mfuko, wala mkoba, wala " viatu ; wala msimwamkie mtu njiani " ( Luka 4 : 10 )***

Tusomavyo shairi hilo hapo juu tunaona Yesu akitoa amri kwa

wanafunzi wake kumtafuta mwana wa Amani. Kuingia nuyumbani kwake kula na kunywa pamoja nao. Maagizo yake ni kwammba watakaa kwa mtu huyo na mtu huyo atawahudumia wakati wote watakaa nyumbani mwake. Tutafanya hivo, zaidi sana wakati ambapo tuna safiri bila pesa tutammtegemea mtu huyo kwa mahitaji yetu ya kila siku, hivo basi mfuko wa pesa kiukweli unakuwa kama ni picha ya mamlaka tuliyo nayo mbele ya mtu yule, na namna tutakavyotumukisha aina hizo mbalimbali za mamlaka[1]

Tukienenda na pesa zetu, tuna mamlaka ya kuanzisha' kisanga chetu Kidogo ' chenye matakwa yetu ndani ya kila aina ya mila, na ndivyo walivyo fanya mishonari kutoka inci za magharibi mahali pote ulimwengu. Ukienda kwa taifa lolote utaona jengo la kuenpeza lenye mapambo ya mtindo wa magharibi. Ndani yake utakutakuna majumba, kanisa na labda zahanati, nyumba ya kulea watoto yatima, na shule la Biblia. Watu wameutoa muda wao, pesa, na bidui nyingi kwa kuanzisha vituo hivyo mahali

[1] Tunatumia mfuko, mkoba, na viatu kama mifano ya mamlaka, mila na namna ya kutenda, siamini kuona hivyo litaazibu texte ao nia ya Yesu lakiini badala yake, ujuzi hutuonyesha namna gani mifano hii inafaa

ambapo mtu wa magharibi anajisikia vema, mwenye nguvu, mahali ambapo anaweza kuongoza. !

Misheni sasa inatafsiriwa kama tendo la kuwakusanya watu wengi kadiri tuwezavyo, watu kutoka mila mbalimbali kando kando yetu ili waingie kwenye maeneo yako kufundishwa na kupewa maelekezo, ya kuwa viongozi wa baadaye.

Kama desturi ya watu walio kando kando ni ya kihindu, kiboudha, ao ya kiislamu, jambo la uasi ambalo waweza kulitenda ni kuwa mkristo.

Hali hii huwavutia sana hsa vijana wanaochana na kukataa mila-desturi zao. Ndani ya bwawa la misioni wanabadili hata majina yao na kuwa na « majina ya Kikristo » , Wanabadili mtindo wa kuvaa, na wanajunza namana ya kutenda Kazi ndani ya Lile Ziwa ndogo kama **MARSHAL MCLUHAN** anvyo julikana kwa kusema, ***" njia iliyotumiwa ni ujumbe"*** . Na kadiri vijana hao wa kiume na wa kike wanavyofundishwa wanakuwa na uhakika kwamba njia pekee ya kuwa kiongozi ni kutumika katika bwawa kama hilo, ukiwa umevalia suti, ukiwa ukizungumza ukiwa madhabahuni ao ukiongoza toka ofisi iliyonunuliwa kwa pesa za wafadhili wa kigeni.

Tatizo lingine ni kwamba kuanzisha kituo kama hicho ni gharama mno. Na Kwa jinsi hiyo ni mambo machache yanaweza kujengwa. Kuna pia kukabiliwa na uharibifu, kwa maana waweza kulengwa na hisia zozote za wasioupenda Ukristo wala chochote kutoka magharibi kufatana katika mila hiyo.

Zaidi ya hayo , kuongoza ao kusimamia kituo Kama hicho kunahitaji bajeti kubwa, kupata wajuzi watakaoendesha huduma mmbalimbali yote hayo yana haja ya wajuzi na pesa kutoka inci za ngambo. Na hao wafadhili watoapo pesa zao kama msaada hutamani mara nyingine zitumiwe kadiri watakavyo wao. Lengo labda laweza kuwa kwamba baadae watawakabidhi " uongozi" "kwa wanafunzi wanao hitimu" wakati ambapo watakuwa tayari, lakini siku hiyo haionekani kutokea. Sheria ya dhahabu ni kwamba: ***"aliye na dhahabu ndye anayetoa amri "!***

Ukweli mwingine ni kwamba lisiloweka hufa. Kituo hichi hakiwezi kuendeshwa bila msaada wa nje. Urahisi unajikuza wenyewe. Mbinu zilizoelezwa na Yesu hapa ni kwamba kinachoweza kuzidishwa na kuendelezwa katika mila na desturi za mahali ndicho kinachokubaliwa. Kisichoeleweka na kilichotegemewa na Kanisa la Kichina, kiliaribiwa na MAO. Kilichokuwa rahisi na kuchukuliwa moyoni, kilizidishwa!

Lakini tatizo kubwa, sio tu kwamba wasomi walijiona wametupiliwa na familia zao, marafiki na desturi, na wamekuwa na matokeo madogo sana juu ya mila zao. Pesa zlizopotezwa hazikuleta mabadiliko yeyote katika mila, badala yake kukataliwa na mila hiyo. Tumetenda tofauti kabisa na yale tungelipashwa kutenda.

**B. MKOBA NA MILA**

Ninaamini Yesu hakuwa kinyume na mkoba, kwa maana mimi binafsi huwa nachukua mkoba mara kwa mara.

Mkoba, begi, landrover, ao meli ya kuchukua mizigo ni njia za kuchukua tabia zetu. Mkoba ni mfano wa elimu yetu yale tu-yapendayo, yale tusiyoyapenda, matakwa yetu, mavazi yetu, Mambo yetu, muziki tupendao, faida za kijamii, mila, ndoa, vyakula vyetu na kadhalika…

Mkoba unahusiana na mfuko wa pesa kwa sababu kama tuna pesa za kutosha tunaweza kuanzisha desturi zetu mahali popote tuendapo. Na ndivyo tulivyo fanya ulimwenguni pote. Hilo huchanganya mioyo na nafsi za watu wale tunaowaeleza habari za Yesu.

Je? Ni ufalme gani? Na mila yetu ni ya aina gani?

Jibu ni kwamba mara nyingi yote mawili hufanana!

Mara nyingine watu walio katika aina Fulani ya mila isiyopendelea mila za magharibi (ngambo) ( na hata hivo kuna baadhi ya mambo katika mila za ngombo ambayo Yesu anachukia) wanakataa pia mambo ya wakristo sababu wa mishonari kutoka magaribi walichanganya Yesu na mila yao ya vngambo (magaribi) kiasi cha kulingana kuwa na sawa na nafsi zao.

Mishonari wa kwanza kutoka ngambo walisifika sana kwa kuwa na lugha sahihi na desturi ya kuwafunza watu muziki, kuimba nyimbo kwa lugha ya kiholanzi, kijerumani, ao kingereza.Hatujui tueleze nini kuhusu kiburi ya aina hii kwa mila, lakini je ? hata leo Je ? tumefunguliwa na hayo?
Tunapenda watu waje kwetu. Wakati tunapowavuta watu kwenye maeneo yetu, katika desturi zetu, ambako tunatosheka na

kuthibiti mambo yote vizuri tunakuwa na nia ya kutenda jambo ambalo Yesu hakutuamuru kutenda na hilo hutufanya kuwa wanafiki **(Math. 23 : 15 ).**

Mnafiki ni mtu anayetufanana , anasema kama sisi, anaomba sawa na sisi na anazishika sheria zote zilizoandikwa, zizisioandikwa za shirika letu, dini yetu. Anaweka mkazo sana kwa mambo ya nje na kutaka kuonekana hadharani. Makanisa yetu yamejaa na watu wanaofanana, wanafiki wanaomba, wana-abudu, kwa namna moja, wanazi heshimu sheria na amri za jinsi ya kuishi ndani ya jamii.

Kuna mashirika mengine ambayo hali hii yakujifananisha ni kawaida yao, kwa wamoja kujipamba ni dhambi, kwa wengine unapashwa kuwa na hali Fulani ili ukubalike. Hali na mwanekano wa uje unafanya ukubalike, na hiyo hupelekea pawepo na kushindania vyeo, nia ya kutaka kutawala, wivu, rushwa , dhambi za siri.

**Eugene Peterson** analizungumzia hili katika tafsiri yake ya Wagalatia 4 :17 ***“ Mafundisho hayo yasiyo kweli yana lengo la kuwafariji, lakini shabaa ni mbaya. Wanataka kuwwaondoa kwenye ulimwengu huru wa neema ya Mungu ili mtegemee kungozwa na kukubaliwa nao, mkiwafanya watu muhimu”.***

Nikama sheria, mwonekano wa inje hutokana na kuzingatia sheria za dini na hiyo inakuwa kama kifuniko cha dhambi za siri. Tunaishi ao kwa neema ao kwa kuongeza mambo mengine.

Hali hiyo yaweza kuonekana namna hii. Yawezekana mtu alikuwa mfungwa wa dhambi Fulani ao kuishi maisha ya hatari. anaanza sasa kutenda lolote lile ili akubalike na kundi fulani la watu.

Kadiri mtu huyo anavyo yahatarisha maisha yake, kadiri anavyo -shangiliwa na kukubaliwa na marafiki zake.

Baada ya siku waweza kuchoshwa na mtindo (aina) hiyo ya maisha na kutafuta kubadilika. Lakini kama haja hiyo ya kukubaliwa hapatikani ndani ya Baba, ndipo wanashawishika kwa urahisi kutekelekea mipango ya shena za dini tu. Watabadili namna ya kuvaa, watatoa pesa zao, watahudhuria kwa kila mkutano. Wanataka kukubaliwa kutokana na mwenendo wao mwaminifu na wa kujitolea. Hata hwo baada ya muda Fulani watagundua kuwa wanatumiwa tu. Kama jibu kwa Jeraha hilo na Kwa maumivu waweza hata kurudilia maisha yao ya hapo awali. Kilichotokea ni kwamba walibadili pande moja kwa nyingine walibadili ujambazi kwa mipango ya dini. Hawajajifunza kamwe kuishi kwa neema na kwa upendo wa Mungu.

Shauku kubwa ya kutaka kukubalika ya watu wengi wana ofahamika kama watu wa kiroho, yaweza kusababisha nia ya kubadili mtindo wa kuishi na jinsi tunavyoonekana kwa inje katika jamii Kutenda hivo ni kutimiza sheria, ni kama kuchukua mkoba wa tabia za inje, ambao ni moyo haujateketezwa na Yesu.

Tatizo ni mabadiliko ya moyo. Mara tena, nikimnukulu ***« EUGENE PETERSON »***[2] lakini mara hii kutoka kwa utangulizi wake kwa kitabu cha wagalatia ***« kwa njia ya Yesu Paulo***

[2] Euqeue Peterson, the message, novpress1994

***alifahamu kuwa Mungu hatumii nguvu kuwafanya watu kutenda yale anayowaamuru, lakini ni mwokozi wetu aliyetuweka huru ili tuishi maisha huru. Mungu hatumii nguvu kwa inje, lakini anatufungua toka ndani »***[3]

Amri zote za Yesu, kama zilivyojumlishwa ndani ya hotuba mlimani, zinahusu sana sana nia ya moyo kama vile kusamehe waliotukosea, kuwarejeshea wale tuliowakosea na kumtafuta Mungu sirini kuliko kufanya hivo mbele ya watu sawa na watu wa dini. Mungu ni upendo wa ushirika wa nafsi tatu zinazoaminiana na kuheshimiana.

Msingi wa ulimwengu ni ushirikiano.

Kufanya wanafunzi kimsingi kasisa sio kuhusu imani ya kweli kwa maana Mungu sio computer ya Theolojia.

Ni upendo. Ulimwengu wake ni wa ushirika. Kuwafanya wengine kuwa wanafunzi kimsingi kabisa ni ushusiano kutoka Kwa moyo ulio huru. Hatuwezi kamwe kuingia katika nyumba ya mwana wa Amani na mukoba wa desturi zetu binafsi. Lakini na moyo wenye upendo, adabu na uhuru. Ufalme wa Mungu umo ndani . huo ndyo tunaamriwa kuupeleka ! Hilo ndilo tunaruhusiwa kueleza. Lengo ni kufanya marafiki na wala sio wanafiki.

## C) VIATU NA MBINU YA BRUCHKO

Vipi je ? Yesu anapinga nini kuhusu viatu ?

---

[3] Ibid, the message

Mwenyewe alikuwa amevaa viatu aliposema haya. Naamini kwamba katika **Luka 10,** neno viatu linaeleza namna tunavyotenda mambo, jinsi tunavyo kusudia kutembea na kushirikiana na Yesu.

Historia ya **Bruce Olsen**, mishonari mwanzilishi kwa wa-Metilone wa India **( waliomwita BRUCHKO** ) , jina la jiwe la kale la kabila moja la Amerika ya kati, inatufunza mengi. Alisafiri misituni bila chochote na miongoni mmwa mojawapo wa vijiji vyao. Hakuwa na mfuko wa feda ao mkoba. Aliishi miongoni mwao kama momja wao na alijifunza luga yao. Hakuwa na mawasiliano yoyote na inje , msaada wowote, vitu, dawa kutoka kwa kanisa la inci yake ya Amerika. Mara nyingi alikuwa karibu kufa kwa homa na daima alipambana na maradhi.

Baada ya miaka kadhaa, mwishowe akamuongoza kijana moja kwenye imani ndani ya Yesu na ndipo akaamini kuwa karibuni wengine wengi wengeweza kufwata. Hata hivyo alikatishwa tamaa na huyo mwamini wake wa kwanza, kwa maana alionekana kuwa na masito ya kushuhudia wengine habari za kristo akisema ya kuwa wakati bado. **Olsen** hangeweza kuelewa kwa nini mwongofu huyu mpya alikataa kushuhudia kwa yeyote yule. Na huku mila za kabila zilikuwa ni kueleza na wala hazi-kuandikwa popote pale, historia yao ilifahamishwa kwa kila mwanamemba alijifunza na kukariri kwa moyo, wakati wa jioni kila mtu kwa zamu. **Olsen** alisikia mara nyingi hotuba hizo, lakini hakujua maana hadi siku ambayo huyu mwamini wake alipomueleza kuwa jioni ile ilikuwa zamu yake ya kuhotubia. Hotuba yake usiku ule ilieleza ndoto ambayo mzee moja aliiota

hapo awali. Aliona mtu mwenye ngozi nyeupe aliyekuja kutoka mbali kutangaza kweli ya mwana wa Mungu katika sehemu yenye majani ya migomba ya ndizi. Mwamini huyo alieleza ndoto, akatafsiri na kudhibitisha utimilifu wake kupitia **Olsen** aliyeleta ujumbe wa Biblia. Usiku huo baadhi ya watu wa kabila hilo katika kijiji hicho waligeuka wanafunzi wa Yesu. Olsen aliache pesa na mkoba lakini bado alikuwa na viatu vyake vya kimarekani. Alitamani mwamini wake azungmze binafsi na kila mtu wa kabila lake akiwafundisha mwamini wake hakuelewa namna hiyo ya kuetenda alizoea ulimwengu wake wa kueleza hadisi na ujamaa, kuliko aina ile yakueleza kwa njia ya maandishi. Katika ulimwengu wa hadisi, habari huonesha ukweli wa hapo hapo na kujumuisha yote. Mtazamo wa wakati haukuwa sawa na ule wa N'gambo. Hakusukumwa na wakati. Alifahamu kuwa wakati wake wa kueleza utafika.[4]

Hapa ni tatizo la mila yetu ,ina maana sisi kama kundi Fulani,tunaamini kwamba Jinsi tunavyofikiri na kutenda mambo ndyo " Sahihi" na " kawaida". Na Jinsi wengine wanavyotenda mambo sio " sahihi na " ni " vibaya". Hata hivo hatusemi kuhusu maadili,nidhamu kuhusu upendo,kueleza ukweli,msamaha,kuepuka uasherati, na unyenyekevu. Agano jipya liko wazi kuhusu uhusiano kamili ambao twapashwa kuwa nao katika Mungu, ni wa Bure na wenye moyo safi lakini namna tunavyoonesha, uhakika wa na jinsi tunavyoishi vinakuwa tofauti kutokana na aina mbalimbali za mila, ambazo Mungu Msanii mkuu aliziumba kwa upendo na furaha.

[4] ''Brucko, '' Bruce Olsen, winsiw. Bruceolsion.conv

**D) HISTORIA YA NJIA YA NGAMIA.**

Inci moja ya kusini – mashariki mwa Asia Kazi ya wamishonari yenye zadi ya miaka mia moja iligeuka kuwa mlolongo wa madhehebu mbalimbali yaliyoingia incini, kujenga majumba, kliniki, masomo , na shule za Biblia. Walifundisha na kukazia sana kwamba waliobatizwa wanapashwa kubadili majina yao ya kiarabu kwa majina ya kikristo.

Walifundisha kwa kusisitiza sana kwamba walipashwa hata kubadili mavazi yao ili wasifananishwe tena na desturi za waislamu wa mahali pale. Matokeo ya hayo ni kwamba waamini hao wapya walikuwa na mvuto mdogo sana katika mila yao, kutokana na vile wanavyoishi, wanavyofanya kazi, kuoana, kuwalea watoto wao kwa mila ya watu wa n'gambo, katika jamii za kikristo. Maisha Yao ya kiroho yalijenga juu ya majumba na watenda kazi wenye ujuzi. Kanisa ndani ya mataifa liligawanyika katika madhehebu

Yanayofadhiliwa na kamati ya misheni…" wamoja wangesema ni hali ya kawaida tu!..*

Baada ya miaka mia moja ya Kazi za shirika mbalimbali za kimishonari katika taifa hilo lenye watu **milioni 160** hesabu ya watu waliobatizwa ni kama **100.000** na ukuaji umesimama.

Kama miaka kumi na mitano iliyopita, vijana wawili kutoka mila hiyo walimpokea yesu na wakafanya uamuzi rahisi wa kujitolea! Hawakubadili majina yao wala mavazi yao. Hawakujifananisha na mila ya N'gambo katika jamii la kikristo.Waliheshimu mila yao

na kutumia vifungu vya ukweli vilivyo katika mila yao kama kilalo cha kuwaleta watu toka mila yao hadi kwa Yesu.

Walipogundua kuwa kuna vifungo ndani ya koroani zinazoeleza kuhusu Yesu, Shura “Sura”, “Mwanamke” inazungumza juu ya Yesu kuzaliwa na Bikira, kutenda miujiza,kuwa mwenye haki,kuondoka na kurudi kwa Mungu. Kifungu kingine kinaamuru kusoma Agano la Kale na Agano Jipya kabla ya kusoma kitabu kingine chochote kile.desturi yao ya kiislamu inaneleza Juu ya vitabu vinne vilivyo muhimu kwa imani: Ndyo Kurani, Hadithi, Agano la Kale na Agano Jipya.waliona kuwa kwa kusoma kurani pamoja na kuuliza maswali kuhusiana na vifungu hivyo, wanaume wengi wengi wa amani watakuja na maswali kuhusiana na vifungu hivyo. Ndipowatwaalika nyumbani na kuwafanya kuwa wanfunzi wa Yesu na kuwabatiza.

Wanapoulizwa wanafikiri kuhusu Muhamadi,walinukulu kutoka kurani mahali ambapo Muhamadi anasema kuwa yeye ni Mutu anayeutafuta ukweli. Wanapoulizwa kuhusu Yesu,wanonyesha aya inayozumzia kuhusu yesus kurudi kwa Mungu. Kurani inaeleza kuwa Yesu hakufa, lakini ni Muhamadi ndye aliye kufa.Hakuna haja ya maelezo zaidi!. Waliepuka mabishano kwa yale wanayofundisha na waliheshimu kurani na kuiacha inzungumze pia.

Jamii za wanafunzi zilianzishwa ndani za nyumba, duka, mahali pa kuuza chai, maeneo ya Biashara na kazini. Walipoambiwa kuhusu mfano huu baadhi ya madhebu ya kidini walisema haiwezekani. Walisema wanafunzi hawa wapya hawataendelea kuishika imani yao, kwamba ni vigumu kwao kuishi bila ulinzi

wa jamii ya kikristo, ndyo baadhi yao walifariki kama mashaidi wa imani yao, lakini sasa mfano huo umekuwa na zaidi ye milioni moja ya waamini waliobatizwa na unaendelea kukua. Tunapo walinganisha na mifano mingine ya kimishonari, wao wamekuwa na wakristo mara kumi zaidi. Kwa muda wa moja ya kumi! [5]

Kuna njia tafauti ya kutenda mambo dhidi ya ile ya wamishonari waliojitolea Kwa mengi kuanzisha ufalme ndani ya taifa lile. Ndiyo wamishonari wa madhehebu walijitoa, walifanya kazi kwa bidii, lakini hata hivyo walichukua mfuko wao wa pesa, mkaba na walishikilia viatu vyao. Bado ni vigumu ao haiweazekani kwa baadhi ya watu hao kuamini kuwa Yesu angeweza kutenda kwa njia nyingineyo ile katika mila hiyo. Bado ni vigumu kwa Baadhi yao kuamini kwamba Mungu angeweza kuonekana katika mila ile bila usimamizi wowote toka kwao.

### E) SALAMU NA KUSUDI LAKE :

Kwanini " tusimsalimu mtu yoyote njiani" inaonesha chuki na kukosa uungwana inaonekana kuwa kinyume kwa maana kazi yetu ni ya kukutana na watu na kutafuta mwana wa Amani.

***"Basi baada ya hayo Bwana aliweka na wengine, sabini, akawatuma wawiliwawale wa mtangulie kwenda mwenyewe" (Luka 10:1***); Hao sabini hawangeenda katika kila mji ila tu mahali ambapo Yesu angepashwa kwenda! Yesu alikuwa kwamba alifanya tu yale aliyoyaona Baba akififanya ***(Yoh 5 : 19***) na kusema tu yale aliyosiki Baba akisema ***(Yohana 6:26}*** alitumika kwa sababu alikuwa na ushirika na Baba yake. Hakujibu tu Kwa mahitaji ya mwanadamu,ndyo wakati mwingine

[5] Ibe camel training maual le vin Greeson, ww charch laning movents.com

yale tuna yotendea aliye mdogo ni Yesu ndyo tunamtendea.. Ndiyo ***Mathayo 25*** na ***Isaya 58*** ni nanga na maelekezo ndani ya yote tunayo fanya, lakini watu katika Israeli hawakuponywa wote wote na Yesu, kuna wafu wengi amabao hawakufufuka.Wengi walikuwa na njaa hawakushibishwa. Yesu alitembea akizingatia uhakika wa mahitaji ya mwanadamu akikubaliana na Baba yake. Kulikuwa na miji mingi ya wasamaria ambamo hakuingia, lakini alingia katika mji mmoja wakati alitenda mapenzi ya Baba yake ***(Yoh 4 :34).***

Haja ya mwanadamu haistahimiliki, na inachoma moyoni kabisa. Kama jibu letu linazingatia tu kwenye haja tutajiharibu, kuwakasirikia wote wasioona mambo kama tuonavyoyaona sisi na pia tutamghadhibikia Mungu kwa kutotupatia yale tunayoyataka. Hatutaenenda njiani tukijaribu kuwa jibu Kwa kila haja. Sisi sio **Jehovah-Jireh**. Tunapashwa kufahamu Mungu anasema nini,kutizama yale Mungu anayotenda na kuenenda na yeye kupitia hayo .Ulimwengu sio wa kwako, na wala kanisa silo la kwako ! Ni ulimwengu wa Baba na na kanisa ni la Yesu Kristo. ***« Maana sisi tu wafanyakazi pamoja na Mungu, ninyi ni shamba la Mungu, ni jengo la Mungu. Kwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa, mimi, kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima, naliuweka mmsingi, na mtu mwengine anajenga juu jake. Lakini kila mtu na aangalie jinsi anavyojenga juu yake » (1Kor 3 : 9 - 10).*** Paulo alifahamu kwamba ni mtendakazi pamoja na Mungu na kuwa, kama mjenzi mwenye hekima, alijua mipaka ya yale aliyopashwa kutenda. Aliuweka msingi na kuwaacha wengine wajenge juu yake ! ni shamba la Mungu ni jengo la Mungu. Hauwezi kutenda yote peke

yako. Tenda yale uliyojaliwa neema kutenda na jambo hilo ulitenda vema. chanzo sio tu mahitaji ya mwanadamu n maisha bora ya mwanadamu. huo ni utu. Kiini ni Mungu na utukufu wake. Hiyo ndiyo kumfwata Yesu.

**MASWALI YANAYOULIZWA DAIMA :**

1. **wakati waamini wanaenenda katika mila kama unavyoeleza, hakuna hatari ya kuchanganya mambo ya mila hiyo na mambo yale tunayoyaamini ya Agano Jipya ?**

ndiyo !, ni hatari, hata hivo, tuna nguvu za kugundua mambo ya mila nyingi ya isiyokuwa na maadili mema yanapochangana na injili ya ufalme, lakini tuna uzaifu kwa kugundua hali yetu tunapochanganya mambo wenyewe (mchanga nycko wa mambo tuyachukuayo taka kwenye nina mbalimbali za imani). Baadhi ya watu toka magharibi wangekwazika kama mkristo mwenye asili ya kiislamu angeomba mara tano kwa siku ao akifunga swaumu ya kiislamu, hata kama mwamini huyo anamuomba Yesu, na kumtegemea, anamtarajia katika yote, na kuhatarisha maisha yake kwa kufanya hivo. Hata hivo mina wasiwasi kwa jinsi hali ya kupenda vitu, ubinafsi na tamaa imeingia wengi na kufanya mafanikio kuwa ibada katika ! Makanisa mengi. Nina wasiwasi zaidi kuhusiana na idadi kubwa ya watu wanaokazia sana desturi, karama, utu, umaarufu na faida na kulipindua kanisa nzima kumwabudu mtu. Tumebatiza tamaa ya pesa kwa nia takatifu na mitindo ya maisha isiyOfaa, kuwa ndyo baraka za Mungu.

2. **kama hauchukui pesa, ni jinsi gani utuwasaidia maskini ? Je? Hiyo sio sehemu ya kazi yetu?**

Ndyo, tunachangiza pesa kwa makusudi mawili ya msingi, kutuma tume za kitume kwa majimbo mapya na kuwasaidia maskini. Hiyo ni sehemu ya kazi yetu.

Sasa ulizo ni namna gani tunatekeleza kazi hiyo ? kwa maoni yako ni njia gani njema ya kuwasaidia mayatima katika jamii ya wakulima vijijini ? Tujenge Mashirika yenye mtindo wa magharibi yanayo dhamiwa kipesa na magharibi ? kwa maendeleo yake ao tusaidie familia za mahali na kuwafundisha kuwashughulikia mayatima ? Kwenye vituo vya kutunza watoto yatima vya huko magaharibi, wana maji yenye joto bafuni, vyoo vya kisasa wakati ambapo katika nyumba z hakuna vifaa kama hivyo ndani. Njia bora ingekuwa ni vipi ?

Shirika la mtindo wa magharibi linahitaji pesa nyingi na linaweza tu kusaidia ma yatima wachache katika jamii. Kuna hitaji la ujuzi mwingi hata inakuwa vigumu kuzidisha. Wenyeji hawawezi kuliongoza ao kulikuza kwa njia ya kutunza mayatima katika vijiji na miji yao. Ni vigumu na inahitaji pesa ambazo hawana. Mashirika kama hayo yanakuza umaskini, kutoweza, na hali ya kutengemea ya jamii la mahali. Waandaa watoto ambao pia hawawezi kuishi katika jamii zao za mahali, wanaopendelea sasa kuishi maisha yenye mtindo wa magharibi. Na sasa kama tungesaidia familia za mahali ku-washughulikia watoto wao na mayatima katika nyumba zao? Hali hiyo ingefananaje ? hali hiyo ingefanana na vile marafiki fulani wanavyofanya huko Kenya walipo saidia famila moja na msaada wa pikiki ili waweze kupata pesa kwa kuitumia kama « taxi » na kupeleka watoto ishirini. Watoto wanaishi kama

watoto wengine katika mila hiyo. Ni mfano  rahisi tena unaoruhusu kuongezeka katika mila hiyo. Mfano huu unatupa matumaini kidogo ya kutoa nyumba za kutosha kwa mayatima wote katika mila hiyo ! Kwa sababu unaweza kuendelezwa kwa pesa za hapo hapo nyumbani. Mfano huu unasababisha ubunifu,  kuwa na vianzo, na unaumba hali ya kujitegemea.

Hatungeweza kamwe kujenga ao kuwa na watenda kazi wa kutosha ili tuwe na vituo vya mayatima sawa na vile vya inci za magharibi kujibu haja iliyopo ; sasa kwa nini tuaendelea kufanya miradi yenye gharama ghali na inayohitaji idadi ya watu wenye ujuzi ? Inatufanya tujisikie vizuri, inatufanya tujisikie kuwa na nguvu. Ndyo mfumo huu  sasa unabadilika,lakini bado kuna namna nyingine nyingi za kusaidia kuingia katika sehemu nyingi.Tufikiri sawa na mahali petu, kwa njia rahisi  inayojizidisha, bunifu,, inayodumu na yenye kujitegemea .

3. **Unafanyaje ? kwa mahitaji usioweza kuyapatia jibu ?** unaamini kwamba Mungu anaona mahitaji kwa undani zaidi kuliko sisi ? unambea watenda kazi kwa ajili ya shamba hilo ? unaomba Mungu kuzidisha mapato yetu yaliyo madogo ? unaomba kwa kupata mawazo mapya yenye ubunifu ili kusuluhisha matatizo yao ya awali ? mnatafuta ufadhili kwa mashirika yaliyo na mwito tofauti na wenu ili mpate misaada na pesa ? je ? mnafungua milango kwao ? wala  mnamuwekea Mungu mipaka kwa yale mnayoweza kutenda ?

inci ya Brazil ina tatizo kubwa la watoto wa barabarani. Watoto hao wanatumia madawa ya kulevya, wana vuta sigara na kuiba ili waishi.Kwa upande mwingine Askari polisi wa mahali hapo wanafamika kwa kuua kwa kuwapiga risasi kama mbwa. Tuna marafiki ambao wameanzisha vituo kwa ajili ya mayatima hawa kwa kuwajengea nyumba ambamo watoto 1o ao 12 wanaweza kuishi pamoja na Baba ao mama Mlezi. Nyumba zao ni nzuri lakini bado maelfu ya watoto yatima wanasalia barabarani Muungano Mmoja wa Makanisa ya Brazil uliuliza serikali kutenda lolote lile kuhusu watoto hao wa barabarani. Je ? kwa uhakika ni wajibu wa serikali ? rafiki zetu walituambia,kama kila kiongozi wa makanisa ya injili Brazil angelichukua angalau mtoto mmoja,hapangekuwepo na watoto wa barabarani.

Huko Mozambique **Roland na Heidi Baker** wamepokea mayatima wengi lakini sehemu ya mafundisho yao kwa wachungaji wao wa mahali ni kwamba wauige mfano wao, wawachukue mayatima katika nyumba zao.Baadhi ya viongozi hao wa kanisa la mahalini maskini na mara nyingine hawawezi hata kutosheleza mahitaji ya watoto wao wenyewe,lakini wanashughulikia wengi.Mungu anheshimu aina hii ya Imani.Je ?unakabiliana na na mahitaji usioweza kujibu ? fwata shauri la **Mama Theresa**, » ***Tenda Lile Uwezalokutenda, Usilenge sana lile usiloweza kutenda na usitazame yale wengine hawakuyatenda.. »***

4. **Utafahamuje ? mahali Mungu anakutuma ? Yesu alitaja miji ambayo wataingia. Ni Jinsi gani tutafahamu mahali pa kwenda?**

Tunapashwa kusikia na kutenda ndyo , kwa maana msingi wa kanisa ni mitume na manabii. Tunaweza kuwa na mawazo mengi mazuri tu, lakini je? Tunasikiliza? Je? Tunatambua lugha ya ndoto na maono sawa **Petro** katika ***Matendo 10*** ao **Paulo** katika ***Matendo 16 ?*** Je? Tunatambua kufunguka kwa milango ya urafiki na uhusiano na Mungu sawa na Paulo katika ***Matendo 18 : 1-3?*** Je? Tuna sikiliza tamaa toka moyoni mwetu? Mungu ameweka kitu gani ndani mwako?Je ? unaota kuhusu nini? Unaombea nini ? Unafikiria kuhusu nini? Una imani na neema kwa ajili ya nini? Je uko tayari kuanzia mahali ulipo.

## SURA YA 5 :

## AMANI YAKO NA MWANA WA AMANI

***" Na nyumba yoyote mtakayoingia, semeni kwanza, Amani iwemo nyumbani humo; na akiwemo mwana wa amani, amani yenu itamkalia; la hayumo amani yenu itarudi kwenu" LUKA 10: 5 – 6.***

### A) AMANI IWE NAWE!

Salamu ya kawaida miongoni mwa jamii yenye desturi za kislamu ni ***'AS-"SALAMU- ALAYKUM"*** yenye maana ya ***" amani iwe nawe***! Jibu ni ***"WA-ALYKUM AS SALAAM"*** , " ***Amani iwe nawe pia.*** Hivo ndivyo anasema hapa. Ni mtu wa mashariki, mwenye mila ya mashariki.Je, unafahamu kuwa wewe ni balozi wa ufalme wa Mungu unayechukuwa uwepo wa mfalme mahali popote uendapo? Je? Unafahamu mamlaka yako kama balozi kuhudumia amani ya ufalme? Je?unahudumu amani ambayo itabaki katika nyumba? Je ? unaingia kwenye maeneo mapya ukiwa na Amani wala woga? Je? hao wasiomjua Yesu hujisikia kuwa unawapenda ,unawakubali, n kuwapa amani kuliko kuwa hukumu na kujiona bora? Bwana wetu aliitwa "Rafiki wa wenye dhambi" Je? Nasi tunaitwa kwa jina hilo? Makahaba walimtafuta maana walifahamu nia yake kwa ajili yao ilikuwa sahihi nay a haki na aliwakubali. Watoza ushuru walijisikia vizuri pamoja naye sababu hakuwahukumu.

Jambo la kwanza la muhimu ni kuhudumu amani. Wakati mingine tunafurahia mijadala, mabishano na tuna sababisha kupingwa na kukataliwa, na hali hiyo hutufanya kusema, tulijaribu kuwashuhudia lakini walikataa. Roho ya dini huleta Kiburina kufurahia mabishano ya maneno. Labda wana kataa mbinu zetu, lakini sio Yesu ? Hatua ya kwanza ni kuhudumu amani. Kweli ndyo inakuchukua. Sio wewe ndiyo uichukue kweli! Jiachilie mikononi mwake. Yesu, ni njia, kweli na uzima alikuja kama rafiki aliyetamani kutumikia. Wewe. Sio mtetezi wa kweli-kweli inakutetea wewe. Amani iwe nawe!

## B) KUMPATA MWANA WA AMANI

Mtu huyu anaitwa **“Mwana wa Amani”** sababu kuna watu wanaotafuta . Mungu amekuwa akitenda kazi mioyoni mwao na tunapashwa kugundua ni wapi Mungu anatenda kazi.Ni jinsi gani twaweza kumpata mtu wa aina hiyo?. Ndugu walioanzisha kundi “alama za Ngamia” , wangeweza kuingia wakati mwingine ndani ya msikiti na kuomba kusoma kuroani kwa waanaume waliokuwepo pale. Wangesoma “SURAT “ Ya mwamamke” na kuanza kuuliza maswali juu ya maana yake. Maswali yaliyoulizwa yalilenga kuzaa maswali mengine mengi zaidi. Maswali ambayo huelekea zaidi kwa maswali kuhusu Yesu na kuhusu “NINGEL”, yaani Agano jipya. Wakati mwingine ilitokea warudi tena kwa mjadala mwingine. Mara nyingine mwanaume mmoja angeliwafwata inje na kawaomba waje nyumbani kwake na wamletee Agano Jipya... Wangeweza kuwa na mazungumzo mara kadhaa pamoja naye na mwishowe kualikwa warudi mara tena na wafikapo wanakuta nyumba imejaa marafiki na familia wa karibu ili wafundishwe “sasa waambieni lolote mliloniambia”.

Maono na ndoto ni mambo ya kawaida sana miongoni mwa waislamu, kiasi cha kwamba , njia moja ya kuanza mazungumzo ni kumuuliza tu kama amewahi kuota ndoto ao kuona maono. Ikiwa mtu huyo amwahikuona maona ya Yesu,anaweza kushangazwa na swali hilo.watashangazwa zaidi ikiwa utauliza kama maono hayo yalihusu mtu mwenye mavazi yenye kung’aa na ambaye walijsikia kuvutiwa naye.

Ukimpata mwana wa amani,amani yako itakaa katika nyumba hiyo.Ikiwa La!, Amani yako itarudi pamoja nawe utakapoondoka. Upako, uwepo wa roho makatifu , na amani hii zina nguvu na ni sehemu, ya ushuhuda unaouchukua. Ukimpata mwana wa amani, atatambua amani unayohudumu na hiyo itakuwa kwa sehemu kubwa kwake yeye kufungua moyo wake na nyumba yake kwako. Ndiyo, watu wanaweza kuhusisha vipaji vyao, tunahitaji kuwa na busara, maana hili halitendeki kwa sababu ya uwezo wetu wala elimu yetu. Inatendeka kwa sababu Mungu anatenda kazi ndani mwao na kupitia wewe Yesu anaita hilo ni msisimko wa amani. Ni aina gani ya nguvu za Mungu iletayo amani mioyoni mwetu mahali ambapo kwa kawaida pangekuwepo chuki na matengano.

Mwana wa amani aweza kuwa mwamini wa kwanza katika kijiji ao kundi la jamii Fulani. Ushuhuda wao waweza kuwa wakuvutia na kufungua kijiji chote hicho ao kundi la watu kumpokea Yesu . Hivyo ndivyo ilivyotokea kwa Yule mwanamke kwenye kisima katika ***Yohana sura ya 4*** na mtu , aliyepagawa mapepo katika ***Marko 5:19.*** Mwana wa amani anaweza kuwa mtu anayeheshimika sana katika jamii lake. Kuna shuhuda nyingi zinazotujia kutoka kaskazini mwa Afrika, ambako viongozi wakiislamu wanageuka kuwa wafwasi wa Yesu na kuiongoza hata miskiti yao kuwa wafwasi wa Yesu vilevile.

Mtu huyu mwenye kuheshimika mwana wa amani ni sehemu ya historia ya Petro na nyumba ya Kornelio. Katika ***Matendo 10*** na vivyo hivyo k,atika historia ya Paulo na

Sila na wokovu wa mfungwa wa Filipi. Katika " kesi zote hizo mbili " Yeye na" familia yake walibatizwa".

Mwana wa amani anaweza kuwa mwamini wa kwanza , lakini lengo lako lingekuwa kuona familia yote ikibatizwa kwa mara moja. Mara nyingi tunakuwa haraka kubatiza na kumtenga mwanamemba moja wa familia na wengine. Ingekuwa vema kufasiria Biblia kwa familia yote na kuwafanya kuwa wafuasi wa Yesu, ndipo kuwabatiza kama kundi. Kwa maana ubatizo ni sherehe pia ya kusherekea kuanzishwa kwa kanisa.

## MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA :

### NI VIPI TWAWEZA KUMPATA MWANA WA AMANI KATIKA MIJI YENYE MILA NA DESTURI ZA MAGHARIBI?

Tumekuwa na mazungumzo ya kutosha kuhusu namna ya kumpata mwana wa Amani katika miji yenye mila ya magharibi. Kulingana na ***Luka 10*** ni wazi kwamba miji na vijiji ni mahali ambapo vizazi vitatu na familia zenyi kaka na dada pamoja na watumwa wao wanakuwa nyumba yenye watu ishirini ao arobaini. Kuishi pamoja nao na kuwafundisha huyo mwana wa Amani kuwa mchungaji/mzee wa familia yao na wa marafiki zao wa kuona mtindo huo ukiongezeka kata kwa familia zingine. Hayo ndiyo yanayotendwa hivi sasa sehemu mbali mbali zenye mila ya ulimwengu wa tatu. Na mtindo huo unakua na kuongeza mpango wa kuanzisha makanisa.

Twawezaje kutekeleza mbinu hizi za kutoka katika ***Luka 10*** katika ulimwengu wenye mila ya miji na mila ya magharibi ambayo ubinafsi ni kawaida na ushirikiano katika familia haupo? Je? Mafundisho ya Yesu katika ***Luka 10*** Yaweza kuifikia mipaka yeyote ile ya mila? , " Ndyo-huyo ndyo Yesu tunayemzungumzia !.Huko magharibi" Famila", ni watu ambao tunakaa sana kwa muda mwingi, wanaelekea kuwa watu wa aina tafauti za kundi ambao wana shauku. Tatizo sio la mavuno. Ni kule kuendelea kungoja mavuno yakujie? Kumbuka Yesu hakusema kamwe wangeweza! Alituamuru kuomba kwa ajili ya watenda kazi ambao wangekwenda na atakutuma kwenda kama jibu la maombi yako mwenyewe.

**Baadhi ya mifano ya kisasa ya watu wa magharibi**..:

Kiongozi wa kundi moja lenye huduma nyingi uingereza alijiunga na klabu ya Kriketi ya mahali na akajitolea sana kwa vyovyote vile katika klabu hiyo.

Matokeo? Baadhi ya wanamemba wengi toka klabu hiyo wamebatizwa kama wafwasi wa Yesu. Rafiki mmoja wa kike huko ujerumani alisikia maelezo ya wazi kwenda kwenyi Bar ya hapo mjini kwao. " Bwana sijawahi kwenda kwa Bar maishani mwangu kwa nini sasa?" Alikwenda na akaketi kwenye meza na wanawake wengine waliokuwa na shauku ya mambo ya kiroho, walikusanyika kwa ajili ya mazungumzo yao ya kila wiki. Wakamkaribisha kwenye mazungumzo yao, Baaada ya kuwasikiliza kwa wiki kadhaa na kuyajibu maswali yao,wakamwalika achukue jioni yote awaeleze kuhusu uhusiano wake na Yesu. Alifanya hilo katika nyumba

hiyo ya Amani, ikafuatia chakula cha pamoja “na waume zao , na wakagundua kuwa mmoja wa waume zao alikuwa akiisoma Biblia na kujiuliza kama” Je? Kuna mtu awezaye kunisaidia kuilewa?”

Rafiki mwingine mjerumani ,alianza kukutana na wasiokuwa na mahali pa , na waathirika mbalimbali kwenye kituo cha mabasi. Matokeo? Wanafunzi wengi wa Yesu walibatizwa na kundi la Yesu likaanzishwa katika kituo hicho. Mmoja wao, kwa utoto wake alikuwa ametendewa vibaya sana , na alikuwa akiishi barabarani kwa muda wa miaka 15.

Unatamani kuwa mchungaji? Kwa nini basi usiwe mchungaji (mzuri, mwalimu) wa timu ya spoti ya mwanao? Rafiki mmoja wa karibu alitenda hivo na kukutana na Baba moja aliyehisi kuvutiwa naye. Kwa muda Fulani Baba huyo aliacha kuhudhuria kwenye mazoezi ya mwanae na hata kwenye mechi. Rafiki yangu aliendelea kumwita kwa simu, ila Baba huyo alikuwa hapokei simu. Hadi siku ya kuamkia noeli ndipo alipojibu simu na kueleza kuwa alikuwa katika hali ya kukatishwa tama tayari kujinyonga. Huo ndyo ulikuwa mwanzo wa majadiliano mengi na sasa Baba huyo na mke wamekuwa wanafunzi wa Yesu. Tulikutana na Petro na Dunshabe , Tujikistan, waanzilishi wa huduma moja hapo. Walikuwa wakitangaza masopmo ya delta plane na vifaa vyake walivyogawa bure. Vijana walitaka sana mchezo wa huo, lakini hawakuwa na uwezo wa kutosha. Petro alianzisha nyumba yake mwenyewe ya Amani kwa njia ya mchezo huo wa delta plane miongoni mwa vijana hao. Katika mji wa

New York, kuna mtindo miongoni mwa jamii ya wanaosema Lugha ya kihispania ambayo inajulikana kama "KUNDI ZA MAWASILIANO". Watu wanaofurahia Yesu wanaalika marafiki, familia , na watu wanaofana nao shughuli mbalimbali za biashara kwanye n yumba zao na kwenye hoteli mahali penye chakula , filamu, mazungumzo na maombi kwa wagonjwa. Wakati watu hao wanapokuja kwa Yesu, hilo kundi la mawasiliano lina weza kuwa kanisa la nyumbani na kundi zingine za masiliano ziliundwa katika miji mikuu na mseto wa inci za magaribi . Nyumba ya Amani inalekea kuwa ni kundi ya wafanya biashara ao ya wahamiaji. Roho mtakatifu ndye muumbaji wa ulimwengu- kwanini makanisa mengi yananekana kutoumba? Muulize yeye. Uote pamoja naye. Utembee kwa imani na upendo pamoja naye. Mpate mwana wako wa Amani.!

Mwisho wako upo mahali mavuno yako yalipo. Mavuno yako yapo mahali mwisho wako ulipo!

## SURA YA 6 :

## TUMERUHUSIWA KULA NA KUNYWA

***" Na akiwemo mwana wa Amani, Amani yenu itamkalia, ; la, hayumo Amani yenu itarudi kwenu. Basi Kaeni katika nyumba hiyo hiyo, mkila na kunywa vya kwao ; maana mtenda kazi amestahisli kupewa ujira wake. Msihame-hame kutoka nyumba hii kwenda nyumba hii."***

***(Luka 10 :6-7).***

## A) UAMINIFU KATIKA USHIRIKIANO NA KUONGEZEKA

Unapopata nyumba yako ya amani, kaa hapo. Kama **Peterson** anavyosema katika ujumbe " msihame hame toka nyumba hii kwenda nyumba hii mkitafuta chakula kilichopikwa vema katika mji ". Mara tu unapopata nyumba ya amani, heshimu nyumba hiyo. Onyesha uaminifu wako kwa ushusiano huo, kwa kujitolea na urafiki. Kama Mungu amekuongoza hapo, weka kando kabisa aina yoyote ya kutoelewana na matatizo na ukae hapo. Tenda ili iwezekane. Amri ya kubaki inalingana na amri ya Yesu ya kwenda kufanya wanafunzi, kuwafundisha kutii yote yesu aliyotuamuru. Hatuhesabu kadi ya kufanya maamuzi. Uhusiano wako na nyumba yako ya amani sio tu tukio la mara moja. Ni la muda mrefu ! unakaa katika nyumba, unashirikiana nao, na haundoki kwao hadi kazi ya kuwafanya kuwa wanafunzi imetendeka na wataendelea kuwa marafiki. Unawafundisha namna ya kuwa mchungaji wa famila na wa marafiki zao katika nyumba yao wenyewe. Rafiki yako mpya aweza kuwa huru kuja nyumbani kwako lakini familia zao na marafiki zao hawawezi. Hauhitaji kukusanyika peke yako. Unahitaji kuziendea nyumba mpya na kumfundisha mwana wako wa Amani kutenda vivyo hivyo. Unahitaji kuongezeka wewe peke yako na waweza kuona kukua , wakati wanafunzi wako wapya wanafanya vivyo hivyo , utaona kuzidishwa. Kufikia kizazi cha nne hatutaongoza tena. Ufunguo ni kuuzidisha uhusiano mzuri.

Yesu alikuwa na wanafunzi 12 na alikaa pamoja nao kwa miaka mitatu. Aliuaga mkutano pale walipotaka kumfanya

mfalme. Aliyaweka maisha yake ndani ya wale kumi na wawili. Hakuongoza juu ya wale kumi na wawili kwa maana hakupenda kuharibu hali na tabia ya uhusiano aliyokuwa nao pamoja nao. Nimesikia shuhuda nyingi za uhusiano wa karibu, wenye furaha , uanaopendeza kwa watu wakati walipoanza kanisa katika nyumba ya mtu. Walikuwa haraka na karibuni tu wakaona haja ya kuwa na jengo na kadiri walivyokomaa wakaanza kupoteza ile tabia ya ushirika wao wa kwanza ? badala ya ushirika, zinakuja mipango (programu) na kadiri wanavyofanikiwa kuwa wengi kwa idadi ya watu,wanaupoteza upendo wao wa kwanza. hiyo ndyo matokeo ya kuongeza kwa kujumlisha.Yesu hakupoteza tabia ya Uhusiano kwa kuwaruhusu wengine kujiunga na kundi la wale kumi na wawili(12). Nafikiri kuwa huenda kuna wengine waliotamani kujiunga lakini hakuwaruhusu. Kama kila mmoja wa wale kumi na wawili angelikuwa na kundi lake binafsi la wanafunzi, Je ? Wangefurahia aina ile ya tabia nzuri ya ushirika. Kukomaa ni kwa njia ya kuzidisha na kufanya vizazi vipya vya wanafunzi. Na wala sio mtindo wa mipango ya kuuza biashara bali ni uhusiano halisi katika maisha

**B) KULA,KUNYWA,KUKUBALIWA,MWENENDO NA UHAKIKA**

Tumegundua kuwa kila mila ina uwiano na nyingine kwa njia moja ao nyingine. Unapokula na marafiki wapya , wana wasi wasi kutaka kujua kama umefurahia chakula . Kwa nini? Ikiwa unafurahia chakula Utawaonyesha kwa kukubali na kufurahia mila yao, yale wanayopenda ,na yale wasiyoyapenda, zawadi yao kwako, mwishowe ni kwamba umewakubali.

Amri ni kwamba tule na tunywe " yote hayo wanayotupa" , ni amri yenye nguvu katika desturi ya wayaudi wenyi itikadi kali ambao walikataa kula baadhi ya vitu eti kwamba " ni najisi".

Kuleni kila kinachowekwa mbele yenu? huu ulikuwa ni mjadala mkali ulioleta mgawanyiko ambao Petro alihitaji maono makubwa yaliyoonekana mara tatu kusudi aelewe na kukubali. Kwa sababu ya ndoto hii alikuwa tayari kula vyakula visivyotakasika pamoja na mataifa ndani ya nyumba ya Kornelio ***(Matendo 10***) na kuutetea uamuzi wake huo baadae mbele ya mitume wengine katika **(Matendo 11).**

Tazama utaratibu katika “ ***Luka 10:1-9…***” Tunapashwa kula , kutumika, na kutangaza ufalme wa Mungu. Kula chakula pamoja huonyesha kukubaliana, lakini kwa mila ya siku zile kula pamoja kulikuwa na maana yenye nguvu zaidi. Kuumega mkate na mtu mwingine ilimaanisha kuwa unajitolea kuwa rafiki yake maishani. Yesu anarudilia amri hii ya kula mara tatu. Kwa hiyo basi tunapashwa kutumka, na tunapashwa kutangaza” ufalme wa Mungu umekaribia”.

Tueleze hilo kwa njia nyingine namna hii, kwanza ukubaliwe, ushirikiane, na familia, na pili mwenendo, kutumika, kukutana na mahitaji, na mwishowe kutangaza ufalme. Kuwa katika ufalme, kuishi maisha ya ufalme na imani. Baadhi ya makanisa ya kiinjili yamegeuza mambo hayo matatu. Tunawaomba watu kwanza wakubaliane na aina ya ukweli wetu, waamini kwa njia ile tunayoamini na baadaye waishi kama tunavyoishi sisi na wakifanya hivo, ndipo tunawakubali sasa kuwa miongoni mwetu. Kukubaliwa kwetu kuna

zawadiwa kwa yale tunayo kwa wengine kwa kuamini, sawa na sisi na kwa kuishi kama tunavyotaka sisi. Yesu hakutenda hivo. Alikwenda kwa nyumba ya Zakayo ***(Luka 19)*** na kwa sababu ya hali ya kuwakubali watu na urafiki, zakayo alipokea uhakika , imani na neema iliyobadili tabia yake. Ombi la kwanza ni kuwa mtume mzuri sio kuwa na miaka mingi ya elimu, bali ni yeyete Yule anayeweza kufurahia kila aina ya watu na mwenye uwezo wa kula na kunywa pamoja nao! Mpango wa mafundisho yenu ukoje?

## C) KUSTAHILI MSHAHARA NA TATIZO LA MAJUKUMU MENGINE

Kuzungumza kuhusu pesa kwenye mila , kundi la uchumi na katika lugha ni vigumu mno, lakini unapoongezea tofauti za mila na tofauti za kiuchumi, una kuwa na shida halisI. Tunapotaka kujenga uhusiano katika mila mbali mbali, hakuna swala linalozua matatizo mengi kama swala hili la kusimamia pesa. Yesu anatupa mwelekezo wa namna ya kuepukana na matatizo haya. Alisema " kama watu waliotumwa, mnategemea ukarimu wa nyumba ya amani. » Wewe, kama mtenda kazi, unastahili mshahara hayo yote yanahusu majukumu na kama mtu hakubali majukumu tangu mwanzo yawezekana asiwajibike .Kama mtu mwenye vya kutosha akimjia mwenye vitu vichache, inatokea mara nyingi kuwa wale walio na vichache hutegemea walio na vingi. Kutegemeana kunaharibu uaminifu, heshima ya mtu, na utu. Hatustahili kuumba urafiki wa kutegemeana. katika ***Yohana 15*** Yesu

aliwatizama wanafunzi wake kumi na wawili na kuwaita marafiki.Hakutumika nao kama watumwa.Hatustahili kuwa na miradi, tunataka kuwa marafiki na kutendewa kama marafiki.

Hata hivo, rafiki huwa hatamani kuwa mzigo chakula kwa wengine. Ndyo marafiki hujitoa mmoja kwa mwingine na kujitoa huko ndyo heshima katika kila mila. Mtihani mmoja wa nyumba ya amani ni mtihani wa ukarimu. Je ? Watuchukua jukumu la kumtunza aliyetumwa na kushughulikia marafiki zao na familia zao binafsi. Je ? Ni wenye kuwajibika na watoaji ? Yesu yuko wazi kwamba mahitaji yetu ya kila siku ndyo wajibu wa pekee wa nyumba ya amani kwa yule aliyetumwa. Hilo ni tafauti na dini ambazo daima zinanyanyasa na kuchukua kutoka kwao. Dini hujenga mahekalu, zinatoa vyeo , gari,nyumba na viwanja kwa makuhani wao.Aidha watu ni maskini ao tajiri wananyanyaswa juu ya pesa na kuambiwa watalaaniwa wasipotoana watabarikiwa wakitenda hivo. Kanisa la hapo kale la kirumi liliuza vitu kwa kupata baraka za maisha yajayo wakati ambayo sisis watu wa kizazi cha sasa tunauza baraka za maisha haya.

Dini kila mara ina baraka za kuuza ! Dini kila mara ina hatia na laana kwa wale wasionunua baraka zinazotolewa. Dini inawaweka watu katika hali ya umaskini. Kwa kiwango hicho baadhi ya yale yanayoitwa makanisa za Yesu Kristo yamegeuka kuwa ibada za mafanikio bila tofauti na dini zingine. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuwa walipokea bure na watatoa bure. Ufalme wa Mungu umetolewa bure na bure tumepokea. Yale tutumiao kuwavuta ndiyo yale tutumiao

kuwapata. Tuwapate na ufalme? Wataishi katika ufalme. Tuwapate na mchele? Wataitaji mchele zaidi. Ukiwaona watu kiama njia ya kupata pesa na kuwa ujanja kuwaomba pesa,umejiondoa mwenyewe kama mtumishi wa ufalme.Unakuwa Mtume wa uongo.

Pesa ni tatizo kubwa! Ndyo maana mara nyingi tumeshindwa kutenda mambo mengi kwa kukosa pesa.Hata hivo,kukua kwa kundi hakutokani na Pesa. Vikundi Vyote huanza na imani,maono,kujitolea,na pesa kidogo. Sio pesa zinazotusukuma, lakini ni Imani,upendo,na maono ndyo vinavyotusukuma.Ni Moyo wa Mungu unaowaka ndani ya Moyo wako ambao una msukumo! Wakati kundi linnaposhindwa kuendelea sio kwa sababu ya Kukosa pesa>Makundi mengi yaliyokomaa yana viwanja,utajiri mwingi,majengo, na vifaa lakini hata hivo yanashindwa kuendelea kwa sababu ya ukosefu wa maono,Imani,uaminifu, na kujitolea. Wameacha kuwa makundi na sasa wamekuwa minara yenye utukufu ulioweka!. Munguhaaangalii sana yale uliyo nayo mkononi sasa sawa na kile ulicho nacho moyoni mwako.Pesa zinakuja kutokana na Maono na imani.Mtu mmoja alisema”hawezi kwenda kwa sababu hawana Gari, wakati mwingine kwa wakati huo huo anakwenda kwenye basin a kutumia muda huo kuzungumza na abiria wengine na kumpata mwana wa amani ndani ya basi.Mwingine hana nauli ya kulipa basi, hivo basi anatembea kwa miguu, anapata wakati wa kuomba,anakutana na wengine wanaotembea kwa miguu walio na njaa ya Yesu Kristo.Mipaka yetu inafungua milango ya utendaji wa Mungu.

Ukiwa unangoja pesa zaidi kabla ya kutii,hautatii kamwe na ikiwa unasema kuwa ungetenda mpaka pale ungekuwa na uwezo wa kutosha wa kifedha. Mungu angojea kuona lile ungetenda nay ale uliyo nayo sasa." Ufalme wa Mungu sio kula na kunywa bali ni haki,amani, na furaha katika roho mtakatifu". Kwa kuwa yeye amtumikiaye Kristo katika mambo hayo humpendeza Mungu tena hukubaliwa na wanadamu."(***Warumi 14:17-18).*** Yesu alipotoa amri ya kufanya wanafunzi,alituamuru kutenda jambo ambalo kila mila,taifa na watu watakuwa na uwezo na muda ule ule wa kulitenda.Kufanya watu kuwa wanafunzi inaomba kuutoa muda kwake Yule unayemuongoza ili awe na moyo safi,kumfundisha kumtengemea Yesu anayeishi ndani yao na kuwafundisha kuzidisha muda wakuwekeza ndani ya wengine.Kifaa pekee kinachohitajika ni Muda.Sisi sote tuna kiasi swa cha muda na jinsi tunavyoutumia muda huo huonyesha nini ambacho moyo wetu unathamini !.

Lakini wawezaje kusafiri bila hela? Safari bila hela ni vigumu lakini kufikia kijiji kingine wala inci ni tendo la kutegemea pesa kikamilifu.Ikiwa utamfanya mtu kuwa mwanafunzi barabarani na mtu akifanya hivo kwa mwanamemba wa familia yake na wao wakitenda hivo na mtu wa familia ya karibu na mji wao, na hao wakitenda vivyo hivyo ka haraka tunaweza kuwa na wanafunzi katika inci nzima ! Kifaa ca msingi kinachohitajika ni Muda! Uhusianouliokuzwa utavuka mipaka na vizuizi vyote !

Ikiwa unaongea kwenye mkutano na kundi kubwa ka watu,ni nani mtu muhimu katika chumba hicho? Ni wewe.Wewe ndye mnenaji. Katika mila zetu mtu huyo hujisikia kuheshimiwa,

maana ni wa muhimu n wakati mwingine huwa mtu mwenye kufahamika sana kwa ajli ya huduma yake hiyo !. Yesu alijuwa kuvutia kundi la watu wengi kuliko mtu mwingine yeyote Yule aliyewahi kuishi, lakini tunasoma kuwa akauaga mkutano ***(Mathayo 14:22; 15:39; Marko 6:45; 8:9 ).*** Katika Yohana alisema wazi kuhusu gharama ya kumfwata sawa na wengi wa wanafunzi wake " hawakutembea naye tena" ***( Yohana 6:66 }.*** Yesu alifahamu kuwa kufaulu hakumo katika kundi>Siku moja walitaka kumfanya mfalme na siku ifwatayo walitaka kumuua.Kile wanadamu wanakupa,wanadamu watakichukua tena.

Kinyume chake, Ikiwa unazungumza na mtu mmojoa ndani ya nyumba yake,nani mtu muhimu ndani ya chumba hicho? Ni Yule aliye mbele yako.Wewe ni Mgeni,wewe ni mtumishi - uhusiano kama wanafunzi ni ni kuhusiana na kila mtu kufahamu kwamba Mungu anawapenda kiasi cha kumtuma Mwanae wa kiume ao wa kike kwao . Mungu anampenda sana kila mtu, kiasi cha kwamba ahakutuma ujumbe tu wala kitabu wala kipindi cha TV (Runinga) bali mwanae wa Kike ao wa kiume. Yesu masiaha yake aliyatoa kwa wale kumi na wawili.lengo la ujumbe huo ni kwamba kila mmoja wao ni wa muhimu machoni pa Mungu.Huo ndyo ujumbe tunaouchukua mioyoni mwetu,wakati tunapokwenda kuwekeza ndani ya mmoja ao ndani ya wachache. Huo ndyo mojawapo wa ujumbe wa msingi wa kufanya wanafunzi kwa mtindo wa Yesu – unaostahili mbele za Mungu! Mungu anataka Uhusiano, urafiki Na Wewe. Na njia ya msingi ya kutangaza ujumbe huo ni kuwekeza muda wako katika kushirikiana na watu. Kutenda hivo ni kuwa watu wanaomuiga Yesu.

## MASWALI YANAYOULIZWA

### 1) NIMEKUSIKIA, NI KAMA UNAPINGA MIKUTANO YA WATU NA KWENYE VYOMBO VYA HABARI ?

Ndiyo ! ni kweli! Yesu aliongea uso kwa uso na wanaume kumi na wawili na anatuomba nasi kumfuata yeye. Aliuaga mkutano. Kwa nini tunafikiri kuwa na njia bora? Baadhi ya mikutano mikubwa ya hadharani kihistoria imefanyika Africa ikifikia hadi kiwango cha watu milioni moja wanaompokea Yesu kwenye mkutano mmoja. Nigeria imewahi kuwa na mikutano mingi ya aina hii na sasa ina baadhi ya makanisa makubwa ulimwenguni.

Kusini mwa taifa hilo asili mia Themanini (80%) ya wakaadhi wanadai kuwa ni wakristo lakini hata hivo Nigeria ni miongoni mwa jamii zenye kuharibiwa na rushwa ulimwenguni. Inci ya Rwanda kabla ya mauaji ya halaiki ilidaiwa kuwa na asili mia tisini (90%) ya wakristo lakini hata hivo wakristo waliohudhuria kanisa na kusali pamoja waligeukiana na kuuana kwa upanga kila mmoja na mwingine.

Waafrika wengi wameka sahihi yao kwenye kadi ya kukata shauri kumpokea Yesu lakini ni wachache walioandaliwa kutii yote Yesu aliyotuamuru.

Idadi kubwa ya watu kwenye mikutano ya hadharani humfanya mwinjilisti kujisikia vizuri na kumwezesha kuchangisha kiasi kikubwa cha pesa lakini matokeo yake ni ya kuangamiza. Kwa nini? Hatutendi yale Yesu alituamuru kutenda. Hata hivi mikutano yenye watu wengi, majukwaa makubwa

na viwango vikuu vya pesa vinavyotolewa ndyo ujumbe pekee ambao waafrika walipokea-huduma ni kuhusu cheo, mamlaka , pesa na idadi kubwa ya watu. Cheo, mamlaka,utajiri na idadi kubwa ya watu ndyo vinavyoonekana sana katika kanisa la Africa. Lakini uaminifu na haki havionekani sana.Kwa nini pesa na mamlaka na inaonekana njia yeyote ya kufikia mambo hayo inatetewa kama haki.

Hali hii pia ni kweli na baadhi ya huduma kwenye Televisheni inasikilika vema kusema kwamba inasikilizwa ndani ya nyumba na maelfu kupitia Televisheni lakini kama hilo lingekuwa jema kwa nini Yesu alituomba kufanya wanafunzi na baadae kutuonyesha namna ya kutenda kwa kushirikiana kwake na wale kumi na wawili ? Ukristo si ujumbe tu kuhusu Yesu. Ukristo ni Kristo ndani mwako akitembea na wachache. Yesu ndani mwetu ni hali inapashwa kutupitia sisi hata kufikia ulimwengu. Huduma ya televisheni inaumba wahudumu mastar( Nyota ) na mtindo wa maisha wa aina yao. Huduma ya televisheni hufanya huduma yenye kujaa maonyesho. Yesu alitupa mfano wa huduma ni kama ushirika ambao unazidishwa katika mila. Huduma kwenye Runinga (televisheni) ina sehemu kubwa mbili:

Uwepo wa mtu ,uaminifu wa tabia, ushirika wenye upendo na ukweli ( usiodai pesa )!

## 2) JE? UNATAKA KUWASHIKILIA WATU KATIKA HALI YA UMASKINI?

Hapana ! hata kama Ralph Winter wa kituo ulimwengu kwa ajili ya misioni alivyoripoti kwangu kama ana mahesabu ( siwezi

kupata somo hilo kusudi nimnukulu moja kwa moja ), ambazo zinaonyesha kuwa kadiri pesa nyingi zinavyomwagika toka inje ndivyo matokeo nayo yanavyoendelea kuwa madogo toka kwa misheni ile. Kwa nini hivi? Sio kwamba ni sababu watu wa ulimwengu wa pili na wa tatu ni wabaya kwa kusimamia pesa dhidi ya watu waa magharibi , sababu ya msingi ni kuwa kadiri pesa nyingi zinakuja kutoka inje, Kadiri wale watu wa inje hufikiri kwamba wana haki ya kuchunguza hawa wanaopokea pesa zao kama wanazitumiaje. Wakati watu hao wa inje ( wafadhili ) wanapochunguza maamuzi yao ni ya kuua imani na uwajibikaji na ubunifu ambazo ndizo njia njema kusema kwamba ufadhili wa inje unamzuia Yesu kulijenga kanisa lake kupitia waamini wa kanisa la mahali.

Suluhisho kwa tatizo hili ni "kutoshikilia watu katika umaskini". Jibu ni kuishi kwa imani ndani ya Yesu kama chemchemi ya mambo yote na kuishi imani ndani ya Roho mtakatifu kama Roho wa kujitoa, ubunifu na kuzidishwa. Suluhisho ni kuwatia nguvu na kuwahimiza marafiki kuwa na usimamizi wa mali zao, Suluhisho pia laweza kujumuisha kujifunza kufanya biashara ndogo ndogo wala kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo. Maskini katika ulimwengu wa tatu sio maskini kwa sababu ni wazembe. Sababu kubwa ni rushwa inayo kithiri, inayowanyima kupata haki ya jasho lao. Siku zilizopita tulifadhiliwa na marafiki toka magharibi ambao sisi tulifikiri tuna imani na maono sawa na wao. Hata hivo tulipokuwa na tatizo maneno yao kwangu ilikuwa " kwa nini usiwaambie (lile timu la Asia ya kati ) lile la kutenda? imani yao ilikuwa , kwa sababu ninaisaidia ile timu kipesa basi nina uwezo wa

kuwaambia la kufanya na lile wasingeliweza kufanya chini ya shinikizo la kutopoteza msaada ule."

Jibu langu lilikuwa kwamba siwezi kuwaambia la kufanya maana situmiki na watumwa ao watu duni bali natumika nao kama marafiki. Rafiki yangu huko Asia ya kati alichukua maamuzi ambayo wangeishi kwa ajili yake. Tulikubaliana kwenye maono ambayo ndyo nidhamu yetu. Tukakubaliana kwamba ikiwa mbinu haikubaliani na maono hatutendi. Tulijitolea kila mmja kwa mwingine kama marafiki. Jukumu langu ni kutoa shauri la busara wala la upumbavu lakini mwishowe wanahitaji kuuendea.

Hii ina maanisha nimekubaliana na maamuzi ambayo nilihisi hayakuwa yenye busara. Hata hivo mara nyingi kesi kama hizo ujuzi unaonyesha kuwa rafiki yangu akitenda jambo la busara inamaanisha pia kuwa nilikubaliana na maamuzi yanayodbihitisha kuwa na busara na tumestahimili matokeo yake pamoja. Urafiki na ufadhili ni muhimu sana kuliko kujilinda mwenyewe toka mateso ikiwa gharama ya ulinzi huo ni amri na utawala.

# SURA YA 7:

# KUDHIHIRISHA NA KUTANGAZA UFALME

"***Wqponyeni wagonjwa waliomo, waambieni, ufalme wa Mungu umewakaribia.***" ***(Luka 10:9)***

***"Tazama ni;ewapa amri ya kukanyaga nyoka na ngem nq nguvu zote za Yule adui. Wala hakuna kitu kitakacho wadhuru " (Luka 10:19)***

**A. PONYENI WAGONJWA NA DHIHIRISHENI UFALME WA MUNGU**

Baadhi ya ulimwengu wa kikristo unajengea kwenye maneno, Vitabu, TV, Radio, mahubiri, CD, DVD na kwa namna nyingine tunashikilia hayo tunapowasikilisha habari njema. Tunastahili " ***Kumtakasa Bwana Mungu niongoni mwetu na daima kwetu tayari kutoa utetezi kwa yeyote yule anayeuliza sababu ya tumaini liliomo ndani yako kwa upole na wema" (1 Pet 3:15)***

***Tunaposhwa kujifunza, kuelewa na kuwa tayari kueleza kuhusu Bwana wetu aliyitakasika mioyoni mwetu! hata hivo, Paulo anasema kwa wakorintho (1 Wakorinto 4:20)***

" Maana ufalme wa Mungu hauwi katika neno, bali katika nguvu)" Msemo huu kulingana na mamlaka yake ya kimaadili unashawishi lakini unatuelekeza kwenye shida pana . Hatuwezi kuwahakikishia watu uhakika (uhalisi) wa ufalme kwa maneno peke yake na hata Yesu hataraji sisi kutenda hivo.

Alituamuru kuponya wagonjwa na pia kutangaza ufalme wa Mungu wakati kwanza tumedhihirisha nguvu yake na uwepo. Udhihirisho huo ungepashwa onekana ndani ya nyumba ya

mwana wa amani. Haupashwi kuonekana katika mkutano maalum wa hadharani na mwinjilisti malum wakati ambapo kwaya inaimba na kutengeneza mazingira mazuri. Upako hautegemei mazingira mazuri yanayotengenezwa na wanamuziki wenye ujuzi wanaoimba kwa saa moja. Upako haushuki chini. Ebu fikiria Yesu akikataa kuombea watu hadi Petro atakapoongoza maabudu kwa muda wa saa moja na kutangazia umati wa watu kuwa roho mtakatifu amekuja sasa!.

Upako ni matokeo ya nguvu na uwezo wa roho mtakatifu akaaye na kutulia ndani yako. Tunahitaji kusoma **Luka 4:18-21** mara tena ! Hatumo tena ndani ya Agano la Kale ambapo upako ulikuja na kurudi juu ya watu maalum. Mwili wako ni hekalu la roho mtakatifu.

Upako hauji ili utuondoke tena. Umekuja kukaa. Sisi ni makadhi Ya Mungu, sio mahali pa kutembelea tu. Tatizo la maneno ni kwamba kila mtu aweza kuongea vizuri akilsikilika kuwa kiroho na anaweza hata kunukulu maandiko lakini wanaweza kuwa wanaaongea maneno kutoka vichwani mwao. Unaweza kudanganya kwa maneno na kushawishi umati na hisia, kiingilio chenye uchangamfu. Lakini changamoto ni ya kuomba na mtu mmoja ao wawili walio wagonjwa na waliopagawa mapepo ndani ya chumba, ao mahali pasipo na umati wenye kuchangamshwa, ndipo ambapo huwezi kudanganya.

Hawajamjua Yesu bado. Hawakufahamu na wewe, wanaweza aidha kuponywa ao la. Aidha unamjua Yesu na kuikaliwa na Roho mtakatifu au la.

Hili halitokani na kiasi gani cha maandiko umekariri kichwani, uko kiroho kiasi gani, unaomba kwa sauti kuu na hata kuruka kando ya mtu jikoni haijalishi , watu wanaponywa kwa sababu ya unyenyekevu wetu wa kutegemea Roho mtakatifu akaaye ndani mwetu na imani ndani ya uwezo wake wa kuwapenda na kuwaponya. Mahitaji ya mwanadamu humfanya kuwa uchi ni mbele ya Mungu. Je ? Tunauchukua ufalme wala hapana ? . Twaweza kudhihirisha ufalme wala hapana?. Tunawapenda watu ao hapana ? Je ? Roho mtakatifu yu hakika juu yetu wala hapana? Kuponya wagonjwa pia inamaanisha pia ni kutumikia watu kwa njia ya kawaida. Kuna mithali isemayo ***"watu hawajali sana kile unachoamini hadi watakapoamini ni kiasi gani unawajali".*** Wakati fulani rafiki mmoja alianza kutafuta kile kiitwacho " kituo cha madawa ya kulevya " pamoja na watoto wa barabarani wasiokuwa na makadhi, wavutao sigara. Baadae akawavuta wengi wao, kwa kuwapa zawadi ndogo ndogo hata na kiasi cha pesa ndogo, kwa matumizi yao. Ndyo, walitumia sehemu ya pesa hizo kununua sigara, pombe, madawa ya kulevya, lakini aliwatumikia. Baada ya muda wale watoto wa barabarani wakaanza kumuuliza maswali baadaye”kituo cha madawa ya kulevya” kikageuka na kufahamika kama ”kituo cha mkutano wa maombi”.

Kutumikia kwa njia ya kawaida kuliongoza na kulisababisha uponyaji, kufunguliwa, wokovu na kuzaliwa kwa kanisa kwenye kituo. Ni ushuhuda daima ulimwenguni pote kuwa mahali ambapo makanisa yanaanzishwa kwa njia rahisi, makanisa hayo yanajizidisha (yanakua) haraka kama vile makanisa mapya ya

nyumbani yalivyoanzishwa na matendo ya Roho mtakatifu kwa uponyaji na kufunguliwa. Mara Kwa mara mwana wa Amani ni mtu aliyewahi kuponywa ao kufunguliwa ao mtu ambaye nyumbani kwake mke wake ao wanae waliponywa. Unapomhakishia mtu kuamini maneno yake, huko inje mtu huyo aweza naye kumhakikishia kwa maneno yake mtu mwingine, lakini ikiwa ameuona upendo wa Mungu ukimponya ao kumfugua mtu unayempenda, unafahamu kile ambacho umeona. Baadhi ya wakristo hasa sehemu za magharibi, huzungumza sana kuhusu jinsi gani mila (desturi) za ulimwengu haziamini tena kamwe ukweli kamili wala mamlaka nyingineyo yeyote ile. Wanaeleza kuhusu ni jinsi gani mila (desturi) hizi za kibinadamu zinavyoamini tu kile wanachojua na kukubali kuwa kweli ni kile ambacho marafiki zao wana waambia. Wanaita hiyo ni mawazo ya kisasa mahali ambapo ujuzi ndyo kweli, na hisia ni alama, na thibitisho ni ushuhuda wa kupeana kubadilishana ujuzi na marafiki. Wakristo wengi wanashindwa kushuhudia Yesu kwenye mila hii inayochukulia mambo yote kuwa sawa.

Ni Kweli ,Mila ya ulimwengu huu haiamini kweli kamili ya Mungu wala haitaki kusikiliza mazungumuzo ya kweli toka watu wanaojijulisha wenyewe kama wenye mamlaka. Lakini hakujawahi kuwa kizazi na mila iliyo wazi zaidi kutaka nguvu za Mungu na udhihirisho wa ufalme wa Mungu. hata hivo tuna shikwa! Hawatakuja kwa mikutano yetu kutizama uthibitisho. Wanafikiri kuwa yale tuyatendao ni ujanja na kutafuta pesa na uonapo maongezi juu ya sadaka kwenye mikutano mikubwa ya hadharani na kwenye TV wako sahihi. Yote hayo ni kuhusu pesa. Kwa nini watuamini sisi? Tunahitaji kuwaendea katika hali yao,

miongoni mwa rafiki zao kutenda kazi ya ufalme mahali wanaweza kuona kuwa ni hakika. Hakujakuwepo na Kizazi ambacho ni rahisi kudhihirishia ufalme . lakini hata hivo tunahitaji kuwaendea miongoni mwao, mahali ambapo wanaweza kujifunza kuamini kuwa ni ukweli unaohusu watu,uarafiki, na wala sio tu kuhusu pesa na mamlaka.

## B) KUTANGAZA NA KUUJULISHA UFALME WA MUNGU

Kumekuwepo na baadhi ya makundi kadhaa ya Kitume ya Urejesho (Kufanywa upya) Tangu mwaka wa 1970 na Jambo moja la jumla wanalokazia wote ni kurejesha mamlaka ya zile huduma tano, wakilenga sana ile huduma ya Mtume kama ndyo yenye mamlaka juu ya Kanisa. Misemo kama " Kurudi kwenye mpango", "Kutambua utaratibu wa Mungu", Kunyenyekea mamlaka ya Ufalme", " Kurejesha utaratibu", "Ulinzi wa Kiroho", "Kuheshimu mamlaka", "Kumtambua Mtu wa Mungu", na " Baba wa Kiroho", hayo yote yamekuwa maneno ya kawaida ya makundi hayo.Picha ya kiakili na ya kiroho inayoongoza hapa ni ule mnara wa utaratibu sawa na wa kisiasa, mashirika ya kibishiara,na ufalme wa Giza mahali ambapo unyenyekevu, heshima na utajiri vinafurika kuelekea juu, huku amri na utawala vinalekea chini. Mamlaka, nguvu, umaarufu na utajiri wa mtu anayeongoza, unatokana na idadi ya watu kwenye ngazi mbali mbali zilizo chini ya utawala wake.

Makundi yote haya ya kitume, yanaaidi uhuru katika roho na yanajulikana kwa mtindo wa kisasa wa kuabudu, kucheza, kupeperusha bendera, kutabiri huku wakiimba, na kupiga kelele nyingi***…".Walakini alipo Roho wa Bwana hapo ndipo penye***

***uhuru..." ( 2wakorintho 3:17 }.*** Mema Yote isipokuwa uhuru apo kati ya kuta nne na hilo hutokana na Jinsi gani watautikisa mwili wako wakati wa ibada. Aina ya uongozi ni wenye mamlaka makubwa na ukienda kinyume na kile kinachofahamika kama maisha ya kunyenyekea kwa njia yeyote ile uta hesabiwa kuwa asiyefaa na uongozi. Ukiwa Mume una roho ya uasi kama Absalomu n kama wewe ni mwanamke wewe ni Yezebeli.

Mpangilio wa madaraka, waweza kuwa njia ya mashirika makubwa kama serikali, mashirika makuba ya kidini,KGB,mafia wala falme za giza, waweza kutenda kwa maana kwenye mpangilio wao mtu mmoja awezaketi mahali pamoja na kuamuru huku akingoja kuletewa ripoti. Hata hivo kuna kazi nyingi zinazotendeka hata katika ulimwengu wa Biashara zikisimamia kwenye aina hii ya uongozi ([6]). Mwili wa Yesu kristo una uongozi usiokuwa na mipaka.Yeye ni mahali pote na wakati wote. Yuko mahali pote kwa wakati wote.Anaona yote na anafahamu yote.hana haja ya kupewa ripoti kutoka kwa yeyote Yule. Na wala haitaji kumpea mtu yeyote yule madaraka. Hakutupa madaraka ya kutawala wengine. Ndyo ! ***" Juu ya mamlaka yote ya adui". (Luka 10:19)***. Lakini hakuna mahali pengine amempa Mume wala Mke mamlaka juu ya mwingine. Amekataa kutumia aina hiyo ya mamlaka, ***" na wala isiwe hivo miongoni mwenu..."*** , ***"Lakini Yesu akawaita akasema mwajua wakuu wa mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. Lakini haitakuwa hivo kwenu bali mtu yeyote atakaye kuwa mkubwa kwnu na awe mtumishi wenu.Na mtu yeyote***

[6] "The seven day weekwnd " by Ricardo Semler " the starfish and the spider " by Ori Brafonan & Rod Beckstrom

***anyetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu kama vile mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika , kutoa nafsi yake iwe fidia kwa wengi…" (Mathayo 20:25-28).***

Unaweza kuswali Je? Mtume sio ndyo karama kubwa miongoni mwa zile huduma?. Ni Swala la Mtazamo usiojenga juu ya Agano Jipya.Ulimwengu wa wakati ule, kiasi cha 1/3 ya wakadhi walikuwa ni watumwa. Sio sawa na utumwa ule uliowahi kuwa huko marekani,wala sawa na ule ulioko sasa hivi kaskazini mwa Afrika ambako Waarabu wa dini ya kiislamu wananunua watunmwa waafrika weusi.Kulingana na sheria za utawala wa warumi,watumwa walistahili kutendewa vema, baadae kuachiwa huru baada ya muda Fulani wa Kazi.Wangeweza kuwa wasomi, wengine waligeuka kuwa wana familia katika nyumba ile kama wana waamini.Kwa hiyo walisimamia shughuli za Bwana zao, na Bwana Zao na wao walisomesha watoto wao na wangeweza hata kununua uhuru wao kwa mshahara wao. Watumwa waliokombolewa walirejea tena katika hali ya utumwa, kwa sababu walikuwa na maisha bora katika hali ya utumwa tofauti vile wanapo kuwa huru.

Neno "Mtume" lina maanisha" aliyetumwa" lakini tumepoteza maana halisi ya neno hili. Mtumwa wa chini sana aliitwa "Mtume". Kwa nini? Usafiri wa wakati ule ulikuwa mgumu na wa hatari.Ukiwa kwenye safari za kidiplomasia wala ukiwa unachukua utajiri mwingi, ilibidi usindikizwe na kundi la askari jeshi kukulinda na wezi. Kama una kitu cha thamani ndogo, unasafiri ukiwa peke yako.Bwana wa mtumwa alimtuma

mtumwa aliye mdogo kupeleka bidhaa yake, pasipokuwa na ulinzi. “Mtume” huyu angeweza kunyang’anywa kila kitu,kutekwa, wala kuuzwa tena kama mtumwa. Kama wewe ni mtu wa thamani ndogo mbele ya Bwana wako,Basi wewe ni Mtume. ***Warumi 1:1*** inatofautisha kidogo ukweli huu!!! ***“ Paulo, Mtumwa wa Yesu Yesu kristo,aliyeitwa kuwa mtume, na kutengwa aihubiri injli ya Mungu…”***

Kwenye mila ya wakati huo, watu walielewa kuwa Paulo alijihesabu kama mtumwa aliye mdogo.lakini hilo linahusiana vipi na ufalme wa Mungu?. Katika Yote hayo! Injili ya ufalme ni ile isemayo kuwa Yesu ni mfalme, Bwana wako, Kichwa chako,utukufu wako, na anaishi ndani yako tumaini la utukufu wako.

Habari njema sio kuambiwa kwamba ili uwe ndani ya ufalme wa Mungu unapashwa kuninyenyekea Mimi!. Unapoambiwa kuwa kila mtu ni kiongozi wako wa kiroho wala ni Yeye ndyo kinga yako hilo ni kinyume na ***1Thimoteo 2:15 “ Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, mwanadamu Kristo Yesu…”.*** Inashangaza kuona kwamba tuko wazi sana juu ya wokovu wetu binafsi, upatikanao kupitia Yesu na kwamba Yesu ndyo kiongozi wetu inafsi.Tunakataa mapokezi ya Kikatoliki na yale ya Ki-othodoxi juu ya kuhani kuwa na uwezo wa kusamehe dhambi, na kukariri ***1Thimoteo 2:15*** ni kutenda hivo, lakini inapofika kutenda sawa na maisha ya ufalme wa Mungu tunayaubiri mapokezi yale yale sawa na wakatoliki na wa othodoxi kuhusu kunyenyekea uongozi wa mwanadamu. Tumeambiwa twaweza kutenda katika ufalme,

ikiwa tutamnyenyekea Mwanadamu aliye kichwa. Tumeambiwa kuwa uhusiano wetu na Yesu unasaidiwa na mpatanishi mwingine dhidi ya Yesu. Wakati hili linatokea Yesu nakuwa kichwa kisichotawala.Hata hivo, Yesu daima na daima atabaki kuwa kweli, kiongozi wa mwili wake,Mafundisho yetu juu ya ubwana wetu kuhusiana na kumnyenyekea mwanadamu kama kichwa ni Shizoprenic. Ni ishara kuwa waamini wamechanganikiwa na wasiozaa matunda?

Ni Jambo la kushangaza kwamba " shida" ya uongozi wa kanisa wanayokuwa nayo na waamini wapya ni kwamba wanakuwa waasi, wasiojali wakati ambapo " wangejifunza kunyenyekea mamlaka." Tatizo la waamini wapya ni kwamba mwamini mpya huyu anapambana na mfalme wao na sauti ya mfalme inasikilika mioyoni mwao roho ya mfalme inatembea katika maisha yao, na wana shauku ya kutembea pamoja na mfalme wao mpya ambaye ameshawajaza makusudi yake na upendo kwa ajili ya watu. Kanisa ( kundi ) linalokuwa kando kando yao lina kuwa lisilokuwa na imani na lisilotii mila ya dini inayojijali yenyewe na iliyo na uhusiaono mdogo na ulimwengu unaowazunguka na wala haienendi popote ! Ndani ya baadhi ya makanisa ( waamini wanaomba na kuimba ) vile walivyo leo ndivyo walivyokuwa miaka ishirini iliyopita. Lakini wakati wote huo walitangaza uamsho waliomba ili jengo lijae na walihubiri hata kuwa mambo yote hayo yatatokea hivi karibuni wanauwa uzima wa Yesu ndani ya maisha ya mwamini mpya na baadae wanandaa mikutano ya uamsho ili kujaribu kurejesha uzima waliofukuza. Inachukua nguvu (bidii) nyingi za kisaikolojia, kushawishi watu kihisia,na

mashurti kumfanya mwamini huyu mpya akubaliana na dini yetu na akuli kama kawaida kukosa utiifu sawa na wengine.

Maandiko yanatafsiriwa vibaya ilI kumhakikishia mwamini huyu mpya hawa wasiotii na waliopoa kiroho lakini watu wazuri hao ndyo wazee wao ndani ya Imani! Hii ni hali ya kuwafanya watu kuwa watu wa Dini ! Kuliko kuwa wanafunzi wa Yesu. Ni Mbinu ya kumfanya mtu awe sana mwaminifu kwa shirika badala ya kuwa Mwaminifu kwa Yesu.

Uaminifu huo kwa uongozi na kwa shirika unafanana na ule unaodaiwa na watu wa mafia,unakuwa mwaminifu hata kama unafahamu kuwa walio juu yako wanatenda vibaya. Unabaki mwaminifu hata kama maswala ya haki hayazingatiwi>Wakati maswala ya umainifu yannainuliwa zaidi kuliko maswala ya kweli hampo tena katika ufalme wa Mungu>Mmekuwa tu ndani ya shirika la wauaji na wakati mwingine viongozi wa Dini hutenda sawa na wauwaji unapokabiliana nao kuhusiana na maswala juu ya kweli !.

Mambo yote hayo hulinganaje na Luka 10 ?. Tunapashwa kutangaza ufalme wa Mungu unakaribia baada ya sisi kuthibitisha ufalme kwa kuponya wagonjwa. Msukumo ni nini hapa? Nini hutendeka wakati mgonjwa anaponywa,mvulana.mume,mke,msichana,?Watakuthamini sana. Unaweza tumia nafasi hiyo kuwa mfalme. Lakini Jibu lako litakuwa nini ? Jibu lako ni kutangaza kuwa ufalme wa Mungu umekaribia. Ndivyo Paulo na Barnaba walivyotenda katika

**Matendo 14:8-18 *“ Na huko Listra palikuwa na mtu mmoja dhaifu wa miguu,kiwete tangu tumboni mwa mamaye,ambaye hajaenda kabisa. Mtu huyo alimsikia Paulo na Barnaba* alipokuwa akinena…..”*Sisi nasi tu wanadamu hali moja na ninyi…”*** .Hii ina maanisha nini? Ina maanisha kuwa mwenyeji wako naye pia anaweza kuingia katika ufalme,akiamua kutenda hivo na kuwa na mamlaka juu ya magonjwa na mapepo sawa na wewe.Wewe ni “Mtume” tu anayedhihirisha ufalme ili mwenyeji wako atizame na aingie ndani ya ufalme huo hata amjue Yesu mwenyewe Binafsi. ! Tunatangaza ufalme kwa kuonyesha mamlaka ya ufalme juu ya ufalme wa Giza na tunajulisha ufalme kwa kuwa watumishi wa wote. Hatujawa kamwe wapatanishi kati ya Mungu na wanadamu.Hatujawa kamwe wapatanishi kati ya Mungu na mwanadamu.Hatujawa viongozi wa kiroho juu ya yeyote Yule. Ni swala nyeti kwa wale wanaotoka kwenye mila ya kiislamu.Wamoja wao wana shauku ya kutafuta kweli na tayari kufa juu ya kweli ambayo wameifahamu.Uislamu maana yake halisi ni Kumnyenyekea Mungu. Kwa hiyo katika kusikia hayo,ili kuingia katika ufalme wa Mungu anapashwa kunyenyekea mila ya Dini Fulani ya kigeni,wala mamlaka,wala kuingia ndani ya jengo Fulani la kigeni!. Kwake Yeye mambo hayo yote hayaeleweki na yanamuumiza maana unyenyekevu wa aina hii upo kinyume.

Tunapashwa kutangaza ufalme wa Mungu ndani ya nyumba yake katika mila yake.Kamwe sisi sio wafalme,bali watumishi daima,na kazi yetu ni kudhihirisha ufalme wa Mungu,kiasi cha kwamba waweze kwa uhuru wote kuingia ndani yake kupitia

Yesu na kuishi ndani yake kwa kumneynyekea Yesu peke Yake,Ni Kweli kuwa ,hii inawezekana kwa kila aina ya mila na watu.

### *C)* NANI MHUSIKA?

Swali la kwanza katika kila shirika la kibinadamu na katika kila Kanisa ni " Nani kiongozi..!". Njia ya matayarisho inayojitokeza akilini mwetu ni ile ya kuwa na wasimamizi. Shirika nalo litategemea mpangilio wa madaraka.Vikundi vipya vya kitume vilijaribu kuzuia ugomvi juu ya mwelekeo, maono na mgao wa mali ndani ya kanisa la mahali kwa kuheshimisha mamlaka ya wote.walisema kuwa ilikuwa ni "kufanya upya" yale yaliyokuwa ndani ya Kanisa la kwanza lakini kwa hakika, ni mbinu ya Kale ya Papa!

Mchukue Papa, Kardinali, Askofu,na Kasisi (Padri) wachukulie kama mtume,nabii,mchungaji,mzee. Hilo linaumba wapapa wengi wadogo, watumwa wengi,matatizo mengi na yote hayo hayalingani kabisa na kanisa la kwanza. Minara inafanywa kwa ajili ya watu. Na Mnara hujengwa na watumwa ! Kwa nini basi bado kuna watu wengi wanaotengeneza tofali kwa ajili ya Farao?

Lakini **Luka 10** inatupatia picha nyingine. Nini ilikuwa ndani ya kanisa la kwanza?Ukienda ndani ya nyumba nyingine,umekuwa mwalikwa,daima mtumishi,wewe sio mhusika.Hutawaambia namna ya kupanga vitu vya nyumbani mwao,kuweka taratibu wala kudai vyakula upendavyo. Kazi yako katika kudhihirisha ufalme, ni kumfanya mwenyeji wako kuwa mwanafunzi ili baade aweze kuwa mchungaji/Mzee/(maneno hayo yote yanatumikwa

kwa namna mbali mbali katika Agano Jipya – Tazama **Matendo 20:17-28).** Kwa familia zao na wa marafiki zao. Mamlaka ya asili, mvuto,ni dhihirisho la ufalme wa Mungu hapa Duniani kwa njia ya familia.

Kwa bahati mbaya mipango ya makanisa mengi yamechangia kuharibu mamlaka ya nyumba na familia. Matokeo yake baadhi ya watoto wanaolelewa katika nyumba za waamini wanaiacha imani wanapokuwa watu wazima.

Unapotangaza ufalme unatangaza pia kuwa mwanafunzi wa huyo mpya ni mwanamemba wa taifa teule, ukuhani wa kifalme,taifa takatifu **( 1 Petro 2;1-10 ).**Mwana wala Binti wa wa Baba wa Mbinguni **( 1 Yohana 3:1-3 ),** ana haki ya kufika mahali patakatifu pa patakatifu kupitia damu ya Yesu Kristo **(Waebrania 10 : 19-25; 12:22-24 ),** ana Roho Mtakatifu akaaye ndani mwake ili kutuongoza ktika kweli yote. **( Yohana 16: 13-14 )** na **( Yohana 2: 24-27).** Ana Roho mpya sasa ambayo Mungu ameandika sheria zake zote **( 2wakorinto 3:3),** ana Yesu kama utukufu na mtawala **(wakolosai 1:18)** na ana yote katika kristo **( waefeso 1:3 )** Na **( Wakorintho 3: 21-23 ).**

Ni Jinsi Gani uongozi wa mwanadamu unahusiana na hayo? Kazi kubwa ni ya kiongozi ni kudhihirisha ufalme kwa kuonyesha kuwa unajiamini na na una uhakika kwamba walio ndani ya Yesu Mungu atawaongoza.Shabaha wala kusudi la uongozi wa Mwanadamu ni kuwafanya watu

wafunguliwe na waupende uungu wa Kristo katika mambo yote.

***" Si kwamba tunatawala imani yenu; bali tu wasaidizi wa furaha yenu; maana kwa imani yenu mnasimama..."***

***( 2 Wakorintho 1:24 ).***

Katika sura hizi mbili za barua ya Paulo kwa wakoritho, Paulo anashauri na kushawishi wakorintho kutatua matatizo yao na kumuonya kila aitwaye ndugu aliye katika dhambi.Hakuwaandikia wazee na kuwaamuru kutenda hivo wala uongozi wowote. Aliliandikia kanisa lote na analisihi kanisa lote kutenda kulingana na yale wanayoelewa kuwa ni haki. Kwa sababu anawapenda na daima aliwatumikia kwa charama yake mwenyewe.

Uongozi katika ufalme wa Mungu ni kuongoza kwa kuwa kielelezo na kutoushauri. Ushauri hutolewa kwa wenye hekima na kwa wajinga na kuacha maamuzi ya mwisho kwa Yule aliyeshauriwa, ni jambo la kuwaacha watoto wa mungu kwenye ya majukumu yao mbele uya Mungu kwenye ya majukumu nyao mbele ya Mungu na kumwachia Yesu kujenga kanisa lake. Uongozi ndani ya makanisa mengi ya siku hizi unajihusisha na kutoa ruhusa. Ni wao wanapashwa kuhalalisha kwa kusema ndio wala hapana. Watakuambia yale upasayo kutenda wala yale usiyopashwa kutenda. Kila kitu kinatokana na taratibu, uchunguzi unaozaa watoto walemavu kiroho wasiojua jinsi ya kushirikiana na Mungu.

Inakubalika kwa jumla kuwa ndani ya kila shirika kubwa usimamizi na uchunguzi ni muhimu. Lakini kanisa la Yesu limekuwa kama shirika kubwa? Tukimtii Yesu na kufanya wanafunzi katika nyumba na tukizidisha hayo, ndipo kila kanisa litabaki ndogo lakini kila mwanamemba atakuwa akitenda kazi hiyo kulinga na kutii sauti ya mwalimu. Yesu alianzisha kanisa la watu kumi na wawili. Na kanisa la Yesu kristo lengekuwa ni mwili wake vuungo hivyo vidogo vilikuwa san ndani utawala (ufalme) wa kirumi kiasi cha kwamba asili mia kumi (10%) ya watu katika ufalme huo wakawa wanafunzi wa Yesu. Walitenda hayo bila usimamizi wa uongozi wowote wala bila mpango kutoka ofisi kuu yeyote ile inayoamuru mambo. Kila mwamini alikuwa na ile mbegu ya kuzaa wengine (AND) moyoni mwake. Kila mwamini alimchukua kiongozi moyoni mwake. Kila mwamini alizaa sawa sawa na ile mbegu (AND) ya mwalimu. Mambo yanakwenda vibaya wakati uongozi wa mwanadamu unajiweka katika ya kuwa kama kichwa cha wana memba wa mwili mambo haiendeki . lakini mambo hunedeka wakati mwili una kuwa kama muungano.

Tumeona kanisa kama tunavyolifahamu kwa muda mrefu kuasi cha kutofikiria ni aina gani ya kanisa Yesu angelitamani liwe. Tumeshurutishwa kukubali, kuhitaji uongozi wa mwanadmu na kuuamini kiasi cha kutofikiria, kuwa Yesu anaweza kuongoza mwili wake.

Tumezoea kuona haja ya uongozi wa mwanadamu kiasi cha kwamba kuonyesha imani yako ndani ya Yesu aliye kichwa cha utendaji wa mwili inaonekana kuwa uasi nini

linaloonyesha vizuri hali ya kanisa sawa vile yesu anavyo-lioona katika **Luka 10?** Mti ulio mzabibu? Tembo ao sungura? Ndiyo Mungu aliumba yote mawili, lakini ni lipi linaloonyesha tabia ya kanisa lenye utufu sawa na **Luka 1o?** Jibu liko wazi! Mzabibu na sungura. Mungu ashukuriwe kwa ajili ya tembo na mzabibu lakini kwa nini wanadamu wanaendelea kujenga miti na tembo? Waweza kuunda ufalme (utawala) ndani ya mti ao juu ya tembo na watu wote waweza kuona utawala wako na kuona ni aina gani ya huduma kubwa uliyo nayo. Lakini waweza kuonekana mpumbavu kuketi juu ya mzabibu ao kujaribu kutembelea sungura. Ukipanda mzabibu ndani ya shamba utatoa matawi ya mizabibu mingine na kila mzabibu utatafuta maji yake mwenyewe utaotesha majani yake na utaogelea ndani ya upendo wa mwana na baadae shamba lote litafunikwa na mizabibu. Utaunganishwa na uhusiano lakini hawatategemeana mmja na mwingine! Hautaweza kueleza ni mzabibu upi uliokuwa wa kwanza! Ukiacha sungura wawili peke yao kwa muda wa miaka miwili, utakuwa na kiasi cha angalau sungura milioni moja. Baada ya miaka miwili tembo watazaa tembo moja zaidi na watahitaji mambo menngi kwa kutenda hivo.

“tatizo” la vyama visivyokuwa na kiongozi ni kwamba ni vigumu kuwatumia ili kujitajirisha. Uongozi unaunda jamaa za utajiri.

Rafiki yangu mpya anasomea stashahada (Degree) katika seminari ya mahali. Baadhi ya waalimu na wanafunzi wanaosomea degree hujadiliana. Juu ya kanisa la

mwanzoni, la kawaida, na wengi wameanza kuamini kuwa ndyo mfano wa Biblia (kanisa lenye uongozi. Usiokuwa na kiongozi mmoja). Lakini hata hiwo wamekuwa na tatizo kubwa kabisa. Wamesoma miaka mingi ili baadae waje watumike kwenye huduma mbalimbali za kanisa. Wakikubaliana na utendaji wakanisa sawa vile yesu alivyo tuamuru, kuwafanya wanafunzi, na wala sio kujenga mashirika, watalazimika sasa, kutafuta njia nyingine ya kuishi ili kutosheleza mahitaji yao na ya familia zao. Hawakuwa viongozi tena nani kiongozi? Yesu !

## A) MTUMISHI DAIMA NA WALA SI MFALME,TUSEMEJE KUHUSU WAZEE ?

Tukipekua **Luka 10** hadi mwisho wa agano jipya waweza kuona maneno 15 yanayoeeleza juu ya kanisa ndani ya nyumba (tazama appendice) hizi ni nyumba ambamo mwana wa amani alilelewa hata kuwa mlinzi/mchungaji/askofu/mzaliwa wa kwanza wa familia yake na marafiki zake.

Ndyo, lakini tuseme, nini kuhusu kuwaombea wazee ? hilo haliusishi uongozi ? hilo litahusiana je na maono haya ya mipango ? kwanza kabisa tuachane na neno « kuombea », (kusimika), kama linavyotumiwa na mashirika ya kidini,Neno hilo linahusisishwa na kukabidhiwa cheo na mamlaka na « mtu mwingine aliye na cheo kuliko wewe katika muungano wenu. Badala yake machakato ambao Paulo anaeleza ndani ya **1 thimoteo 3** na **tito 1** ni

kutambua neema ya Mungu juu ya mtu inayotambulikana kwa tunda lilikomaa. Tukazie pia uhalisi wa mila ya mashariki , heshima ya wale walio wazaee kwa miaka, ujuzi wa maisha na muda waliopitisha katika kazi Mungu. Sio kuinuliwa kwa mtindo wa mashariki kunakotokana na karama, vipawa ao utu. Ni heshima ya mashariki kwa wale wanaostahili kuwa wazee kulingana na ujuzi wao wa maisha. Paulo alipita krete akasimika makanisa mengi ya ndani ya nyumba. Sasa katika **Tito 1,** anamuomba **Tito** kurudi tena krete ili awatambue wazee. Na anampa amri ya kutizama tabia na utu kuliko kuzingatia karama. Kulingana na **Luka 10,** aliamriwa kusimika mzee kwa kila nyumba atakayetambuliwa kuhudumu nje ya nyumba zao, mwenye uwezo wa kutoa shauri katika mikutano mingine ya kanisa ya mji.

Viongozi wamoja wa familia hawa kuwa na mwenendo mzuri maishani mwao, mwenendo muhimu kuwatambua kama wazee, wale waliokuwa na tabia hizo walitajwa kama wazee wa kanisa la krete. Ninini kilichobadilika ndani ya nyumba yam zee huyu mpya? Hakuna, ni nini kilibadilika ndani ya nyumba ya yule ambaye hakutambuliwa kama mzee? Hakuna, ingawaje mzee angetambuliwa kama mtu ambaye angesaidia makanisa mengine ya nyumbani ndani ya jimbo lao. Tutizame kazi ya Paulo kwa wazee wa efeso. Mchakato ni ule ule wa kuanzisha makanisa, kuchunguza na kutambua na wakati Paulo alipowakusanya wazee wakati wa safari yake ya mwisho kuelekea Yerusalemu, aliwaongya katika **Matendo 20:29-30**, "***Najua mimi ya kuwa baada***

***ya kuondoka kwangu mbwa mwitu wakali watingia kwenu,wasilihurumie kundi,tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao".*** Anaona hatari za aina mbili. Ya kwanza ni mbwa mwitu watakao toka inje. Amezungumzia hili pia katika **2wakorintho 11** aliposimama juu ya mitume wa uongo wanaotafuta tu uwezo na pesa. Alizungumza kuhuusu hatari hii ya inje tena katika **Tito 1:10-11** ***"ambao yawapasa wazibwe vinywa vyao hao wanapindua watu wa nyumba nzima. Wakifundisha yasiyowapasa kwa ajili ya mapato ya aibu***". Hatari ya pili ilikuwa ni ya ndani hatari ya ndani ilihusiana na baadhi ya wazee watakaojivutia wanafunzi. wanasukumwa na nini hapa?

Mzee ni mtu aliyetambulika ndani ya kanisa lililo nyumbani mwake na inje ndani ya mji kama mzee wa kanisa katika mji. Jukumu la kwanza la watumishi hawa lilikuwa ni kulinda afya ya makanisa za nyumbani kwa kujulisha na kutangaza ufalme pili kuwa tayari kutoa huduma ya uponyaji kwa kuweka mikono, tatu kutumika kwa ushirika na makundi mengine ya mahali, ambayo ni makanisa ndani ya mji ao ndani ya jimbo, nne kuwasaidia kuanzisha makanisa mapya ya nyumbani ndani ya jimbo. Tano kurahisisha utendaji wa huduma inje ya mji wao kama alivyofanya Paulo alipokusanya msaada wa watu wa makedonia na wakorintho kwa makanisa ya uyaudi yaliyokabiliwa na njaa.

Kuliko kutimiza kazi zile tano za huduma wazee Fulani walitumia karama zao kutoa rushwa kwa ufalme na kujivutia wanafunzi wengi wa makanisa ya nyumbani kwao. Huku wakiendelea kutumikia nyumba zao na kuendeleza agizo **la Luka 10,** walibaki watumishi, walio na shauku na nia ya kusaidia makanisa mapya kuwa wanafunzi wa Yesu . Wazee wakiwavuta wanafunzi kwao, waweza kuwa wafalme. Waweza tumia karama zao, upako wao, nguvu na utu wao kuchukua nafasi ya Yesu juu ya kanisa lake. Waweza kujenga msingi imara unaoruhusu cheo, mamlaka, utajiri na kupuuzia mchakato wa kuzaa. Paulo anasema wale wasioenenda kama watumishi na wanaojivutia watu kwao wanatende hivyo kwa kunena mambo potofu".

Lakini kwenye ukristo wa kisasa wale wanaojivutia idadi kubwa ya watu ndyo wanaonekana kufaulu. Wanafanya mikutano kufundisha viongozi wengine namna ya kuiga ufanisi huo. Kulingana na Paulo wanafundisha wengine namna ya kusema "mambo potofu.

Kwa hiyo, wazee walitambuliwa, hata hivyo hawakutenda huduma yao kwa kuambia wengine lile wangelitenda na lile wasigelitenda. Hawakukataa wala kutoa vibali vya kuruhusu. Walitumikia watu na walikuwa vyelelezo katika mwenendo na uhusiano wao na wengine. Kuchukua uamuzi wa namna wengine wangetumika haikuwa kazi yao. Kupeana ruhusu sio kazi ya wazee ndani ya agano jipya. Wazee wa agano jipya ni viongozi ndani ya makanisa za nyumbani, wanaotambulika kuwa na uwezo wa kutumika. Wakianza kujivitia watu kwao, wanakiuka huduma yao.

Wakiwa wanaotoa vibali vya kukataa wala vya kuruhusu wanachukua nafasi ya Yesu, kichwa cha mwili.

Je wewe ni mzee? Unawapenda watu ? kama ndiyo uwape uhuru ule ule unaohitaji wewe ndani ya Yesu ndiyo utakuwa mfano wa unyenyekevu, utaeleza kweli, utatoa na utakapokea heima.

**E ) YESU NI KICHWA HALISI WALA SIO MTU WA KAWAIDA**

Mara tena, tunataka kudhihirisha ufalme kwa namna ya kumheshimu mfalme ni jinsi gani kanisa la ndani ya nyumba linaendeshwa? , ni jinsi gani kundi la makuhani waaminifu linaendeshwa ? ni jinsi gani washirika wa mwili wa kristo huonyesha heshima yao na ibada yao kwa Mungu aliye ndani ya kila mmoja wao ? Mfano wa mwili wa kristo ndani ya agano jipya unajumusiha mwili, kupitia kwa hekalu hadi kwa familia na kwa jeshi. Mfano wa umati haujawahi kutumiwa kamwe ! Mwili haujumuishwi na watizamaji tu wanaolipa kuwatizama tu viongozi wao wakitenda huduma. Hatugawanywi kama washirika na makuhani. Wamoja watazamaji ao wengine watendaji ikiwa twaamini kuwa Roho mtakatifu anakaa ndani ya kila mwamini, basi kuna haja ya kuona anatenda kazi ndani ya kila mshirika (mwamini). Kuna karibu vifungo (40) arobaini vinayo tuonyesha uhusiano unaopashwa kuwa katikati yetu sawa «pendaneni nyinyi kwa nyinyi » « chukulianeni

mizigo ninyi kwa nyinyi » « semeni ukweli kila mmoja na mwingine » nyenyekeaneni yaani kila mmoja na mwingine katika woga wa Mungu » , (kwa maelezo kamili kuhusu somo hili tazama appendice 3 ), tukiongeza aya zinaeleza,kuhusu kumupenda jirani ao ndugu, idadi ya vifungu kuhusu upendo vitakuwa zaidi ya sabini na pamoja na ile amri ya utampenda jirani yako kama unayvojipenda mwenye ».

Kuna vifungu kama sita tu vinayvotunza juu ya namna tunapaswa kuheshimu walio juu, yetu katika Bwana, ni kwenye vifungu 6 vya maandiKo makanisa, na dini wanasimamia wakiweka mkazo ? sawa ! kuna vifungu vichache vinavyohusu kunyenyekea viongozi. Ni makosa kukazia vifungu hiyvo, vifungu hivyo vinatumiwa kueleza kiongozi huku baadhi ya maandiko matakatifu hueleza juu ya mwili wa makuhani watakatifu walio chini ya kuhani mkuu . Hilo linapuuzwa. Huko mangaribi mwa marekani, baadhi ya vifungu vya maandiko matakatifu vilitumiwa vibaya kwa kukazia utumwa. Africa kusini walitumia vifungu ili kukazia ubaguzi wa rangi, lakini vifungu vya maandiko matakatifu vingi vinavyoeleza juu ya usawa na upendo Kati ya ndungu havielezwi. Maandiko yote pia yanapoeleza kuwaheshimu wazee Yana ukweli kuhusu mmoja kwa mwingine” kwa hiyo maelezo yote yanayotolewa ndani ya **waefeso 5** yanatanguliwa na neon”hali mkinyenyekeana katika kicho cha kristo**”(waefeso 5:21)** maelezo ya Petro katika **1 Petro 5 :5** ***”vivyo hivyo ninyi vijana,watiini wazee, nani ninyi nyote jifunzeni***

***,unyenyekevu, mpate kuhudumiana kwa sababu mungu huwanpinge wanye kiburi, kakini huwapa wanyenyekevu neema."*** Ni kweli kwamba kuna viongozi, ndiyo yote hutoka Na kurejea kwa viongozi.lakini kama asemavyo Petro katika **1 Petro 5:3** tusiongoze kama wanaowatawala , lakini kama vielezo kwa lile kundi"tuongoze kama walio wa kwanza kuteswa , wa kwanza kuyatoa maisha yako , wa kwanza kusamehe, na wa kwanza kusema "nimekosea, Je? Mnaweza kunesamehe?. Tunaongoza zaidi sana kwa kuwa kilelezo na kuvutia kiongozi anayedai anyenyekewe amepoteza malaka yake. Je? Mnapenda mabwana na watumwa ao ndugu na marafiki? Utumwa wala kutumikia sio tabia ya dini . Ndiyo, sisi ni watoto wa mfalme, ndiyo,tumewekwa pamoja na kristo mahali pa juu. Lakini tunapashwa kufuata maelekezo katika **wafilipi 2:5**"***iweni na nia hiyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya kristo Yesu ambaye yeye mwanzo alikuwa yu namna ya Mungu , naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho,bali alijifanya kuwa hana utukufu akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu! . Tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu ,alijinyenyekeza akawa mtu hata mauti, nam, mauti ya msalaba ...." Iweni na nia ile ile iliyokuwa ndani ya kristo yesu !*** kwa jinsi hiyo, kama kweli Yesu ni kichwa cha mwili wake na wala sio tu Bwana wa watu binafsi, mojawapo wa nidhamu (tabia) muhimu ya mwili ni kuweka kando matakwa yetu na kuelewana sisi

kwa sisi. Ndiyo ujumbe muhimu mojawapo wa **1 wakorintho 11 :21-34.** " ***Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu na watu kadha wa kadha wamelala "*** . Hii ndiyo ilikuwa nia yao juu ya mwili wa kristo inayodhihirika katika tabia yao ya kula pamoja. Tunaumega mkate kuonyesha kuwa tu mwili mmoja. Tunakinywea kikombe kuonyesha kuwa tunachangia uzima. Tunatangaza kifo chake hadi atakaporudi tena. Tunatangaza kifo kilichotufanya kuwa mmoja. Tunapokusanyika kula tunapashwa kuongojeana. Tatizo lilikuwa nini korintho ? chakula cha Bwana kilikuwa chakula kamili hakikuwa mfano hapana.

Matajiri walileta chakula kingi pamoja na kinywaji,na walikula na kushiba na walikunywa hata kulewa, lakini maskini walirudi wakiwa na njaa matajiri waliaibisha maskini hawa kupambanua mwili wa Bwana. Maskini na wao ni sehemu ya mwili wa Bwana sawa na matajiri. Kwa kuaibisha maskini, hawakumheshimu Yesu na wale wote amabao aliwafia. Suluhisho? ***" Kwa hiyo, ndugu zaugu, mkutakanipo mpate kuta, mgonjeaneni***". ***(1wakorintho 11:33)***, Mna njaa sana kiasi cha kwamba hamwezi kungojeana wakati wa kula? Basi ule kwanza chochote kabla ili usije ukala hukumu ***(1wakorintho 11:34)***. Na akiwapo mtu maskini asiweza kujilisha ao kuilisha familia yake! Hakikisheni kuwa naye awe amepata chakula nyumbani kwake ili haja yake isijulikane na wote, na ukarimu wenu uwe na heshima kama kiungo cha mwili wa kristo.

Kungojeana kunajumuisha mambo mengi sana. Kama kweli Yesu ndiyo kichwa changu, nitaheshimu na kungoja wazee na walio komaa kuliko mimi. Nitamtambua kristo ndani mwao. Hivyo ndivyo **Waebrania 13:8** anasma: ***" yesu kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele".*** Kifungo hiki cha maandiko hakielezi tu kuhusu Yesu peke yake. Ndiyo ni kweli kwa Yesu. Andiko hili linaeleza juu ya yale tunayoyaona kama matokeo ndani ya maisha ya mtu. Je tunaona Yesu ndani ya maisha yao? Imani ndyo tunapashwa kufuata watu ambao ndani mwao tuna mwona Yesu Kristo. Hawaoni aibu kunyenyekewa!

Kama kweli ninatembea na Yesu kama kichwa changu, kama kiungo pevu cha mwili wa kristo, nitamtambua na kupokea hata Yule aliye mdogo wa kiungo cha mwili. Nitamuona Yesu ndani mwake. Na kama nina usalama ndani ya Yesu, sitamuomba yeyote kuninyenyekea mimi. Kama hawaoni Yesu ndani yangu na kama Roho mtakatifu hakunizungumzia kwa nini basi nIshuritishe? Nitawezaje

**MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA ;**

1. **Tusemeje juu ya "Baba wa kiroho" hatuwahitaji Baba wa kiroho kutushauri na kutufungua katika maisha yetu?**

Ni kweli, Paulo alimwita Thimoteo ***" mwanangu mpendwa katika imani" (1 thim 1:2)*** na alienenda ndani ya shauri, ushirika mbele ya timoteo. Paulo pia alionyesha nia ya Baba

halisi kinyume na waalimu wengi wa wakati ule ***(1wakorinto 4:15-17)***. Tatizo la Baba wa kiroho kama tulivyoona kwenye mpangilio wenye aina ya mnara, ni kwamba kunakuwa na hali ya kutawala, pesa na kununuana . Hilo ndilo linalotokea tunapotaka kila mtu awe na Baba wa kiroho na kila mwana kumheshimu Baba wa kiroho kwa kumpa moja ya kumi.

Mfano uliyotolewa ni wa Yoshua chini ya Musa, Elisha chini ya Eliya na Timoteo chini ya Paulo. Somo tulipatalo kwa mifano hiyo ni kuwa unapashwa kuwa na ushirika wa Baba" kukufungua katika maisha yako ya baadaye" lakini tukitizama mifano hiyo inayotajwa, tunaona Musa, Eliya na Paulo wao wenyewe hawakuwa na Baba wa kiroho. Mifano hii inatupa maana kwa sehemu mbili ni vema kuwa na ndugu aliyekomaa katika imani, mshauri, Baba wa kiroho lakini si lazima ao muhimu kutokuwa nao haikukatazi kutimiza yale yaliyokusidiwa kutimizwa. Kwanza Paulo anasema, sababu ya kutokuwa na mshauri katika imani kama uhalali wa ufunuo alioupokea moja kwa moja toka kwa Yesu. ***'lakini wale wenye sifa ya kuwa wana cheo, (walivyokuwa vyovyote ni mamoja kwangu, Mungu hapokei uso wa mwanadamu), nasema hao wenye sifa hawakuniongezea kitu.." (Wagalatia 2:6)*** alieleza alipozungumza kuhusu mitume pale Yerusalemu. " Wale waliokuwa kitu! " Baba halisi wa kiroho huwaongoza wanao kwa Baba wa mbinguni na kuleta maneno ya Yesu mioyoni mwao ili wasichukue nafasi mbaya katika ushirikiano wao. Waliomwona Yesu hawajiamini sana wala kuwa kama

watawala ***" bali ninyi msiitwe Rabi, maana mwalimu wenu ni mmoja na ninyi nyote ni ndugu wala msimwite mtu Baba duniani; maana Baba yenu ni mmoja aliye mbinguni. Wala msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndye kristo. Naye aliye mkubwa kwenu atakuwa mtumishi wenu. Na yeye yote atakayejikweza, atadhiliwa, na yeyote atakayejikweza, atashushwa!." (Math 23:8-12)*** .

**Tuseme nini kuhusu Baba wa kiroho wanao waomba watoto wao wa kiroho moja ya kumi?.**

Paulo anasema maombi yao ya pesa inawaondolea heshima ya kuwa Baba wa aina yeyote na kueleza wakorinto nia yake kama Baba." ***Wala sitawalemea maana sivitafuti vitu vyenu bali nawatafuta ninyi, maana haiwapasi watoto kuweka akiba kwa wazazi bali wazazi kwa watoto" (1wakorinto 12:14)***

2. **NA VIPI KUHUSU MTUME YVAN AO NABII JIMY? NI KWELI WALA HAPANA? TUTAWATAMBUAJE ?**

Kulingana na ***Mathayo 7:21-23***, waongo waweza kutenda miujiza, ishara, na maajabu huku wakitenda uovu, hawafanyi mapenzi ya Baba na hawamjui hata ishara ziwe kweli. Katika jhema la Yesu hazifahamishi huduma, karama vivyo hivyo. Badala yake tabia, uaminifu na upendo ndivyo vinavyofamisha huduma, karama na mtu. Kulingana na

Yesu katika **Mathayo 23** ishara zea waongo ni kwamba wanawabesha watu mizigo mizito mabegani (sawa kutoa moja ya kumii kwa shurti) na kupenda vyeo, na kutambuliwa hadharani. Kulingana na (**Mathayo 20 :25-28),** waongo hao hufahamika kwa hali yao ya kuongoza ambayo ni kama ile ya dunia, badala ya kuiga mfano wa huduma ya kujitoa ya Bwana.

Kulingana na Paulo katika **(Matendo 20 :30),** waongo wanatambuliwa kwa mtindo wao wa kuwavuta watu kwao" wakiwaambia maneno ya upotevu" sawa na kuwalazimisha kuwa Baba wa kiroho.

Kulingana na Paulo katika **2 wakorinto 11** alama za mtume wa uongo ni katika hali yake yakujifanya kiongozi wa watu na hali yao yakuchukua pesa kwa watu, Asiye wa kweli anaonekana kwa kuegemea kwake katika mamlaka na pesa. Asiye wa kweli (wa uongo) wanatumia karama halisi, muujiza halisi, nguvu za Mungu ili kujivutia watu na kuwatumia watu hao wa Mungu kujipatia pesa. Baadhi ya makanisa za kisasa ni mchanganyiko wa ibada ya kuabudu mtu, wala pesa . Bibi arusi wa kristo ameraruliwa! Tangazo ngumu ? Rafiki yangu huko Nigeria anasema kuwa andiko la pekee linalohubiriwa katika jimbo lake ni **Malaki 3.** Viongozi hushurutisha watu wao kutoa moja ya kumi na sadaka wakiwavutia kwa kuwahidi baraka watendapo hayo na kupanda woga wala laana wasipotenda. Viongozi huendesha magari ya aina ya mercedes Benz wakati ambapo watu wao hawawezi kuwalisha watoto wao.

Unasema ndiyo, lakini hii ni Afrika utitaka kuona asili kalisi ya jambo fulani ni vema kuangalia chanzo chake.

Chukua injili ya mafanikio ya wamarekani na fikiri chanzo chake. Huko marekani yaweza kuwa si mbaya, kwa maana karibu kila mtu ana uwezo wa kulisha watoto wake. Kutoa na kupokea ina maana 6 ami Africa ? inafananishwa na kumwibia masikini, ni wizi halisi. Kama yule anayehubiri imani anaamini sana kanuni ya kupanda na kuvna kwa nin basi asigawe kwa kila mtu ndani ya umati Euro 100 ili apokea mavuno ya imani yake na ya sadaka yake ? sababu infanyayo asitende hivyo ni kwa sababu mwenyewe anafahamu haiwezekani. Anafahamu ni uongo. Kwa nini watu wengi wanatoa kwa uongo na ujanja huo ? wanapenda kuamini uongo. Ni mchezo wa kamali » ya kikristo ladba mara hii, nitakuwa na imani ya kutosha, labda mara hii mhubiri ana upako mwingi, ladbda mara hii mambo yataendeka kwangu. Labda mara hii ndiyo siku yangu ya kupenya kipesa.

- Wakati mmoja katika mazungumzo, mtu mmoja alisema kuwa baadhi ya wahubiri wazungukaji ni kama makahaba, wachungaji huwalipa kusudi watu wasaidiwe kiroho, kusudi watu waendelee kuja na sadaka ziwe nyingi. Wakati mwili unakuwa biashara, ni ukahaba. Na mwili wa kristo sasa ?
- Rafiki mwingine husema daima, tunasikia mengi yasiyofaa kuhusu pesa ndani ya maisha ya ukristo. Kuna wengi wanaotafuta faida yao katika mwili wa kristo » hivi karibuni John Wimber alichukua taxi toka airport kuelekea mahali alialikwa kama mnenaji. Alianza kuzungumza na derava

taxi, na wakati dereva taxi alipofahamu kuwa ni kiongozi wa kikristo alianza kuongelea juu ya kashfa za pesa na ngono zinazowakabili wahubiri maarufu wa kikristo. Aliwafahamu wote dereva huyo alipotulia Wimber alimuuliza « kama Yesu yupo na kanisa lipo, unafikiri kanisa lingefanya nini ? dereva taxi akamjibu, wapendane na kusaidia maskini. Ulimwengu unafahamu yale tungetenda na namna tungeishi. Ni mkasa kuona wengine wanaoitwa wakristo hawatendi hayo.

3. **Je? Vipi Wale wasemao kuwa mwili wa kristo sio demokrasia, bali theokrasia (uongoziwa Mungu) na kwa jinsi hiyo hatupaswi kunyenyekea uongozi uliowekwa na Yesu na zile huduma ?**

Ni kweli, mwili wa krito ni theokrasia (uongozi wa Mungu), lakini unaponyenyekea mamlaka ya mtu mwingine, haumo tena ndani ya theokrasia. Umekuwa chini ya utawala wa kifalme. Ndiyo maana Mungu na samweli katika ***1 samweli 8 :1*** hawakutaka kutoa mfalme kwa watu ***» kwa maana hawakukutaa wewe bali wamenikataa mimi ili nisiwe mfalme juu yao '…*** hakuna utawala uliotolewa ndani ya mwili wa kristo. Kuna utawala uliotolewa wa kifalme kwa kila mwanamemba na utawala huo tunautumia kwa kuhudumiana mmoja kwa mwingine. Iweni waangalifu wakati viongozi wanapozungumzia sana kuhusu Saulo, Daudi na sulemani

Mifano yetu sio ya Daudi na Sulemani. Mfano wetu ni Yesu na Paulo. Tumo katika theokrasia na Yesu ndiye mfalme

sisi sote ni watumishi wake na ndugu zake. Je mnawataka mabwana ao ndugu ? , Nini kinatokea wakati ndugu hawapatani ? Mnapokubaliana kutembea na kutumika pamoja, mnastahili kuelewana hata nyote mtapofikia mamoja toka kwa Bwana na kama hamwezi kupatana ? kama Paulo na barnaba katika Matendo 15 :36-40, mkubaliane kutopatana na endeleeni na kazi.

4. **Vipi kuhusu makosa na mafundisho ya uongo ndani ya makanisa ?**

Mniruhusu nimnukulu Rolland Allamé » imani halisi hutokana na ujuzi wa uwezo wa kristo badala ya mafundisho ya kawaida ya akili . Mafundisho ya uongo sio matokeo ya ujinga, bali yanasambazwa na wajuzi ». Je tunaamini sana Roho mtakatifu kuliko Yesu ? Aliamini kuwa Roho mtakatifu atatuongoza katika kweli yote. Aliamini wakati alipowaacha wanafunzi wake baada ya kukaa nao miaka mitatu. Je tunajitegemea wenyewe wala tuna mtegemea Roho mtakatifu ? Je tungeandika Yohana 16 kwa wanafunzi wetu ?

5. **Unataka kusema wale wote walio na huduma kubwa wana nia mbaya, na kwamba wale wapandao juu ya punda wanatenda hivo kusidi waonekane ?** [7]

Ndiyo, inaelekea hivyo bali kuna watumishi wengi, na viongozi walio kwenye mazingira tofauti. Mungu aliumba tembo na miti mikubwa. Kuna viongozi wazuri tu walio juu

[7] Rolland Allan » the spontaneous expansion of the cherche page 126 (london workld domining)

ya tembo na wana funzi wengi wapendao kuzilisha tembo. Lakini lengo sio la kuwapata viongozi bure wa tembo walio na moyo wenye nia njema na kutetea wale wote wenye nia tete za kujenga tembo. Kusudi (lengo) liwe ni la kufanya wanafunzi wa Yesu na kuwafa kwa njia aliyotuamureu kutenda.

Je sisi ni wanafunzi wa Yesu ao wanafunzi wa tatu waliofaulu ? Ukweli ni kwamba hata pamoja na nia njema tukitenda mambo ambayo yesu hakutenda wala kutuamuru kutenda, tunajikuta mahali palinya. Sisi ni wanafunzi kwa mfano wa yesu na wa aini za Yesu ! Hata hivyo ulewi na mna gani mtu aliye na ufunuo wa wazi kuhusu Yesu kristo na ufalme wake amaweza tosheka na kuendelea kuzilisha tembo !

## SURA YA 8

## KUKATALIWA KUKUBALIWA NA UTU WETU

***« Na mji wowote mtakasiuingia, nao hawa wakazibishi, tokeni humo, nanyi mkipita katika njia zake semeni, hata mavumbi ya mji wenu yaliyogandamana na miguu yetu tunaya kunguta juu***

***yenu. Lakini jueni hili, ya kuwa ufalme wa Mungu umekaribia « luka 10 :10-11).***

Mashamba ni meupe, tayari kwa mavuno, lakini kama haupo kelewe yakungungute mavumbi mahali hapo na endeleeni ! Yesu anatupa tahadhari hapa ! wote hawakunipokea na wote hawatawapokea. jivikeni ujasiri huo na wala kukataliwa kusiwavunje moyo » Mfahamu kuwa si kwa ajili yenu ninyi ni kwa sababu ya ufalme wa mbingu uliokaribia watu nao wakaukataa.

Mtu mmoja alisema « *jehanamu ni kupokea kile ulichoomba na kupata yale tuliyo tamani. Unakataa ufalme wa mbingu* ? Mungu ataheshimu uchaguzi wako juu ya mahali utaishi milele na utagundua hayo wakati ambayo neema ya Mungu haitakuwepo tena. Unataka tusikusumbue ? utagundua jinsi gani uko mpweke bila uwepo wa Mungu. Unataka kutenda mapenzi ya Mungu ? utapokea uzima wa milele na utafurahia.

Hakuna jambo baya sawa baridi kali. huwezi kuongeza lolote ili baridi iongezeke. Unaweza tu kukifanya kitu kiwe baridi mno kwa kuondoa nguvu za (colorie). Ni ukosefu wa nguvu za joto ndyo unaweza ongenza kitu kuwa baridi. Hakuna kilicho sawa na giza. Huwezi tenda lolote kuongeza giza mno. Giza linakuwa giza kali unapoondoa nuru. Giza kuu ni ukosefu wa aina yeyote ile ya muru.

Hakuna chochote kama ubaya. Hatuwi wabaya kwa kupokea daima ubaya, lakini kwa kukataa haki. Ubaya kamili ni ukosefu wa haki. Hamna lililon sawa na chuki. Huwezi kumfanya mtu achukie mno kwa kumwongezea

chuki. Mtu huchukia daima anapokataa upendo. Chuki ni ukosefu wa upendo.

Unakataa ufalme wa Mungu? Unamkataa Mungu unakataa haki na upendo wake? Ataheshimu uamuzi wako, hataruhusu ufalme wake, upendo wake, nuru yake haki yake na neema yake kutiririka kwako na ata kaptenda hivyo, utaelewa ni yeye chemchemi ya mema yote.

Mungu hakuumba ubaya, Mungu haja ruhusu ubaya anaturuhusu kuwa na njia zetu. Unaye mkataa? Anaheshimu uchaguzi wako na utaachiwa ndani upweke wenye giza kuu. Kukubaliwa na kukataliwa kunatisha. Uhuru wa mwanadamu kuchagua ni muhimu kwa ajili ya maisha ya milele. Lakini, ni jambo la kushangaza kuwa Yesu anajilinganisha nasi tunapoingia katika mavuno, maana mtu akitukubali ao ukitukataa, hiyo ni kumkataa ao kumpokea Baba wa mbinguni. Sisi tu mwili wake na ametufanya kuwa mmokaj ndani yake. Ni ukweli huo iliokutana na Paulo njia ya Dameski, ***(Matendo 9:4-5)*** Yesu alipomuuliza" ***Sauli, Sauli kwa nin unanitesa? Akasema" wewe ni nani Bwana? Ndipo Bwana akamwembia" mimi ni Yesu unayetesa".***

Yesu anatoa mlingano kamili katika **Mathayo 25** alipowasifu wenye haki kuwatembelea wagonjwa na wafungwa kulisha wenye njaa kuvika aliye uchi, kumtunza mkimbizi. Akawambia wakati wowote mlipo mlitenda haya kwa mojawapo wa wadogo hawa, ni kwangu mimi mlitenda" anaendelea mlingano huo alipowaambia walio mkono wake wa kushoto wakati wowote hamkutendea mojawapo wa

wadogo hawa ni kwangu mimi hamkutenea" kukataliwa, ndiyo kukataliwa.

Mara nyingi watu wenye nia njema hutoa swali ngumu. Mungu yuko wapi katika mateso mengi kama na haya? Kwa nini Mungu anaruhu haya yatokee? Kwa nini kama ni Mungu mwenye upendo asiingilie kati? Je ana uwezo ao utendaji mdogo? Ao jinsi gani aweza kuwa Mungu mwenye uwezo na mamlaka na aliyeziumba mbingu na inci na asiingilie kati? Je yeye ni dhaifu kiasi cha kutodhihirisha upendo wake? Mungu hutazama ulimwengu alioumba, hutizama mwanadamu alivyompa uhuru, mwanadamu aliyekabidhiwa kutunza na kuuchunga ulimwengu huu na anauliza masali yale yale. Kwa nini unaruhusu mateso haya kudumu? Je umekosa uwezo kweli? Haujali hata kidogo? Ni kweli, hakuna mtu awezaye tenda lolote kuhusu haya, lakini mmoja wetu aweza tenda kitu Fulani. Kwa nini basi utendaji wetu ni mdogo? Tuna uwezo na mamlaka ya kulisha, kusomesha, kuhifadhi kila mtu ulimwenguni. Isipokuwa tu hatuna nia. Tunapendelea kutawanya hela (pesa) kwa ujenzi wa nyumba, kongamano, na kadhalika kuliko kulisha watoto wadogo.

Mungu yako wapi katika mateso yote haya? Yako kwenye sehemu mbili. Yumo ndani ya yule anayeteswa. Yumo ndani ya mtu mdogo sana ulimwenguni na yumo pia ndani ya mwili wake. Yumo ndani ya watu wake. Mungu huonekana wakati watu wake wanapohudumia wanaoteswa. Mungu anaonekana wakati watu wake wanamkumbatia mtu Yule asiyefaa wa ulimwengu.

Ufunuo huu wa Mungu sio ule wa nguvu na uwezo wa Mungu ufanyao kwamba watu wote wamwabudu! Maabudu ya kulazimishwa sio maabudu. Ni Mungu aliyefanyika mwili. Ni neno lililofanyika mwili ambao wanadamu wanatamani kuuona utukufu, utukufu kama wa Mwana wa Mungu unaojaa neema na kweli. Ni Mungu aliyefanyika mtoto mchanga tumboni mwa bikira, aliyekua akisema, acheni watoto wadogo waje kwangu maana ufalme wa Mungu ni kwa wale walio kama wao. Watu wanaochagua kuona utukufu huo, wana chagua pia kupenda kuabudu na kuwa sawa na yeye. Wana chagua kumruhusu awajaze, aishi ndani mwao na kupitia wao wana chagua kumkumbatia mtu anayedharaulika wa ulimwengu.

"Yote ni juu ya mpangilio wa ufalme wa mbingu kuna mtu asiyefaa ulimwenguni. Ule asiyefaa ulimwenguni ni Yesu. Ni ufalme uliopinduka.

**MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA**

1. **Kwa hiyo Mungu hajaumba ubaya?**

Hapana , Mungu Aliumba ulimwengu na malaika wenye uwezo wa kuchagua, kuabudu utukufu wake ao kukataa. Giza na chuki ubinafsi na uchu wa madaraka ni matokeo ya nia iliyokataa utukufu wa upendo.

## SURA YA 9

## KUFURAHIA UHUSIANO

***" Ndipo wale sabini waliporudi kwa furaha wakisema, bwana, hata pepo wanatutii kwa jina lako.***

***Akawaambia,nilimwona shetani,akianguka kutoka mbinguni kama umeme. Tazama,nimewapa amri yakukanyaga nyoka ao nge,aoaguvu zote za yale adui,wala hakuna kitu kitakacho waahusu,lakini msifurahi kwa vile pepo wanavyowatii,bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni.''(luka 10:17-20)***

***''saa ile alishangilia kwa Roho mtakatifu , akasema, nakushukuru, baba,bwana wa mbingu na inci, kwa kuwa mambo haya ume waficha wenye hekima na akili , umewafaulia watoto wachanga , naam, Baba kwa kuwa ndivyo ilivyokupendeza !.Akasema,nimekabidhiwa vyote na Baba yangu, wala hakuna amjuaye mwana ila Baba; wala hakuna Baba ila mwana, na yeyote ambaye mwana apenda kumfunulia" (Luka 10:21-22)***

## A ) MAMLAKA YOTE

Vifungu hivi vya luka vinalingana na **Mathayo28:18-20** na vinaeleza vizuri jinsi maandiko haya yanavyo wekwa katika matendo. Yesu anatangaza kuwa ana mamlaka yote huko mbinguni, duniani na kusema amewapa wanafunzi wake "mamlaka yote juu ya adui". hakuna mahali popote katika injili tunamuona Yesu akipeana mamlaka ya aina yeyote kwa wanafunzi wake .

Vivyo hivyo katika agano jipya, kuhani mkuu hakupewa mamlaka juu ya kuhani mwingine. amri inayotawala ni kwamba "tujazwe Roho mtakatifu"

Wakati watu wake wanamkumbatia mtu Yule asiyefaa wa ulimwengu .Ufunuo huu wa Mungu sio ule wa nguvu na uwezo wa Mungu ufanyao kwamba watu wote wamwabudu!

Maabudu ya kulazimishwa sio maabudu. Ni Mungu aliye fanyika mwili.

« ***Huku tukimshukuro Mungu katika yote…Hali mnanyenyekeana katika kicho cha kristo" ( waefeso 5:18-21).*** Uhalisi wa Roho mtakatifu akaaye ndani yetu anapashwa kutenda kazi kwa kuwa heshimu wale wengine wanaojazwa Roho mtakatifu.

Kama kiti cha enzi cha Mungu kimo moyoni mwa ndugu yako kwa nini basi kujiweka juu yake? Lakini, Yesu ametupa kweli mamlaka juu ya uwezo wote wa Yule adui' ni vema kuona uponyaji na kufunguliwa ni alama ya ufalme we mbingu ulio ndani ni dhihirisho la ufalme uliopo. Ufalme wa mbingu umekuja upo hapa, na sasa vipi wakati unapoomba na hakuna kinachotokea? **Waebrania 2:8-9** inashikilia ukweli juu ya mamlaka yote na inazungumza juu ya mamlaka yote na inazungumza pia kwa nini wote hawawezi kuponya (licha ya mamlaka hiyo) katika maisha tutaendelea kushikilia ukweli huo (mamlaka).

***"Basi vitu vyote vinusha kutiishwa chini yake ndipo mwana mwenyewe atatiisha chini yake yeye aliye mtiishia vitu vyote, ili kwamba mungu awe yote katika yote " (1 wakorintho 15:20-28)*** ina ukweli ule ule. Ni Bwana wa yote lakini yote hayapo chini ya miguu yako ni mwenye mamlaka yote, lakini vyote haviji mbele yake kumwabudu.

Ufalme wa Mungu upo hapa lakini ufalme unakuja. Ufalme wa Mungu ni sasa na ufalme haujaja bado. Ufalme umekuja na ufalme unakuja. Ufalme unaweza kuja maana ufalme umesha-kuja.

Ufalme unaendelea kuja huku kola mtu anaanza kumwabudu, kumpenda na kumtii kama mfalme. Ni kwa imani ndiyo tunaona utimilifu wa ahadi ao tunangojea utimilifu wake **(Waebrania 11:40)** labda mpaka sasa hatujaona bado mambo yote chini ya miguu yetu lakini tunamwona Yesu.

## B) JAMBO MUHIMU NI UHUSIANO

Hata hivo, jambo la muhimu sio mamlaka juu ya pepo. Yesu hakufa ili uwena huduma. Alikufa ili uingie katika uhusiano na baba yake. Tafsiri ya Eugene Peterson ya **Mathayo 11:25-30** inaeleza vizuri. Kwa gafla Yesu aliomba:..... ***Na kushukuru, Baba, Bwana, wa mbinguni na inchi kwa kuwa mambo haya uliwaficha wenye hakima na akili, ukawa funulia watoto wachanga. Na sema, Baba, kwa kuwa ndivyo ilivyo pendeza mbele zako"*** Yesu alirudilia kuhotubia watu lakini kwa upole sasa ' Baba amenipa mambo yote hayo kutenda na kusema. Ni oparisheni yake Mwana **Baba**, inayotokana na uhusiano wa mwana na Baba. Hakuna amjuaye mwana kama Baba wala Baba kama mwana. Lakini sichungi lolote kwa ajili yangu, nipo tayari kumpa yeyote aliye tayari kusikiliza.

Je mmechoka? Mmeishiwa? Mmetumwa na dini ? njoni kwangu. Mtoroke pamoja nami na mchukue uzima wenu. Tazameni ninavyotenda. Jifunze mtindo wa neema. Sitaweka chochote kilicho na uzito ao kisichofaa juu yenu. Kaeni nami na mtaishi kwa uhuru na urahisi.

Kabla ya kuanguka kwa mwanadamu kabla mwanadamu kuhitaji ukombozi, kabla ya shetani kutawala duniani, kabla ya ulimwengu kuharibika na kabla ya kuwepo na hitaji lolote la mwenadamu. Mungu ilikuwa na lengo katika neno lake. Lengo hilol lilikuwa kuumba mwanadamu ili ashirikiane naye. Alitamani wanawe wawe na moyo kama wake. Alitamani ndugu ili Mungu mwana adhihirishe moyo wake ndani mwao. Alitamani hekalu linaloishi kwa Roho mtakatifu ili Roho mtakatifu aongeze kukuza Roho ya kumwabudu Baba na neno lake. Mungu alitamani kuwa siri ya moto na kujitoa ndani mwake izidishwe ndani ya mioyo ya walimwengu na wakubali kwa hiari kuingia katika moto na msukumo huo. Hatuwezi kumwita mtu "upendo" mtu mmoja pekee hawezi kuonekana kama "upendo" wa Mungu Baba, Mungu Neno, na Mungu Roho ni uhusiano wa utatu katika kunyenyekeana ndani ya uaminifu, heshima adabu na upendo Mungu ni upendo! Yesu ni kondoo aliyechinjwa na alikuwa kondoo aliye chinjwa tangu kuumbwa kwa misingi ya ulimwengu kwa sababu siri ya upendo ni uzima uliowekwa ndani ya heshima uaminifu, kujitolea kutendea wengine mema. Upendo sio hisia, sio hisia za muda. Ni kujitoa kikamilifu maishani kumtendea mwingine mema, ambao waweza kuniletea Mateso na kujitoa kwaza,

ingawaje matunda ya kujitolea huko yaweza kusababisha hisia zenye nguvu.

Yote ambayo Mungu, Baba alikusudia na kutayarisha milele yanajulishwa nyakati za agano la kale, aliyakabidhi Mungu mwana. Baba alikuwa na uhakika kuwa mwana atatenda kama atendavyo. Baba aliamini kuwa neno litasema tu yale aliyosema. Baba aliweka uaminifu wake wote ndani ya Mungu mwana na Mungu mwana aliheshimu uaminifu huo kwa gharama ya kifo msalabani. Mungu mwana hakutafuta utukufu wake mwenyewe, bali mapenzi ya Baba. Hivyo Baba husema mtu asipompokea Mungu mwana, hawezi kamwe kumfahamu mungu Baba, baba anaheshimu mungu masana katika mambo yote na anatupokea kupitia mwaka.

Yote ambayo Ysu alipokea toka kwa Baba aliyadhihirisha wakati wake na kuyakabidhi kwa Roho mtakatifu. Yesu alijiachilia kwa Roho mtakatifu ili kulifunua neno, na kamwe hakusema kwa ajili yake. Roho mtakatifu, sawa na Mungu mwana walimfunua Mungu Baba. Yote aliyotimiza Mungu mwana kwa kifo chake, aliyaweka mikononi mwa Roho mtakatifu na kumtegemea Roho mtakatifu kuleta utimilifu huo hapa ulimwenguni. Maana Roho mtakatifu huheshimu Mungu mwana, Mungu Baba humheshimu Roho mtakatifu na atasamehe makosa yote dhidi yake lakini hatasemehe dhambi ya kukataa Roho mtakatifu. Hakuna ajaye kwa Mungu isipokuwa kupitia huduma ya Roho mtakatifu. isipokuwa kupitia huduma ya Roho mtakatifu. Yote ambayo Baba, Neno na Roho mtakatifu waliyokusudia na kuyajulisha kwa wakati wake,waliyakabidhi mikononi mwa familia ya Mungu

Baba,kwa mwili wa kristo,na kwa hekalu hai la Roho mtakatifu. Mungu ambaye ni ushirika kamili wenye kuheshimiana,kuaminiana, na kunyenyekeana,alisimamia tu kwenye kazi ya kutimiza mipango yake ulimwenguni.

Makusufi yake itatimizwa kwa njia ya uhusiano badala ya matendo. Ni uhusiano wenye upendo. Upendo ndiyo mkuu. Anatualika kwenye uhusiano huo. kusudi lake sio tu la kukomboa ulimwengu ulioanguka. Kusudi lake lilikuwa kuonyesha wote na kupitia wote utukufu wa Mungu mwana kwa njia ya uhusiano wetu naye[8].

Yesu hakufa ili tu uweze kuendesha maisha mema na furaha ni hali ya dini. Yesu alikufa ili uishi kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Wakati uliopita (wa kale), kwa stefano ilimaanisha kufa kwa kupigwa mawe. Kwako wewe ina maanisha nini ? Mungu ni hakimu wa yale yaliyo utuku wake, sio wewe. Yesu hakufa ili uishi heri mbinguni nayo pia ni hali ya dini. Mwanadamu sio kiini ao kipimo cha kwa ajili ya utukufu wa Mungu hapa na sasa hivi.

## NILIWAITA MARAFIKI ZANGU

***« Amri yangu ndiyo hii, mpendane, kama nilivyowapenda ninyi. Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu wa mtu kuutoa uhai wake rafiki zangu, mkitenda niwaamuroyo » (yohana 15 :16-15).***

[8] Ara ya kwanza nilipoelewa : ni wakati nilipomsika DERERN FROMKE alizumza juu ya miaka 70, sitasahau kamwe shauku na unyenyekevu aliotumia alipokuwa akiongea kitabu chake

Yule ambaye anagelidai heshima, cheo utukufu, mamlaka hakutenda hivyo ! alichunguza macho ya wanadamu ambayo hivi karibuni yangemsaliti na kuwaita marafiki zake. Na alipotenda hivyo aliharibu kikamilifu na daima uwezekano wowote wa vyeo vya wanadamu kuwakilisha ufalme wake. Minara ni kwa ajili ya wafu !

Mble ya kiti cha enzi kuna bahari ya kioo ! hakuna mlima wala bonde juu ya bahari. Kila bonde litainuliwa na kila mlima utashushwa. Sisi sote ni ndugu na dada mbele ya kiti cha enzi ! ndiyo sababu kuna amri arobaini (40) zina zohusu « mmoja na mwingine' ndani ya agano jipya ! iliyo kuuzaidi ni urafiki ndani ya kila uongozi, watu wa chini ni watumishi.kiongozi waweza tumia kutoamini. Minara hujengwa na watumwa. Katika kila uongozi watu walio juu yako ni watawala na mabwana.

Unaweza kuwa mnyenyekevu lakini mara nyingi una shauku ya kutaka kuchukua na fasi yao unawezatumia lugha ya urafiki, heshima na adabu lakini ufanisi unapitia kwa ngazi.walio chini yako na kando kando yako na pinzinani wako. Yesu anatuamuru tusiongose kama mataifa wanaowatawala watu wao kwa nguvu. Tuongoze kama alivyotendant yesu. Kusudi la uongozi wake ni kutoa moyo wake na kutoa maisha yake kwa rafiki zake. Kama lengo lake ni kupanda mangazi hutaka marafiki utapatatu watu utakaowatumia.

Tafsiri ya **Eugene Peterson ya 1wakoriontho 10 :14** inatupa changamoto , ***''kwa ajili ya hayo rafiki zangu wapendwa, muonapo watu wamfanyapo Mungu kama kitu ambacho***

***wanaongoza wala kutumia , ondokeni miongoni mwao haraka iwezekanvyo »*** lengo la kufanya wanafunzi ni kujifanyia marafiki kuanzisha urafiki unaoumba uhusiano na Baba, neno na Roho mtakatifu. Lengo ni kutunza uhusiano ambao ndani mwake ulimwengu wetu waweza kuona upendo, kuheshimiana, kuamiana, na kazi katika uungu.

Mfano wa Yesu unaoelezwa katika **Yohana 16,** ni wakushangaza ! ***« lakini mimi nawaambia iliyo kweli ; yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoindoka, huyo msaidizi hatakuja kwenu, bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu »(yohana 11 :6)***

Wanafunzi hawakufikiria kuondoka kwa Yesu ! Yesu kiongozi bora asiyewahi kuonekana duniani , akiwaambia ni vema kwenu niondoke !na sisi tunaona kuwa tu muhimu, wanaostahili hata ? Tunafiri tu watu gani ? Yesu alifahamu kuwa ilibidi wanafunzi waongoze kwa ndani na Roho mtakatifu badala ya mwili na damu ! Yesu alitamani rafiki zake wawe na moto ule ule aliyoufahamu ndani yao.

Kazi yetu ni kuondoa kila pingamizi linalozuia rafiki zetu kufahamu uongozi wa ndani wa Roho mtakatifu na utendaji wa Bwana yesu juu ya maisha yao na yetu kwa jumla.

Maelekezo mengi ya wanadamu husababisha maendeleo ya watu itutegemee sisi, wajitoe kwetu, watarajie kwetu, watuheshimu, na watusaidie hata. Kuanzisha hali ya kutegemewa,ni kuanzisha ufalme wako mwenyewe ni kumsaliti mfalme wa wafalme .

Yesu aliamini sana uwezo uliomo ndani ya utendaji wa utendaji wa Roho mtakatifu kuongoza watu katika kweli. Je?

ndivyo tulivyo ? ndyo maana yesu alisema alistahili kwenda. Ndiyo maana alitoa amri kwa wanafunzi kufanya wanafunzi na pia kwenda kwa kijiji jirani

Kama kwa unyenyekevu wote siwezi pokea kweli toka kwako ni kama sijawahi kukupenda wala sijawahi kukuamini kama rafiki . Sehemu kubwa ya mwili wa kristo imo katika hali ya kuchelewa kiroho na uchanga mkubwa, sababu wanasikia kweli zinazoelezwa toka madhabahu ya kweli mbili. Kweli inayotolewa na kupokelewa toka moyo wa rafiki. Ukitaka kufanya wanafunzi pangilia kwa kulijenga kanisa lake.

## MASWALI YANAYOULIZWA MAKA KWA MARA

1. **Kuhusiana na majengo, je si ni hakika kwambo kanisa la agano jipya hali kuwa na majengo kutokana na umaskini wao na dhiki (kuteswa)?**
2. Ni sawa, hakuna thibitisho lolote la kihistoria kuhusu majengo ao mpangilio wowote ju mikutano wakati wa karne tatu na kwanza na kanisa. Ingajawaje si kwa sababu ya umaskini ao mateso. Waamini wengi walikuwa na pesa na hata kama kulikuwepo na nyakati za mateso kulikuwepo pia na nyakati za amani na uhuru. Walikuwa na utajiri na uhuru wa kujenga majumba kama walivyotamani. Kumbuka kuwa presha ya mila ilikuwa juu ya kanisa hili la kwanza ili hujinga na kutumia majumba maalumu kukusanyika. Upande mmoja kulikuwa na mtindo wa kiyaudi wa sinagogi, majumba yake na marabi. Na upande mwingine Mtindo wa kirumi na hekalu za kipagani na makasisi wake. Hata kama kanisa la kwanza lilipambana

na mateso makali sababu hawakuwa na majumba maalum ya kidini. Kwa warumi, kama hamna hekalu na madhababu, alikuwa mpagani na ndyo maana kanisa la kwanza liliteswa sana!

Shinikizo la nyumba lilikuwepo na pesa zilikuwa tayari! Lakini watakatifu hawa wa kwanza hawakujenga majumba kutokana na ufunuo ao kutokana na imani waliamini ukuhani wa waamini wote kwa hiyo hwakuunga mkono, ao kulichukulia hatua tabaka Fulani ya ukuhani. Waliamini kwamba ufalme wa mbingu ulikuja na unakubali yote ya mwanadamu kwa Mungu! Yesu alikufa kutakasa uzima wote na kazi yote ya mwanadamu kwa Mungu. Walikutana ndani ya nyumba, walikuwa na uhakika kuwa miili yao ni hekalu la Roho mtakatifu maana Mungu hakai ndani ya hekalu lililotengenezwa kwa mikono ya wanadamu bali ndani ya hekalu hai lililotengenezwa kwa mawe yaliyo hai. Mahali palipo na uzima kuonyesha kwamba Yesu yu kati yao.

Wakikubaliana na imani yao kuwa hekalu ya Mungu ni watu wa Mungu, hawakuwekeza pesa ndani ya tofali na kina balindani ya watu. Sadaka katika agano jupya ilichukuliwa kwa ajili ya wahanga wanjaa, mayatima, wajane na maskini. Tungeweza kutosheleza mahitaji ya maskini kuhusu malazi, masomo, chakula, na maji kama pesa zinazowekezwa katika majumba, vyombo vya muziki vingewekezwa ndani ya hekalu la kweli la Mungu yaani watoto wa Mungu. **Mathayo 25,** inasema kwamba ***"kinachotendewa mojawapo wa wadogo hawa***". Ndicho

kipimo ambacho wanaojiita, wanafunzi wa Yesu watahukumiwa kwa hicho, ndicho kipimo ambacho Yesu atatumia kutenga kondoo na mbuzi (ndama na mbuzi dume). Ule upendo wetu kwa watu na kumtumikia Yesu havitokani na majumba. Majumbani ni falme zetu wenyewe. Majumba ni miradi ya uwezo na umaarufu, ni minara yetu na haja yetu ya kutaka kufanana na dini zingine kando kando yetu.

Kila dola linalowekezwa katika ujenzi wa jumba, ni dola inayopungua kulisha mwenye njaa, kuvika aliye uchi, kumhudumia mgonjwa na kuwatembelea walio gerezani. Kila jengo ni mnara wa ubinafsi na kiburi. Kila dola iliyowekezwa itahukumiwa na Yesu kama pesa mbuzi

Wanatumia historia za agano la kale juu ya kujenga hema ao juu ya ujenzi wa hekalu wanadanganyika. Hatumo tena ndani ya agano la kale

hata hivyo nia, hizo zimezama sana!! Baraza la mji wa Yerusalemu lilijawa na hasira ya uhusiano wa Mungu na taifa la wayaudi ila yeye aliye juu hakai katika nyumba zilizo tengenezwa kwa mikono, kama vile asemavyo rabu (Mdo 7:48).

Stefano alikemea hali yao ya dini na hali yao ya kupata faida maisha aliposema hekalu lillitengenezwa kwa mikono ya mwanadamu sio mahali pa mapumuziko ya mungu. Wafia dini wa kwanza wa kanisa, alitoa uzima wake akitangaza kuwa mungu anaishi sasa ndani ya watu badala ya kuishi ndani ya majumba za dini yeyoteb anayethubutu

kushambulia mvuto huo wa kuabudu sanamu za majumba , anapambana na vipingaamizi hivyo hata leo.

Je? Ni kuwa mgumu kuongelea juu ya" pesa ya mbuei? mniziehusu kueleza hadithi tatu maja ilitokea karibu ya nyumbani kwangu canada

Kundi moja la vijana lilifanya safari ya kimishonari katika inci moja ya ulimwengu wa tatu. Wakiwa huko walitembelea na kutumika ndani ya nyumba (kituo)chakula watoto yatima walitambua kwamba watoto walikuwa njaa maana msaada wa pesa ulikuwa umipungua na bey ya mchele ilikuwa imependa mara drufu mwaka ule.

Mitume wametolewa na Mungu kama zawadi kwa Kanisa na kwa ulimwengu **( Waefeso 4 :11)** na tunawahitaji. Kanisa bila mitume ( manabii, ni kama moto pasipo miali yake). Tatizo la mwili huo ni nini ? Tumeondoa kiungo moja muhimu , kiungo cha Mtume, na badala yake tumeweka elimu,uongozi wa Dini, mwili na kadhalika…( na baadhi ya karama zimelala na hazileti utukufu kwa Mungu – Kazi ya itume ni kama nguzo katika kuandaa mwili wa Kristo kwa huduma na kukomaa ; **( Waefeso 4 : 11 ).** Baadhi ya Mitume hawaonekani « Kanisani kama tujuavyo » na ndyo sababu moto unawaka mahali pengine. Yesu ndye Bwana – Kama alivyotumwa, naye amewatuma wale alio nao ili wateswe na kumtumikia wakitangaza uwepo wake na ukamilifu unaokuja wa ufalme wake. Mitume na manabii ndyo msingi wa « Kanisa kama vile Mungu atakavyo. » **( Waefeso 2:20; 3:5-6; 4:11 ) .**

Tunahitaji kwamba wafunguliwe. Ni Mitume na Manabii wenye herufi ndogo “ A” na herufi ndogo “ P”, watu wa tabaka ya chini ambao sasa wamekuwa wa thamani kwa Mungu kupitia Yesu Kristo. Hatuzungumzii kuhusu mtindo mpya wa “ one man Show” anayelisumbua Kanisa kama tunavyolifahamu. Kuna Mitume na manabii wenye herufi ndogo “P “ na herufi kubwa “ S” mwishoni.

Na Mungu amewapa wengine kama Mitume, na wengine kama Manabii. Hatuitaji wa super stars. Tunahitaji walio mfano usemao ***" Hali mnanyenyekeana katika kicho cha kristo "*** **(Waefeso 5:11).**

Tafadhali Bwana tuma watenda kazi wako katika Mavuno..!!!

BrianJosephdodd@yahoo.com

14/1/2007

**Ruhusa imetolewa kutumia na kufwata BrianDodd (Mwalimu wa somo la Agano Jipya, Sheffield University) Ni mwandishi Wa " kuhimiza uongozi wa kanisa": Kuhudumu katika Roho kulingana na Paulo.(Dowers: Intervasity Press,1991).**

**APPENDICE-2**

**KANISA LA NYUMBANI KATIKA AGANO JIPYA [27]**

Tutaanza sehemu hii kwa kufata habari ya Luka na tutaeleza namna Yesu alivyoitimiza huduma yake katika nyumba za watu. Ndyo , Yeye na Paulo na mitume wengine wilitekeleza huduma zao ndani ya sinagogi hata kwenye milango ya hekalu mwanzoni mwa kitabu cha matendo : hata hivo ni wazikuwa Paulo alifikia wamuzi wa kutowa- endea , isipokuwa kwa wapagani.Mdo ***(Mdo 18 :6-7).*** Kitabu cha Matendo kinaeleza pia kuwa : *"**wayaudi wengi ....waliamini walivyo elfu nyingi, nao wote wana wivu sana kwa ajili ya torati...". (Mdo 21 :20)***

Hata hivo sehemu hii ya maandiko hakuishi sana kwenye karne ya tatu, bila shaka maana wale waliyomwamini yesu walimezwa na mtinfo wa sinagogi. Kwa hiyo, kulikuwepo na mchauganiko wa mahali pa mikutano mwanzoni, Lakini kwa wale ambao Agano jipya kwa ajili yao liliandikwa walikutuana popote pale ambapo uzima ulidhihirika na ilikuwa zaidi sana katika manyumba.

**A) Vifungo vya maandiko tisa, vya Luka na huduma ya Yesu ndani ya nyumba :**

- ***Luka 5 :19 : "Hata walipokosa nafasi ya kumpeleka ndani kwa ajili ya lile kundi la watgu, walipanda juu ya dani wakampisha katika matofali ya juu, wakamshusha yeye na kitanda ckake katika mbele uya Yesu ".***
- ***Luka 5 :29 : " Na la wi akamfanyia karamu kubwa nyuimbani mwake : palikuwa na mkutano mkuu wa watotot ushuru na watu wengineao walikuwa wa meketi chakulani Pamoja nao ".***
- ***Luka 7 :36 : " Mtu mmoja katika mafasiriyo alimwalika aje ale nyumbani yake yule farisayo, aka keti chakulani ".***
- ***Luka 10 :39 : " Naye alukuwa na umbu lake aitwaye mariamu, aliyeketi miguuni pake Yesu, akasikiliza maneno yake "***
- ***Luka 11 :37 : " Alipokuwa akinena farisayo mmoja alimwita aje kwake ale chakula ; akaingia , akaketi chakulani ".***

- ***Luka 14 :1 : " Ikawa alipoingia ndani ya nyumba ya mtu mmoja miongoni mwa wakuu wa mafari sayo siku ya sabatoi, ale chakula, walikuwa wakimvizia ".***
- ***Luka 19 :5 : " na Yesu, alipofika mahali palre, alitazama juu, akamwambia zakayto , shuka upsesi, kwa kuwa leo imenipase kushinda nyumbani mwako".***
- ***Luka 22 :11,12 : " Na mtamwambia mwenye nyumba, mwalimu akuambia, nin wapi chumba cha wageni ? Nipateb kula sadaka humo pamoja hawanfunzi wangu ? Naye ata waonesha chumba kikubwa erofani, kimekwisha andikwa ; andaeni humo". (Sherehe ya upendo ilianzishwa na mwalimu katika nyumba.)***

**B) Vifungu vya maandiko kumi na tano vinavyoeleza kuhusu kanisa ndani ya nyumba katika Agano Jipya :**

Kwa kutizama **Luka 10,** tunaelewa kuwa Paulo mara kwa mara aliandikia kanisa la mjini akilinganisha makanisa banafsi za ndani ya nyumba za watakatifu mbali mbali . Makanisa hayo mbali mabli ya nyumbani ndyo yaliyojumuisha kanisa la mji. Wazee na mashemasi walichaguliwa toka miongoni mwa kanisa ndani ya nyumba ili kuongoza kanisa la mji. Waliokomaa walichukua uangalizi wa jumla, huku mashemasi walishugulikia na kuwatunza mayatima na wajane ndani ya makanisa.

Sasa, Paulo hajawahi kuwaandikia wazee wa kanisa , bali watakatifu hakutoa maelekezo kwa wazee kuwaeleza wanayostahili kutenda bali anatoa mwaliko kwa kanisa lote.

***Mdo 1 :13-14 : « hata walipongia, wakapanda ozofani , walipokuwa wakikiaa , Petro na Yohana , na yakobo, na Andrea , Filipo na Tomaso, Bartolomayo na mathoya, yakobo wa alfayo na simoni zolote, na yuda wa Yakobo. Hawa wote moyo mmoja katika kusali, pamoja nao wanawake, na ndugu zake ».***

***Mdo 2 :2 : « Kukaja gahalfa toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi , ukaijaza yote walipokuwa wameketi.***

***Matendo 2 :46 : « Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushuzika, na katika kuumega mkate, na katika kusali".***

***Matendo 5 :42 : « na kila , ndani ya hekalu na nyumbani mwaoo, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari nkema za Yesu kwamba ni Kristo.***

***Matendo 8 :3 : » Sauli akaliharibu kanisa , akiingiya kila nyumba, na kuwabuzuta wanaume na wanawake na kawatu pa berezani».***

***Matendo 10 :24 : « Siku ya pili yake wakaingia kaisaria. Na Kornelio alikuwa aakiwangojea. Hali amekusanya jamma zake na rafiki zake.***

- ***Mdo 12:12: "na alipokuwa akifikiri haya akafika nyumbani kwa mariamu, mamaye Yohana, ambaye jina lake la pili ni Marko; na watu wenyi walikuwa wsmekutana humo wakiomba".***
- ***Mdo 16:15: " hata alikwisha kubatizwa, yeye na nyumba yake , akatusihhi, akisema kama mmeniona kawa mwaminifu kwa bwana , ingieni nyumbani mwangu mkakee. Akatushuzutisha".***
- ***Mdo 16:25-34: " lakini panapo usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakimwimbia Mungu na kumwimbia nyimbo za kummsifu , na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza . Ghafula pakawa na tetemeko kuu la inchi, hata misingi ya Gereza ikatikisika , na mara hiyo milango ikafunguka, vifungo vyote vyote vikalegezwa. Yule mlinzi wa gereza akaamka, naye alipoona ya kuwa milango ya gereza imefunguka, alifuta upanga, akataka kujiua, akidhani ya kuwa wafungwa wamekimbia. Ila Paulo akapaza sauti yake kwa nguvu,akisema,usijidhuru kwa maana sisi sote tupo hapa. Akataka taa ziletwe akarukia ndani , akitetemeka kwa hofu, akawaangukia Paulo na sila ; kisha akawaleta nje akasema , Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka ? Wakamwambia , mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako . <u>Wakamwambia neno la Bwana, yeye na watu wote waliomo nyumbani mwake.</u> Akawakaribisha saa ile ya usiku,***

***akawaosha mapigo yao, kisha akabatizwa, yeye na watu wake wote wakati huo huo. Akawaleta juu nyumbani kwake , akawaandalia chakula,akafurahi sana yeye na nyumba yake yote, maana amekwisha kumwamini Mungu.***

***Mdo 16 :40 : ‘ Nao wa katoka gerezani wakangia nyumbani mwa Lidia :<na walipo kwisha kuonana na ndogu wakawafariji, wakaenda zao ».***

***Mdo 26 :30-31 : « Akakaa muda wa miaka miwili mizima katika nyumba yake aliyokuwa ameinpanga ,akawakaribisha wato wote waliokuwa wakimwendea, akihubiri habari za ufalme wa Mungu, na kayafundisha mambo ya Bwana Yesu kristo, kwa ujasiri, mwingi asikatazwe na mtu ».***

***Warumi 16 :5 : « Nisalimieni Epaineto, mpenzi wangu, aliye malimuako ya Asia kwa Kristo ».***

***Warumi 16 :23 : « Gayo mwenyeji wangu na wa kanisa lote pia awasalimu Erasto , wakili wa mji, awasalimu, na karpo, ndugu yetu”.***

***1 Wakorinto 16 :19 : «Makanisa ya Asia wawasalimu sana katika Bwana pamoja na kanisa lililoko ndani ya nyumba yao ».***

***Wakalosai 4 :15 : « Wasalimuni ndugu walioko laodikia, na nimfa , na kanisa lilio katika nyumba yake ».***

***Filemoni 1 :2 : « Na kwa afya , ndugu yetu kwa arkipo askari mwenzetu, na kwa kanisa lililo katika nyuma yako ».***

### ***C) Vifungo vya maandiko kumi a tano kwa makanisa ya ndani ya nyumba katika Agano Jipya***

Tunaposoma vifungu hivi kwa kufikiria jamii zilizo na majengo kama msingi hatutanufaika sana , bali tukivitizama kulingana na **Luka 10** na kwa sababu kanisa la Karne ya kwanza lilikuwa na msingi kwenye nyumba,wana maana tofauti kabisa kwa kuwa sehemu ya Historia ya Kanisa la nyumbani.

***Mdo 18 :7 : « Akaondoka huko akaingia katika nyumba ya mtu moje jina lake tito yusto, mcha Mungu ambayo ilikuwa mpaka moja na sinagogi.***

***Mdo 19 :9 : « Lakini wengine walikaidi, wakakataa kuamini, wakiitukana ile njia mbele ya mkutano; basi akaondoka akawacha akawatenga wanafunzi, akahonjiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja tirano ».***

***Mdo 20 :8 : « Ya kuwa sikujiepusha katika kuwatangazia neeno lolote liwezalo kuwafaa bali naliwandisha wazi wazi, na nyumba kwa nyumba ».***

***Warumi 16 :10 : « Nisalimieni Apele, mwenye kukubaliwa katika Kristo.***

***Nisalimieni watu wa nyumbani mwa aristobulo ».***

***Warumi 16 :11 : « Nisalimieni herodioni, njamaa yangu. Nisalimieni watu wa nyumbani mwa Narkiso walio katika Bwana ».***

***1Wakorintho 1 :11 : « Kwa maana, ndugu zangu, nimenrifiwa habari zenu na wale walio wa nyumbani mwa Kloe, ya kuwa iko fitina kwenu.***

***1 Wakorintho 1 :16 : « Tena naliwabatiza watu wa nyumbani mwa stefano, zaidi ya hao, sijuii kama nalimbatiza mtu yeyote mwingine ».***

***1 Wakorintho 16 :15 ; « Tena ndugu mnawajua watu wa nyumbani mwa Stefana kwamba ni malimbuko ya Akaya, nao wamejitoa katika kazi ya kuwa hudumu watakatifu ».***

***Wafilipi 4 :22 : « Watakatifu wote wawasalimu, hasa walio wa nyumbani mwa Kaisaria".***

***2 Thimoteo 4 :19 : « Nisalimieni Priska na Akila, na wale wa nyumbani mwa Onesiforo ».***

***Tito 1:11: " Hao wanapindua watu wa nyumba nzima, wakifundisha yasipowapasa kwa ajili ya mapato ya aibu.***

***2Yoh 1:1:" Mzee kwa mama mteule na watoto wake niwapendao katika kweli; wala si mimi peke yangu bali na wote waijuao ile kweli.***

## APPENDICE 3:

## VIFUNGO VYA BIBLIA VINAVYOELEZA KUHUSU UHUSIANO WETU NA WENGINE

Imani ya kweli pasipo kuwa na uhusiano mwema imani hiyo imekufa , haina uzima . Hatuwezi kujifunza urafiki kwa kuketi darasani wala kwa kusikiliza somo. Tunajifunza kuwa marafiki kwa kumfwata Yesu katika maisha yetu ya kila siku. Agano jipya limejaa amri kuhusu uhusiano.Vifungu vya biblia Arobaini vinavoeleza juu ya uhusiano wetu " wa Mmoja kwa mwingine " vinatolewa hapa na orodha yaweza kuwa ndefu kufikia hadi sabini ukijumuisha na vifungu vingine sawa na hivyo vinavyotumia maneno kama " Ndugu", " Jirani", ao " Mwanamemba".

Amri hizi zinazoonekana popote pale katika Agano jipya zinasababisha matendo uhakika katika jamii za watu na marafiki uhusiano toka moyoni ili huhudiamiana sisi kwa sisi na kwa namna hiyo kumtumikia mfalme aishiye ndani ya kila mmoja wao .

1) ***Yohana 13:34-35, "Amri mpya nawapa mpendane kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watawatambua kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi....".***
2) ***Yohana 15:12:"Amri yangu ndyo hii , mpendane , kama nilivyo wapenda ninyi".***
3) ***Yahana 15:17: "haya nawaamrzu ninyi, mpate kupendana".***

4) ***Warumi 12:10:" Kwa pendo la ndugu, mpendane ninyi kwa ninyi.***
5) ***Warumi 12:10:"Kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu".***
6) ***Warumi 12:16:" Mpatane nia zenu ninyi kwa ninyi. Msinie yaliyo makuu, lakini mkubali kujishughulisha na mambo manyonge, msiwe watu wa kujivunia akili."***
7) ***Warumi 13:8:" Msiwiwe na mtu chochote, isipokuwa kupendana , kwa maana ampendaye mwenzake ameitimiza sheria".***
8) ***Warumi 14:13: " Basi tusizidi kuhukamiana, bali afadhali toeni hukumu hii, mtu asitie cha kumakaza ndugu ao cha kumwangusha".***
9) ***Warumi 15:7, Kwa hiyo mkaribishane ninyi kwa ninyi, kama naye Krsito alivyotukaribisha ili Mungu atukuzwe.***
10) ***Warumi 15:7: " Ndugu zangu nimehakikishwa mimi mwenyewe kwa habari zenu ya kuwa ninyi mmejaa wema , nimejazwa elimu yote , tena mwaweza kuonyana".***
11) ***Warumi 16:16: " Salimianeni kwa busu takatifu makanisani yote ya Kristo yawasalimu".***
12) ***1 Wakorintho 1:10: "Basi ndugu, nawasihi kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja".***

***13) 1Wakorintho 10:24 :"mtu asitafute faida yake mwenyewe, bali ya mwenzake.***

***14) 1 Wakorinthi 11:33 :" Kwa hiyo ndungu zangu, mkutanikapo mpate kula, mngojaneni".***

***15) 1 Wakorintho 12:25-27 :" Ili kusiwe na faraka katika mwili, bali viungo vitunazane kila kiungo na mwenzake na kiungo kimoja kikiumia , viungo vyote huumia nacho ,na kiungo kimoja kikitukuzwa,viungo vyote hufarihi pamoja nacho. Basi ninyi mmekuwa mwili wa kristo , na viungo kila kimoja peke yake".***

***16) Wagalalia 5:13-15 : " Maana ninyi ndugu mliitwa mpate uhuru; lakini uhuru wenu usiwe sababu ya kuufwata mwili, bali tumikianeni kwa upendo. Maana torati yote imetimilika katika neno moja nalo ni hili , umpende Jirani yako kama nafsi yako. Lakini mkiumana na kulana , aangalieni msije mkaangamizana".***

***17) Wagalatia 5:26 : " Tusijisifu bure tukichokozana na kuhusuliane mizigo na kuhitimiza hivyo sheria ya Kristo".***

***18) Wagalatia 6:2: " Mchukuliane mzizigo na kuhutimiza hivyo sheria ya Kristo.***

***19) Waefeso 4:2: " Kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana katika upendo".***

***20) Waefeso 4:32: " Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Muungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi".***

***21) Waefeso 5:19: "Mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana miyoni mwenu".***

***22) Waefeso 5:21: " Hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo".***

***23) Wafilipi 2:3-4, "Msitende neno lolote kwa kushindana wala kwa majivuno, bali kwa unyenyekvcu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake".***

***24) Wakolosai 3:9-10," Msiambiane uongo, kwa kuwa mmeuvua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake. Mkivaa utu mpya , unaofanywa upya upate ufahamu sawasawa na mfano wake yeye aliyewaumba".***

***25) Wakolosai 3:13, "Mkichukuliana, na kusameheana , mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo hivyo na ninyi".***

***26) Wakolosai 3:16, " Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote mkifundishana kwa zaburi, na nyimbo na tenzi za rohoni, huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu.***

***27) 1 Wathesalonike 4:18, "Basi farijianeni na kujengana kila mtu na mwenzake, vile vile kama mnavyofanya".***

***28) 1 Wathesolonika 5:11," Basi farijianeni na kujengana kila mtu na mwenzake , vile vile kama kama mnavyofanya".***

***29) Waebrania 3:13, " Lakini mwonyane kila siku , maadamu iitiwapo leo , ili mmoja wenu asifanye moyo mgumu kwa udanganyifu wa dhambi".***

***30) Waebrania 10:24-25, "Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri. Wala tusiacha kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri tuonavyo siku ile kuwa inakaribia.***

***31) Yakobo 5:9, "Ndugu, msinungunikiane, msije mkahukumiwa. Angalieni , mwamuzi amesimama mbele ya mlango".***

***32) Yakobo 4 :11,« Ndugu msisingiziane ; amsingiziaye nduku yake , au kumhukumu ndugu yake , huinsingizia sheria na kuihukumu sheria .***

***33) Yakobo 5 :16, « Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana , akiomba kwa bidii ».***

***34) 1 Petro 1 :22, « Mkiisha kuitakasa roho zenu kwa kuitii kweli , hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo ».***

***35) 1 Petro 3 :8, « Neno la mwihso ni hili, mwe na nia moja, wenye kuhurumiana, wenye kupendana kama ndugu, wasikitikivu , wanyenyekevu ».***

***36) 1 Petro 4 :8-9, « Zaidi ya yote iwe na juhudi nyingi katika kupendana ; kwa sababu upendano husitiri***

***wingi wa dhambi . mkaribishane ninyi kwa ninyi , pasipo kunung'unika ».***

***37) 1 Petro 4 :10, « Kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama , itumieni kwa kuhudumiana, kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu ».***

***38) 1 Petro 5 :5 , « vyo hivyo ninyi vijana , watiini wazee. Naam , ninyi nyote jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana ; kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi lakini hawapa wanyenyekevu neema.***

***39) 1 Yohana 1 :7, « Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi na damu yake yesu , mwana wake , yatusafisha dhambi.***

***40) 1 Yohana 3 :11, « Maana , hii ndyo habari mliyoisikiya tangu mwanzo, kwamba tupendane sisi kwa sisi ».***

***41) 1 Yohana 3 :23, « Na hii ndyo amri yake, kwamba tuliamini jina la mwana wake Yesu Kristo na Kupendana sisi kwa sisi, kama alivyo tupa amri ».***

**APPENDICE 4 :**

**HUDUMA YA WAKATI WOTE NA PESA KATIKA AGANO JIPYA ;**

Katika maeneo Fulani ya wakristo " huduma ya kumtumikia Mungu kwa wakati wote " inaabudiwa sana kiasi cha kuitamani kwa gharama yoyote ile. Nia iliyo nyuma ya tamaa hiyo ni yenye uharibifu kwa mwili wa Kristo.

Sanamu huyu anayeabudiwa ameingiza mchanganyiko ndani ya maisha yetu kana kwamba huduma ya kikristo ni kazi ya " kiroho" ao "takatifu" wakati ambapo kazi nyingine yeyoye ile ni ya "dunia" ao "ya " ulimwengu " . Ni kuchanganikiwa kwa dini na haihusiani na vile tunavyoelewa Agano jipya wala Namna tunavyoutizama ulimwengu.

Paulo anafundisha kwa **wakolosai** waliotumika kama watumwa kwenye **sura ya 3 mstari wa 22-24"** ***Ninyi watumwa , watiini hao ambao kwa mwili ni Bwana zenu, katika mambo yote, si kwa utumwa wa macho , kama wajipendekezao kwa wanadamu, bali kwa unyofu wa moyo, mkimcha Bwana. Lolote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa Bwana, wala si kwa wanadamu, mkijua ya kuwa si kwa wanadamu, ujira wa urithi mtapokea kwa Bwana ujira wa urithi. Mnamtumikia Bwana Kristo."***

Ni kiini cha Agano jipya maana sisi sote tu makuhani wa ufalme mmoja , katika **Wagalatia 3:26-28** ***"kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani Yesu. Maana mmenvaa Kristo. Hapana nyahaudi wala***

***nyunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika kristo Yesu."***

Kondoo na mbuzi sio dhabihu tena. Tumekuwa dhaibu iliyo hai (**Warumi 12:1-2)** na hivo licha ya hayo maisha yangu ya kila siku ni dhabihu yangu kwake. Hakuna ubaguzi kati ya kilicho kiroho wala kilicho takatifu na kilicho najisi wala kilicho kiroho wala kilicho cha dunia. Kristo ameyakomboa maisha yangu? Licha ya yale tuyatendayo, tunayatenda kwa ajili yake na kutoa hivo dhabihu yetu ya kila siku.

Wengi hufanya huduma kwa ajili ya pesa , wengine ili waonekane na kutafuta cheo. Huduma sio utu wetu. Yesu hapokei kamwe huduma ya namna hiyo kama dhabibu inayokubalika. Silo linalotendeka ndilo linamaanisha kinachokubalika kama dhabibu iliyo hai. Bali ni moyo ambao kwa huo unatenda na ni kwa nani unatoa . Dhawabu inatolewa kutokana na uaminifu katika mwito. Kumhudumia aliye mdogo sana ni kumhudumia Yesu. Ufalme wa mbingu ni ufalme uliopinduka, ambamo wa kwanza atakuwa wa mwisho na wa mwisho atakuwa wa kwanza. Kwa hiyo Yule asiye fahamika anayemtumikia kwa uaminifu aliye mdogo sana anaweza kupata dhawabu kubwa kuliko mnenaji anayefahamika sana kwenye kongamano na ambaye vitabu vyake vimevutia wengi.

Kazi yeyote inayostahili ni huduma , nani basi aliye na huduma muhimu mnenaji ao mpishi? Mnenaji wala yule ananyeosha Gari? Mnenaji wala anayeendesha Gari? Bila wapishi waosha

choo na waendesha gari, hapangekuwapo na semina yeyote. Sisi ni mwili wa Kristo. Sote tu makuhani wa ufalme na bila huduma yetu ya mmoja kwa mwingine na kwa Yesu ufalme hauwezi kuendelea kamwe.

Yesu anataka Uzima wake uonekane katika kila sehemu yenye bidii ya mwanadamu ili waone jinsi neno limefanyika mwili !.

**A) Hata hivo Agano jipya linaeleza sana kuhusu wale wanaohubiri injili kuwa ni " haki" yao na kwamba haki yao hiyo imeamriwa na Bwana:**

***1) Luka 8:1-3, " inatueleza kuwa Yesu na wanafunzi wake walisafiri bila kuwa na haja ya chochote kwa sababu ya kundi moja la wanawake lililowahudumia na vitu vyao.***

***2) Mdo 6: 1-7 inatueleza kuwa kundi la mitume na vile vile pia mashemasi walihudumia kwenye meza wakisaidiwa na msaada wa kanisa lote.***

***3) 1 Wakorentho 9:1-14 inaeleza kuhusu haki ya wale wapandao vitu vya rohoni wanastahili kupokea vitu vya mwilini na kumalizia kwa kusema kuwa Bwana aliamuru wale wanaohubiri injili waishi kwa injili ndivyo alivyotenda Yesu na kuamuru kama kawaida kwa wale wanaosafiri kama yeye na Paulo kwa kuhubiri habari njema ya ufalme wa mbingu.***

***4) 2 Wakorintho 11:9 ni ushuhuda wa Paulo wa jinsi mahitaji yake , wakati alipokuwa korintho yalito***

***shelezwa na ndugu wa makedonia alitumia haki yake ya kuishi kwa injili.***

5) ***Wafilipi 4:10-15 anawasifu wafilipi kwa uaminifu na kuwashukuru kwa waminifu na kuwa shukuru kwa namna walivyo kuwa wapekee niongoni mwa makanisa yote , waliokuwa tayari kushiriki pamoja naye kwa kutoa na kupokea.***

6) ***1 Timotheo 5:17-20 inaeleza juu ya kuwaheshimu maradafu wazee watawalao vema hasa wale wanao hudumu kwa mahubiri na mafundisho.*** Labda tungesema kuwa hii ina maanisha kutoa mshahara mkubwa kwa wachungaji wa mahali. Mniruhusu turudi kidogo kwenye Luka 10. Kwa nini kundi ambalo hukutana nyumbani lingehitaji wala kutamani kutoa mshahara kwa Askofu/mchungaji/mzee/mwangalizi wao? Kwa nini wangetamani kutenda hivo? Tukiwaona wazea kama viongozi wa makanisa ya nyumbani walio tenda kazi nzuri pamoja na familia zao na wanaotambuliwa kama wanaostahili kuhudumu kwa makanisa yao ya nyumbani. Wanasafiri ili kutoa mashauri, kufundisha na kusaidia kuanzisha makanisa mapya ya nyumbani. Kama watumishi hao wanavyosafitri, hawana uwezo tena wa kuzitenda kazi zao na ndipo wanapashwa kutumia haki yao ya kuishi kwa injili.

Badala yake mojawapo ya tabia za kanisa la nyumbani zinazokua haraka ni kule kujitegemea kwa viongozi wa mahali na mara nyingi ao mara haba, ni kujitosheleza kwa viongozi wanaosafiri pia viongozi wanaotesheleza

mahitaji yao. Ikiwa unaonekana kama mtu anayestahili kulipwa ili unene unayopaswa kunena, maneno yako yatajaa mamlaka ya kinidhamu peke yake. Unastahili kuamini unayoyasema ! Dhidi ya hapo kazi inayokuruhusu kutosheleza mahitaji yako inakutunza katika ulimwengu wa kawaida ambapo ndyo mahali pa mavuno.

Baadhi ya viongozi wengi ni wapweke wamefungwa ndani ya maeneo yao ya ghetto za kikristo. Wanaongea kati yao tu, wanaongoza kwa nyaraka, ina maana wanaeleza jmabo fulani,wanatenda kwa ajili yao kitu hicho hicho. Hawawajibiki katika maisha ya kawaida (hawajihusishi) na wana hukumiwa kwa matunda yao.

**Paulo ni mfano wa viongozi wanaotosheleza mahitaji yao.**

A) Mfano wa Paulo na mafundisho kuhusu sababu iliyomfanya akatae kutumia haki yake ya kuishi kwa injili….

***1) Matendo 20:26-35*** ni historia ya hotuba ya mwisho ya Paulo kwa wazee wa efeso anawapa changamoto kuhusiana na mafundisho yake na mfano wake

Anatangaza kuwa hakutamani kitu cha mtu yeyote , alitumika kwa mikono yake mwenyewe kutosheleza mahitaji yake na kwa wale aliokuwa pamoja nao. Na anaendelea kusema ***“ ninyi wenyewe mnajua ya kuwa mikono yangu hii imetumika kwa mahitaji yangu na ya wale waliokuwa pamoja nami”,*** na kwamba kwa kutumika hivyo tunawasaidia wasiojiweza na kuyakumbuka maneno ya Bwana aliyoyasema mwenyewe. kuwa« ***Kuna heri katika kutoa kuliko kupokea”.***

Anatoa maisha yake kama mfano na kielelezo kwa wale watakaowaongoza wengine kumfwata Yesu. Anataraji kuwa wazee wa Efeso wataufwata mfano wake na watumike kama alivyotenda yeye. Ni mfano kwa ajili ya wazee wote daima. Na pia mashairi haya kuhusu pesa , ni mashairi ambayo hutayasikia popote pale kwenye kongamano!

1) **1 Wakorintho 4:12** inaeleza kuwa tunachoka kutumika kwa mikono yetu Paulo anaonyesha hayo kama alama ya "upendo wake na ya ulinzi wake kwa wakorinto kama vile alama ya mzazi kwao.
2) **1 Wakorintho 9:1-19** ni kifungu ambacho ndani yake Paulo anaeleza namna mitume wengine wanatumia hadi yao ya kuenenda na mwanamke na kuishi kwa injili. Anatangaza mara tena nkuwa yeye na barnaba hawakutumia haki yao katika injili, lakini walikuletea kutumika kutosheleza mahitaji yao na hata kutokuwa sababu ya kuleta kizuizi chochote kwa injili ya Kristo. Ni jinsi gari kukubali pesa za wakorinto ingezuia injili? Kwa urahisi sana , wangemshitaki kuja kwao kwa matumaini ya kupata kitu toka kwao.
3) **2 Wakorintho 11:7-9,** inaeleza sehemu ya mamlaka ya kiridhamu ya Paulo juu ya wakorinto, kwa maana aliwahubiria bure na akajizuia kuwa mzigo kwao.
4) **2 Wakorintho 12:13** inatukumbusha mara tena jinsi Paulo, alivyojizuia kuwa mzigo kwa wakorintho.
5) **2 Wakorinto 12:14** irudilia tena juu ya kutokuwa mzigo, " sio kwa ajili ya watoto , kukusanya kwa ajili ya wazazi wao, bali wazazi kwa watoto" wanaojiita "Baba-mitume"

na wanaofundisha kuwa watoto wao wanapashwa kuwatolea fungu la kumi hawajasoma Biblia yao na wanafahamika kwa hali yao ya kupenda pesa. Sio mitume kama alivyo kuwa Paulo. Kulingana na Paulo, mituma hao ni mitume wa uongo.

6) **2 Wakorinto 12:17-18,** inaturuhusu kuelewa kuwa wale waliokuwa katika timu ya Paulo walitembea kama yeye kuhusiana na maswala ya Pesa.

   Mara nyingine kiongozi wa huduma hatazungumzia kuhusu pesa , bali atamruhusu mtu mmoja wa timu yake kutenda hilo na alionyesha timu yake yote kuzingatia msimamo wake kuo.

*7)* **2 Wathesalonike 3:6-12** ni maelekezo rahisi. Paulo anawashauri kujitenga na kila aitwaye ndugu asiye enenda kwa utaratibu , akimaanisha mtu asiyetumika ! mfano wake wa kutumika unaungwa mkono licha ya kuonyesha haki yake ya kuishi kwa injili na anawaomba kuufwata mfano wake. Kwa kifupi ? ***« asiyetumika na asile ».***

**Mitume wa uongo na manabii wanafahamika kwa kupenda pesa….**

Paulo alikuwa mkali sana alipowakemea mitume na manabii wa uongo kwa , ajili ya nia yao mbele ya pesa. Katika hali hii, haishangazi kuona kuwa alikuwa na msimamo mkuu juu ya kufanya kazi na alionyesha mfano kwa viongozi wengine.

Yesu aliwalaumu viongozi wa kiyaudi kwa kupenda pesa , cheo na heshima. Aliwalaumu maana waliweka mizigo juu ya

mabega ya watu ambao wao wenyewe hawawezi kuichukua hata kwa incha ya kidole **(Mathayo 23:4)** na sehemu ya mzigo huo ilikuwa ni kutamani pesa.

Mbinu zote za ukuhani na za hekalu ulimwenguni huweka mzigo mzito wa pesa kwao wale wanaowaendea.

Dini inanyanyasa daima watu na maskini , ili kupata pesa. Paulo kakutamani kuwa miongoni mwao, na sawa na Yesu, ni wazi kuwa hakika anawalaumu wale waliokuwa wakifanya huduma kwa ajili ya Pesa. Katika kutumika usikuna mchana ili kutosheleza mahitaji yake aliamua kujitofautisha na wale ambao nia yao ilikuwa tamaa ya pesa. Alitamani kuteswa kuliko kushitakiwa na mtu yeyote kuwa anauza neno la Mungu. Ikiwa hilo ni kweli kwa wakati wa Paulo, ni mara ngapi zaidi leo, ambako ulimwengu hufikiria kuwa kila kiongozi wa kikristo hutenda huduma kwa ajili ya pesa. Tunatoa matangazo ya vitabu, tunauza vitu mbalimbali vya Biblia na tunaeleza uongo tukiaidi watu kubarikiwa mara mia ikiwa tu kama watatoa. Na yote hayo hufanyika na watu wanaovalia saa za bey ghali aina ya Rolex na suti za aina yake. Lakini hata hivo neno la Mungu haliuzwi.

1) ***2 Wakorinto 11:13-20***, Paulo anasema moja kwa moja kwa mitume wa uongo. Paulo anawalaumu wakorinto kuchukuliana na mwenendo wao unao- kwaza. Ikiwa kuna mtu yeyote aliyewafanya watumwa ,ikiwa kuna mtu aliyewararua, ikiwa kuna mtu aliyewashikilia , ikiwa kuna mtu mwenye kiburi , ikiwa kuna mtu aliyewapiga kwenye uso, wanavumiliana na naye . Ni

mitume wa uongo wanawaleta watakatifu chini ya utawala wao, wanawadanganya ili kupata pesa na kuwatumia ili kujenga falme zao ndogo.

2) ***1 Timothoe 6-3:10.*** Paulo anamweleza timoteo kuhusu waalimu wa uongo wanaodhani kuwa utakatifu ndyo chanzo cha kupata pesa. Na amri yake kwa watakatifu ni nini wanopokutana na waalimu hao wa uongo ? wakimbieni. Kwa namna hii tunastahili kuwa mbali na baadhi ya wale wanaohubiri kwenye Televisheni na wale wote wanaohubiri mafanikio kama alama ya utiifu na uaminifu.

3) ***Tito 1:11*** Paulo anafundisha tito kuwa kutakuwepo na waalimu wa uongo ambao vinywa vyao vinastahili kufungwa , wanaopindua nyumba nzima, wakifundisha juu ya mapato ya aibu, yasiyopashwa kufundishwa. Hao wachungaji wa televisheni hutumia Biblia. Ndyo wanajiita wakristo . ndyo wana dalili za kufanikiwa. Lakini Paulo anasema kuwa vinywa vyao vinapashwa kufungwa. Kwa nini? Kusudi kubwa la yote wayatendayo ni kupata pesa.

4) ***1 Petro 5:2-3,*** ni mwito kwa wachungaji kutumikia taifa la Mungu walio chini ya uangalizi wao, sio kwa kuwalazimisha bali kwa hiari, kulingana na Mungu, sio kwa ajili ya mapato ya aibu, lakini kwa moyo , sio kama watawalao juu yao , bali kama walio vielezo kwa kundi. Mara tena kupenda pesa na mamlaka vinaharibu hali yetu ya kuongoza. Inafwatiwa na tangazo la ajabu lisemalo kuwa Mungu huwapinga wenyi kiburi, lakini huwapa neema wanyenyekevu. Mungu huwapingaje

wenye kiburi? Neno hilo laweza kusomwa namna hii " hushindana na wenye kiburi ". Sitamani Mungu ashindane nami !

5) ***2 Petro 2:3 na 14*** ni vifungu vya Biblia vinavyoeleza wazi wazi juu ya kuchukuliwa na tamaa ya pesa. Inatembeaje? Kiongozi mmoja ana kiasi Fulani cha magari wala vifaa vya ofisini na mwingine pia anatamani, kuwa hivo. Hali kama hii haipanui injili " ni uongo , ni tama ya Pesa.

Wakati viongozi maarufu wa kikristo ndyo wanaohusishwa mmoja kwa moja kwenye mambo ya ufisadi , rushwa na ngono , ni wazi kuwa , Mungu huwapinga wenye kuburi. Huruhusu utatu wa ubaya kupata kile wanachotaka. Kwanza kuna kiburi cha uzima, kiburi cha cheo, mafanikio na karama.sasa ndipo tama ya macho inapoanza kutoshelezwa. Tunaweza kupata tunayotamani. Kutumia vibaya pesa za watoto wa Mungu kwa kuendesha maisha ya aina ya viongozi wa ngazi ya juu. Ndipo huja tamaa ya mwili na dhambi ya ngono **(Mithali 22-14)** nikitamani kupata kile nikipendacho, kwa nini sasa mwanamke huyu wala mume Yule:

Wakati Paulo anapomjulisha Timoteo ni uhusiono wa aina gani angekuwa nao na wazee katika ***1 Timoteo 5:17-21*** aliona ni haki kupokea mashitaka juu ya Mzee na kuwaonya walio katika dhambi. Mashitaka yasingelitokea kwa mtu mmoja tu peke yake. Lakini kwa viongozi hawa

wapatikanao wakitenda dhambi , Thimoteo alipashwa kuwaonya mbele ya wote , ili wengine waogope.

Tuanona mara kwa mara dhambi ya ajabu miongoni mwa viongozi maarufu inayofunikwa na walio kando kando yao na hata wale walio katika huduma pamoja nao. Yeyote anayetaka kuwaonya na kuwadhibu kwa sababu ya uchu wao wa pesa wanamwambia kuwa ana roho ya dini, umaskini na ya kuwahukumu wengine. Ukitaka kuwaonya juu ya dhambi yao ya ngono, wanasema eti hatuna huruma yoyote, kuwa sisi sio wakombozi na mwishowe kuwa ulimwengu unahitaji karama ya wale walioanguka ili pawepo na kuhuhishwa. Hamna kukemea wala woga: : kuna kuhesabiwa haki maonyesho yanayoendelea.

Baadhi ya " vyombo vya habari vya kikristo: vinafanya vizuri sana vinapowapa watu fursa ya kueleza yale wasingelieleza jau nya kupat faida haramu lakini zaifu sana inapokuwa kufanya wanafunzi. Vyombo vya habari vina fanya vema sana katika kuanzisha mikutano ya kutafuta pesa, lakini zaifu sana katika kufanya wanafunzi wanaajitolea kwa yesu. Yesu alkabidhi huduma ya uzima wake wote kwa wanafunzi kumi na wawili na aliwaamini kuzidishi uzima wake huo ndani wa kutebda viovyo hivyo. Hatuwezi kubiresha ntindo wake. Neda na utende vivyo hivyo.

### 3) Kushughulikia maskini katika Agano jipya.

Tunaeleza kuhusu ukweli kuwa Yesu alijilinganisha kwa unamilifu na maskini na kusema kuwa kinachotendwa kwa aliye mdogo ni kwake yeye kimetendwa.

**Mathayo 25 na Isaya 58** vingekuwa vifungu vya msingi kwa maisha yetu , kama ilivyokuwa kwa Kanisa la Kwanza . Sababu mojawapo ya kukua kwa haraka kwa kanisa la kwanza ilikuwa ni matendo yao ya kuwapokea watoto wachanga walioachwa kwenye barabara za ufalme wa kizumi na kuwalea kama watoto wao.

***Yakobo 1:27, " Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu baba ni hii, kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, ao kujilinda na dunia pasipo mawaa.***

***Matendo 6:1, " hata siku zile wanafunzi walipokuwa wakuingeza ka hesabu yao, palikuwa na manunguniko ya wa yahidi wa kiyunani juu ya waebrania kwa sababu wajana wao walisahauliwa katika hudumua ya kila siku".***

***1 Timotheo 5:3, " Wakeshimu wajane , walio wajane kweli".***

***1 Timotheo 5:16, " Mwanamke aaminiye, akiwa ana wajane , na awa saidiwe mwenyewe, kanisa lisilemewe, ili wasaidie walu walio wajane kweli".***

Mashemasi wanawakilisha wale wanaosimamia kazi za matendo mema ya mwili wa Kristo. Walishughulika na namna ya kusaidia , kufahamu ni kwa nani kupeleka msaada, kuchagua miongoni mwa waliofanya maombi, kwa maana kuna wale ambao kabisa hawakuitaji msaada.

Wasi wasi huu kwa maskini ndyo maelekezo ya pekee ya kifedha iliyotoka kwa baraza la Yerusalemu katika ***Mdo 15*** na hadisi hailezi lolote kuhusu fedha.

Tunafahamu haya kutoka ***Wagalatia 2:10, " ila neno moja tu walitutakia, tuwakumbuke maskini; nami neno lilo hilo nalikuwa na bidii kulifanya...".***

Hata hivo ni changizo ya makanisa kusaidia watakatifu wa Yerusalemu wakati wa njaa inayotupatia picha ya wazi ya jinsi Paulo alivyofikiri kukusanya pesa za kusaidia maskini.

***1 wakorintho 16 : 1-2, " Kwa habari ya ile chnagizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia nanyi fanyeni vivyo hivyo.Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake; kwa kadiri ya kufanikiwa kwake ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja "***

Kwanza kabisa mchango uliamriwa lakini hapakuwepo na kiwango wala kiasi Fulani kilichodaiwa. Kila mtu alitoa kulingana na vile alivyobarikiwa.

Jambo la pili fahamu kwamba Paulo alitamani kwamba Mchango ufanyike na kukamilika kabla hajafika. Wachungaji wetu wengi wa mafanikio wanapenda kuchukua sadaka zao wenyewe.Kwa

nini ? Wanajihusisha kwenye uwezo wao wa kuvutia watu ili watoe.. Paulo hakutaka kutumia ujanja wala mtindo huo wa aina yeyote ule . Katika hali ya utulivu moyoni mwao mbele za Mungu,watu walipashwa kuamua wenyewe ni nini wangetoa . Alionyesha imani yake katika Roho mtakatifu ili kusema na taifa la Mungu.

***2 wakorintho 8 : 1- 8, " Tne Ndugu zangu twaarifu habari ya neema ya Mungu waliyopewa makanisa ya makedonia, Maana walipokuwa wakijaribiwa kwa dhiki nyingi,wingi wa furaha yao na umaskini wao uliokuwa mwingi uliwaongezea ukarimu wao.Maana nawashuhudia kwamba, kwa uwezo wao, na zaidi ya uwezo wao, kwa hiari yao wenyewe walitoa vitu vyao.wakituomba sana pamoja na kutusii kwa habari ya neema hii, na shirika hili la kuwahudumia watakatifu, tena walitenda hivi si kama tulivyotumaini tu,bali kwanza walijitoa nafsi zao kwa Bwana na kwetu pia,kwa mapenzi ya Mungu.Hata tukamwonya Tito kuwatimilizia neema hii kwenu kama vile yeye alivyotangulia kuianzisha. Lakini kama mlivyo na wingi wa mambo yote, imani, na usemi,na elimu na bidii yote,na upendo wenu kwetu sisi; basi vivyo hivyo mpate wingi wa neema hii pia.Sineni ili kuwaamuru,bali kwa bidii ya watu wengine nijaribu unyofu wa upendo wenu. "***

Sadaka ilielekea kwa watakatifu na ushirika wa huduma kwa watakatifu ulitokana na kujitoa kwingi na furaha. Ni vigumu kuwa na furaha ikiwa inabidi kulipa mshahara wa mwandishi,

bili ya zamu ili uendelee kuliendesha Jengo . Ni Jambo lingine kufahamu ushirika wa kujitolea kwa ajili ya Ndugu na Dada.

***2 wakorintho 8 : 13 – 15, " Maana sisemi hayo, ili wengine wapate raha nanyi mpate dhiki ; bali mambo yawe sawasawa wakati huu wingi wenu uwafae ninyi mtakapopungukiwa; ili mambo yawe sawa sawa. Kama ilivyoandikwa, aliyekusanya vingi, hakuzidi wala aliyekusanya vichache, hakupungukiwa.***

Ushirika huo wa kuwahudumia watakatifu ulikuwa wa halali na jibu kwa mahitaji ili mahitaji yetu itoshelezwe hapo baadaye. Tunaonaje? Wajibu wetu mbele zao? Ni jinsi gani lile wazo la usawa linaingia kwenye mafikiri yetu? Ni vipi ? kuelewana kwa mmoja na mwingine kunaweza tekelezwa hapa ?

Wachunagji wengi maarufu huonyesha utajiri wao na hali yao ya kuishi ili kudhihirisha kibali cha Mungu na kuhakikisha ujumbe wa kuwadanganya watu ili watoe zaidi maana wamekuwa « Udongo Mzuri « wa kupanda mbegu yao ya pesa kwa matumaini ya kuvuna Pesa. Wanaonyesha hali ya ubaguzi na kuchekelea maskini kama ni « udongo mbaya » ambamo kupanda Pesa ni uongo mtupu.

Mungu anasema kwamba ***« maskini wa ulimwengu huu ndyo matajiri wa imani na warithi wa ufalme aliwaahidia wampendao ». (Yakobo 2 : 5 ) .***

**Mithali inasema** ***« Amhurumiaye maskini humkopesha Bwana.Naye atamlipa kwa tendo lake jema « (Mithali 19 :17)***

***2 wakorintho 9 : 1, «  Kwa habari ya kuwahudumia watakatifu sina haja ya kuwaandikia. »***

Sadaka zilikuwa kwa ajili ya watakatifu, na wala si kwa ajili ya viongozi. Hata katika kitabu cha matendo ya Mitume tunaona kuwa sadaka ziliwekwa miguuni pa mitume, Lengo kuu la sadaka lilikuwa ni kushughulikia watakatifu zaidi sana wajane na mayatima. Sadaka hazikutumiwa ili wanaoongoza wawe na maisha bora.

***2 wakorintho 9 : 5, « na hivi iwe kama kipawa, wala si kama kitu kitolewacho kwa unyimivu… »***

Msaada katika gano Jipya unastahili kutendeka kwa hiari na wema na kamwe si kwa kulazimishwa. Agano Jipya ni Agano la Moyo linalotoka kwa Mungu,lililo kama Mungu, moyo wa ukarimu. Je ? Tuna imani na ukarimu kwa Mungu kwa watu wake ? wala  hapana ?

***2 wakorintho 9 : 6, «  Lakini nasema neno hili, apndaye haba atavuna haba, apandaye kwa ukarimu atavuna ukarimu. «***

Ahadi ya kupanda na kuvuna hutendeka wakati ambapo sadaka kwa ajili ya maskini inatekelezwa na sadaka hiyo husababisha mavuno yenye neema kuu, kuzidi sana katika kila tendo jema.

***( 9 : 8) kuzidisha mbegu mliyopnda na kuongeza matunda ya haki yenu.***

***( 9 : 10 ), Amabye kwa njia yake, yatatoa shukurani kwa Mungu. (9 : 11 ), Wanamtukuza Mungu kwa ajili ya utii***

***wenu katika*** kuikiri injili ya kristo, **(9 : 13** ) na kuongeza maombi yao kwa ajili yenu **( 9 : 14 ).**

Shukurani, maombi na utukufu wa Mungu zinatajwa kama zinazozidishwa kama vile mbegu ya kupanda upya siku zijazo.

***Yakobo 2 : 5 , « ndugu zangu wapenzi, sikilizeni, Je ! Mungu Hakuwachagua maskini wa Dunia hii wawe matajiri wa Imani na warithi wa ufalme alio waaidia wampendao ? »***

Yakobo anaadhibu kanisa kwa kuwapendelea matajiri na anaonya ya kwamba kwa kutenda hivo ni kuonyesha upendeleo na kuwa waamuzi wenye mawazo mabaya. Kawaida ni kwamba umpende Jirani yako kama nafsi yako. Tunauliza daima swali hili, « Nani jirani yangu ? « . Ni swali pana katika ulimwengu huu ambamo tunafahamu mateso ya watu wengi. Ni swali kuu katika kila mji ambamo unamfahamu mtu amayeishi karibu nawe, kwenye mtaa wako. Yakobo ansema nini kwa Mwisho ?

***Yakobo 2 : 15 – 17. « Ikiwa ndugu Mwanaume au mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki, na mtu wa kwenu akwaambia, enendeni zenu kwa amani makaote moto na kushiba, lakini asiwape mahitaji ya mwili yafaa nini ?. Vivyo hivyo na Imani , isipokuwa ina matendo imekufa nafsini mwake. «***

Agano Jipya halifahamu lolote kuhusu sadaka ya kujenga majumba na kuishi maisha yenye fahari. Lililo muhimu ni watu na jambo lililo la msingi ndilo lililo muhimu kwa mwalimu anaposema kwamba, **Tunayotenda kwa mojawapo wa wadogo , ni kwake yeye tunatenda.**

**Steve na Marilyn Hill**

Steve@harvest-now.com

**www.harvest-now.org**